BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Tatu – Tarehe 21 Aprili, 2016

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo ni Kikao cha Tatu cha Mkutano wetu wa Tatu, Katibu.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea nimepokea barua ambayo inatoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ikisema kwamba, atakuwa nje ya Dodoma leo siku ya Alhamisi, tarehe 21 Aprili, 2016. Kwa hiyo, shughuli za Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa siku ya leo zitasimamiwa na Mheshimiwa William Lukuvi ambaye tunamwona yuko pale. *(Makofi)*

Katibu!

MASWALI NA MAJIBU

Na. 21

Maafa Yaliyosababishwa na Mvua
ya Tarehe 3 Machi, 2016

MHE. EZEKIEL M. MAIGE aliuliza:-

Mvua ya theluji ilionyesha terehe 3 Machi, 2015 ilisababisha maafa makubwa ambapo familia zilikosa makazi na Mheshimiwa Rais wakati huo aliwaahidi wahanga wa maafa hayo kuwa Serikali itasaidia kujenga nyumba 343:-

(a) Je, ni nyumba ngapi hadi sasa zimejengwa katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais?

(b) Je, ni kiasi gani cha pesa kinahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi hiyo?

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha na misaada ya kibinadamu ya aina nyingine iliyotolewa na Serikali katika kukabiliana na janga hilo?

NAIBU WAZIRI WA SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. DKT. ABDALLAH S. POSSI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolya Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa nyumba mbili za mfano kwa lengo la kujua gharama halisi za ujenzi wa nyumba zilizoahidiwa na Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, jumla ya Sh.2,500,000,000 zinahitajika kugharamia ujenzi wa nyumba hizo. Gharama hizi zimepatikana baada ya kukamilika kwa tathmini ya gharama za ujenzi wa nyumba moja moja.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na maafa haya Serikali ilitoa huduma za dharura za malazi, makazi ya muda na matibabu. Misaada mingine iliyotolewa na Serikali ni pamoja na mahindi tani 100.4, Sh.45,290,045 kwa ajili ya ununuzi wa maharage, mafuta ya kupikia na usafirishaji wa mahindi. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mfuko wa Maafa ilitoa Sh.10,000,000 kwa ajili ya mahitaji mbalimbali.

SPIKA: Mheshimiwa Maige swali la nyongeza.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ya kweli. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kumekuwepo na malalamiko mengi sana kutoka kwa wananchi wa Mwakata walioathirika na hiyo mvua ya tarehe 3 mwaka jana kwamba usimamizi wa misaada mbalimbali nje ya ile iliyotoka Serikalini umekuwa na harufu mbaya, umekuwa na dalili za ufisadi. Nataka kujua Serikali iko tayari kufanya uchunguzi maalum wa Kiwizara ili kujua misaada yote iliyokusanywa na jinsi ambavyo ilitumika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, maafa haya yalikuwa na madhara makubwa sana kwa wananchi wanaoishi kwenye nyumba za tope. Serikali katika Ilani yake inayoitekeleza sasa hivi moja ya mkakati ni kujenga nyumba bora kwa maana nyumba za saruji. Nataka kujua Serikali imefikia wapi katika kupunguza ushuru wa vifaa vya ujenzi hasa simenti na kuweka *standardization* ya bei ili wananchi wanaoishi upande wa Magharibi mwa nchi yetu ambako hakuna viwanda na huipata bidhaa hiyo kwa gharama kubwa waweze kuipata kwa bei rahisi ili waweze kujenga nyumba bora na kuepuka majanga kama haya ambayo yanaweza yakawa yanajirudia endapo nyumba zitaendelea kutokuwa na ubora?

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa kwa maswali yako mawili. Majibu ya maswali hayo kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi!

NAIBU WAZIRI WA SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. DKT. ABDALLAH S. POSSI): Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ni kwamba Serikali ipo tayari siyo tu kufanya uchunguzi, lakini kuhakikisha kwamba kuna usimamizi wa karibu wa misaada yote inayotolewa kwa ajili ya kuwasaidia waathirika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali kupitia Wizara husika na nafikiri Waziri yupo, zinatekeleza mikakati maalum ya kuhakikisha kwamba Watanzania wana uwezo wa kujenga nyumba kwa gharama nafuu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge kijana kuliko wote, Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 22

Ajira kwa vijana.

MHE. HALIMA A. BULEMBO aliuliza:-

Nchi ya Tanzania ni moja kati ya nchi zenye vijana wengi, asilimia 72 ya Watanzania wapo kwenye umri chini ya miaka 29 kwa mujibu wa taarifa ya Taifa ya Takwimu ya 2013 na ajira kwa vijana hao ndiyo suluhisho la kuhakikisha kuwa vijana wanalihudumia Taifa lao:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha vijana wawe wajasiriamali kwa kuwapa mitaji, mikopo na ni vigezo gani vitakavyosimamia na kuwalinda na kuweka usawa wa upatikanaji wa ushiriki wao katika fursa hizo?

(b) Je, ni lini ahadi ya Sh. 50,000,000 kwa kila kijiji itatekelezwa na vijana watapata mgao wao wa asilimia ngapi?

NAIBU WAZIRI WA SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa vijana wanakuwa wajasiriamali na wanaweza kupatiwa mikopo na mitaji, Serikali imejiwekea mikakati ifuatayo:-

(i) Kutambua vijana na mahitaji yao katika ngazi mbalimbali;

(ii) Kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa makundi mbalimbali ya vijana; na

(iii) Kutekeleza mkakati wa Kitaifa wa kukuza ujuzi nchini ambao umelenga kutoa mafunzo ya vitendo maeneo ya kazi kwa wahitimu hususani wa vyuo vya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati hiyo yote, vigezo ambavyo vimekuwa vikitumika katika kutoa mikopo na mitaji kwa vijana ni umri usiozidi miaka 35; kujiunga katika *SACCOS* za Vijana za Wilaya na kuunda vikundi na kuvisajili kisheria.

(b) Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya Sh.50,000,000 kwa kila kijiji itaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha ujao yaani 2016/2017. Utaratibu wa kugawa fedha hizi unaandaliwa na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

SPIKA: Mheshimiwa Halima ameridhika, tunaendelea.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Hapana Mheshimiwa, nina swali la nyongeza. *(Kicheko)*

SPIKA: Mheshimiwa Halima swali la nyongeza.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara haijataja asilimia ngapi itakwenda kwa vijana wa kike na wa kiume; naomba Wizara ichukue ushauri wangu kwamba zile fedha zitakapopelekwa halmashauri waweze kusema asilimia kumi itakuwa kwa vijana wa kike na wa kiume na hii itapunguza mkanganyiko katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze katika maswali yangu mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Je, kwa nini Serikali isianzishe dhamana kwa vijana kukopa (*credit guarantee scheme for youth)*?

(b) Je, Serikali inaona kuna umuhimu wa kujenga mfumo madhubuti wa hifadhi ya jamii ili kuwezesha vijana kuweka akiba yao ya uzeeni, kupata bima ya afya na hata kuweza kupata mikopo katika biashara zao? *(Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

NAIBU WAZIRI WA SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE): Mheshimiwa Spika, katika eneo la kwanza la mikopo kwa ajili ya vijana, upo mpango wa muda mrefu na wa muda mfupi. Kwa sasa Serikali imeendelea kutoa mikopo kwa vikundi mbalimbali vya vijana kupitia katika *SACCOS* za Halmashauri lakini mpango wa muda mrefu ni kuja kuanzisha benki maalum ya vijana ambayo ndiyo itakuwa sehemu pekee ya vijana wengi kupata mikopo. Kwa hiyo, mpango wa muda mrefu ni uanzishwaji wa benki lakini tumeanza na *SACCOS* kwa ajili ya kuwajengea tabia vijana ya kufahamu masuala ya fedha kwa maana ya ukopaji na nidhamu ya urudishaji fedha.

Mheshimiwa Spika, la pili la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwashirikisha vijana, tayari katika programu mbalimbali za Mifuko ya Hifadhi za Jamii wamekuwa na eneo hili la kuwashirikisha vijana kupitia shughuli mbalimbali. Mojawapo ni Shirika la *NSSF* ambao tayari wameanzisha programu ambayo inaitwa *AA Plus* kwa maana ya Akiba na Afya kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, ambapo wanafunzi watachangia Sh. 20,000 kwa mwezi na watapata matibabu bure kwa muda wote ambao watakuwepo vyuoni lakini atakapohitimu mafunzo yake ya chuoni ile fedha anaweza kurejeshewa au akiamua ibaki

kama akiba basi anaendelea kuitumia ikiwa ni sehemu yake pia kumsaidia baadaye kupata mikopo akiwa mwanachama wa shirika.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa, swali la nyongeza.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii…

MBUNGE FULANI: Ni mimi hapa, mimi ndiyo Mbunge kijana. *(Kicheko)*

MHE. KASUKU S. BILAGO: Ni mimi hapa.

SPIKA: Ni huyo anayeongea, ahsante endelea.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Hii nafasi ni ya Mwalimu.

Mheshimiwa Spika, nina swali dogo kuhusiana na fedha hizi zinazotarajiwa kutolewa vijijini za Sh. 50,000,000 kwa kila kijiji. Sasa hivi imeanza mizengwe kwamba fedha hizi zitatolewa kwa wanachama wa Chama cha Mapinduzi. Naomba Serikali itoe kauli fedha hizi zitatolewa kwa utaratibu gani ili kuepuka kwenda kwa wanachama wa Chama cha Mapinduzi peke yao? Ahsante.

SPIKA: Hilo swali kweli hayo mambo yapo?

WABUNGE FULANI: Yapo.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niseme fedha hizi za Sh. 50,000,000 ilikuwa ni ahadi ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kupitia kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Watanzania ambao walichagua Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Serikali hii iliamua kuwatumikia Watanzania wote bila kujali itikadi ya vyama vyao wala jambo lingine lolote. Katika majibu yetu ya msingi tumesema Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Tanzania wameshaanza kutengeneza utaratibu wa namna ambavyo fedha hiyo ya Sh. 50,000,000 itaweza kuwafaidisha wananchi wetu kule vijijini wakiwemo vijana, wanawake lakini vilevile na Watanzania wengine wote. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mbunge jambo hilo analolisema ni hofu tu, lakini Serikali ipo imara na itazingatia utaratibu wa kisheria wa kuhakikisha fedha hizi zinawafikia Watanzania. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Tuendelee na swali linalofuata Waheshimiwa Wabunge.

Na. 23

Utaratibu wa Vijana Kwenda Kufanya Kazi Nje ya Nchi

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN aliuliza:-

Kuna idadi kubwa ya vijana wa Tanzania ambao wanafanya kazi nje ya nchi zikiwemo kazi za ndani (*house girls*):-

(a) Je, kuna utaratibu gani unatumika kwa vijana hao kwenda kufanya kazi hizo nje ya nchi?

(b) Je, vijana wangapi wanafanya kazi hizo nje ya nchi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuratibu ajira za Watanzania wanaokwenda kufanya kazi nje ya nchi, Serikali imeweka utaratibu wa kutumia Wakala wa Serikali wa Huduma za Ajira Tanzania *(TaESA)* na kurasimisha wakala binafsi wa huduma za ajira ambao wana jukumu la kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri wa ndani na nje ya nchi. Kabla wakala binafsi hajampeleka mfanyakazi nje ya nchi anapaswa kuwasiliana na *TaESA* kwa lengo la kuhakiki mikataba ya kazi na kupeleka taarifa za mfanyakazi kwa Balozi wetu katika nchi husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, sheria haikatazi Mtanzania kujitafutia kazi na kwenda kufanya kazi nje bila kupitia utaratibu huu. Hivyo, wapo baadhi ya Watanzania wanaokwenda nje kufanya kazi kwa utaratibu wao binafsi. Napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba wananchi wanaokwenda kufanya kazi nje ya nchi kufuata utaratibu mzuri uliowekwa na Serikali ambao utawawezesha kusaidiwa na Serikali hususani wakati wanapopata matatizo kupitia Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Watanzania wapatao 4,992 waliopitia utaratibu rasmi uliowekwa na Serikali kupitia *TaESA* wanafanya kazi nje ya nchi yetu ya Tanzania.

SPIKA: Mheshimiwa Yussuf, Mbunge wa Chambani, swali la nyongeza!

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Katika *paragraph* ya pili ya majibu yake ndiyo nitajenga maswali yangu ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, siku ya tarehe 9 Desemba, 2016, nilikuwa nasafiri kutoka Dubai kurudi Tanzania nikakutana na binti wa Kitanzania anaitwa Zuhura Yussuf Manda, mkazi wa Tegeta Kibaoni, Dar es Salaam. Binti alipelekwa kufanya kazi na *agent* wa Kitanzania anayeitwa Amne, akafanya kazi Oman kwa miezi mitatu kwa Anna na badala yake Anna akampa dada yake ambaye anaishi Dubai anaitwa Zahra akafanya kazi kwa muda wa miezi mitatu. Huyu Zahra hawakuridhiana kwa hiyo ikabidi binti atoroke akutane na Mzungu ambaye alimchukua akampeleka kwenye Ubalozi wa Tanzania.

SPIKA: Sasa swali.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, hapo ndiyo swali langu linakuja. Alikaa katika Ubalozi wa Tanzania kwa kipindi cha miezi sita bila ya kupatiwa *passport* yake ambayo aliizuia mwajiri wake, bila ya kupatiwa vifaa vyake ambavyo alivizuia mwajiri wake hadi alipokuja Mtanzania mwingine kwa wiki moja ndiyo akatengenezewa safari ya kurudi Tanzania. Swali linakuja, je, ni utaratibu gani ambao Serikali imeweka sasa kwa wale ambao wameshafikishwa kwenye Balozi zetu kuweza kuwarudisha Tanzania kwa muda mfupi ili kuipunguzia Serikali gharama za kimaisha kwa kubeba mzigo wa watu wale ambao wako pale katika Balozi zetu? Hilo swali la kwanza.

SPIKA: Aaaah kaka! Kama kila mtu atachukua muda mrefu kiasi hiki kwa kweli kwa muda wa saa moja maswali hayawezi kwisha.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nashukuru, nilikuwa najenga hoja ili Waziri…

SPIKA: Tafadhali jielekeze moja kwa moja kwenye swali.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Ahsante! Nilikuwa najenga hoja ili Mheshimiwa Waziri akijibu ajibu vizuri…

SPIKA: Hapana usijenge hoja, nenda kwenye swali moja kwa moja. Kanuni zinataka uulize swali moja kwa moja.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, hawa ma-*agent* ambao wanaopeleka watu kufanya kazi nje ya nchi linapotokea tatizo

kama hili wao wanawajibika vipi kurudisha gharama kwa Serikali kwa wale watu wao ambao hawakuwatendea vilivyo?

SPIKA: Ahsante sana, majibu umeshaeleweka.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Spika, katika jibu letu la msingi tumesema Serikali imeweka utaratibu rasmi ambao utawasaidia Watanzania wanapofanya kazi nje ya nchi na kupata matatizo waweze kusaidiwa kwa haraka. Kwa hiyo, katika jibu langu la kwanza kwa swali la kwanza la nyongeza ili kupunguza gharama kwa Serikali, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu niendelee kuwaarifu na kuwaomba Watanzania wote wanapokwenda nje ya nchi watumie utaratibu ulio rasmi ambao utawasaidia wao kuwa salama na kupunguza gharama kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, linasema hawa ma-*agent* ambao wanawapeleka nje Watanzania halafu kunatokea matatizo wanaweza kutozwa kiasi gani kulipia gharama za fidia kwa waathirika? Majibu ni yale yale kama hukupitia kwenye utaratibu wa Serikali, Serikali itakuwa ni ngumu sana kufuatilia hizo haki zako. Ukipitia kwenye utaratibu wa Serikali, Serikali kupitia sheria tulizonazo tutasimamia na tutaweza kuchukua hatua kwa hao ma-*agent* ambao wanafanya mambo hayo kinyume cha sheria.

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwa kujibu kwa ufupi kabisa. Tunahamia Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 24

DMO Aliyekuwa Akiongoza Hospitali ya Geita

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU (K.n.y. JOSEPH K. MUSUKUMA) aliuliza:-

Hospitali ya Geita imefanywa kuwa Hospitali ya Mkoa tangu tarehe 8 Januari, 2016:-

Je, ni lini *DMO* aliyekuwa akiongoza Hospitali hiyo atahamia katika hospitali iliyopendekezwa na kikao cha *RCC* kuwa Hospitali ya Wilaya?

NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, licha ya kupandisha hadhi ya Hospitali ya Wilaya ya Geita kuwa Hospitali ya Mkoa lakini bado inaendelea kuwa ya Wilaya hadi tarehe 1 Julai, 2017 itakapokabidhiwa rasmi. Hivyo, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Geita *(DMO)* bado anaendelea kuwa msimamizi wa hospitali hii hadi kipindi hicho itakapohamia rasmi ngazi ya Mkoa na kusimamiwa na Mganga Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, halmashauri inaendelea na taratibu za kupendekeza kituo cha afya ambacho kitapandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya katika kipindi cha mpito wakati taratibu za kujenga Hospitali ya Wilaya zinafanyika. Natoa wito kwa halmashauri kuwasilisha pendekezo hilo mapema katika vikao vya kisheria ili liweze kujadiliwa na hatimaye kuwasilishwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kupata ridhaa.

SPIKA: Mheshimiwa Kanyasu swali la nyongeza!

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, katika Kituo cha Afya cha Nzela ambacho kimekuwa kikihudumia wananchi wa Jimbo la Geita na ni kikubwa na tayari kimekwishafanyiwa maamuzi na Halmashauri ya Wilaya. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda katika kituo hicho na kuona kama kinafaa kufanywa kuwa Hospitali ya Wilaya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, baada ya Hospitali ya Geita ambayo ndiyo ilikuwa Hospitali ya Wilaya kuwa Hospitali ya Mkoa, hivi sasa kuna vifaa vingi ambavyo zimeletwa na Mkoa lakini hakuna Madaktari na watumishi mbalimbali. Je, lini Mheshimiwa Waziri atapeleka watumishi na watalaam katika Hospitali ya Wilaya ya Geita? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nipende kuwapongeza Wabunge wote wa Geita kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kushirikiana na *Geita Gold Mine (GGM)* kwa kuhakikisha kwamba Hospitali yao ya Wilaya ya Geita imekuwa na *structure* ambayo inarahisisha sasa kufanya hospitali hiyo kuweza kutoa huduma bora. Nishukuru sana kwa sababu tulikuwa na Makamu wa Rais pale na Waziri

mwenye dhamana wa sekta ya afya na kushuhudia hospitali ile kukabidhiwa vile vifaa kwa kweli tunawapongeza sana kwa kazi kubwa mliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jinsi gani ya kuambatana nami, naomba nikiri wazi mchakato huu wa Bunge la Bajeti ukiisha nilikuwa na ziara maalum ya Mkoa wa Geita, hili litakuwa ni miongoni mwa eneo moja ambalo tutakwenda kulifanyia kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala zima la kupatiwa wataalam, naomba niwajulishe ndugu zangu si muda mrefu mtasikia sasa Wizara ya Afya inatoa idadi ya waajiriwa katika sekta hiyo na Hospitali yetu ya Geita itakuwa ni kipaumbele kwa sababu ina hadhi ya kutosha ili wananchi wa Mkoa wa Geita wapate fursa kubwa ya kupata matibabu katika Mkoa wao.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Nina swali moja dogo tu. Wilaya nyingi mpya za Tanzania hazina Hospitali za Wilaya ikiwemo Wilaya ya Chemba ninakotoka mimi. Je, Serikali itatuhakikishia ndani ya Bunge hili kwamba katika bajeti inayokuja wametenga fedha kujenga hospitali mpya katika Wilaya zote mpya Tanzania? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu. Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jafo.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, ni kweli na naifahamu Chemba, kaka yangu Mheshimiwa Nkamia tumeshaongea sana kufika Chemba pale kuangalia siyo suala zima la afya, lakini na mambo mengine. Ninavyojua ni kwamba katika bajeti ya mwaka huu ambayo tutakuja kuisoma wiki ijayo ina mikakati mbalimbali katika halmashauri mbalmbali. Halmashauri zingine wamejielekeza katika kuboresha vituo vya afya, wengine wamejielekeza katika Hospitali zetu za Wilaya, lakini wengine wamejielekeza katika Hospitali za Mkoa.

Mheshimiwa Spika, katika hili ninavyojua wazi kwamba michakato yote aidha ya ujenzi wa zahanati, Hospitali ya Wilaya au ya Mkoa, vikao husika kwanza vinaanza na mchakato huo. Imani yangu kwamba na wenzetu katika Jimbo la Chemba jambo hilo watakuwa wameliangalia kwa jicho la upana zaidi. Katika haya maana yake Serikali sasa itafanya juhudi kubwa kupeleka *resources* kutokana na mipango iliyopangwa kutoka katika Halmashauri ili mradi wananchi wetu waweze kupata huduma katika maeneo hayo. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Tunahamia Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Na. 25

Mfumo wa Wazi wa Upimaji na Ujazaji wa Mkataba wa Utendaji Kazi *(OPRAS)*

MHE. JAPHET N. HASUNGA aliuliza:-

Mwaka 2002 Serikali ilipitisha Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 na Marekebisho yake ya mwaka 2008 yaliweka Mfumo wa Wazi wa Upimaji na Ujazaji wa Mkataba wa Utendaji Kazi *(OPRAS)*:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani mfumo huu umetekelezwa nchini?

(b) Ni lini mfumo wa kupima taasisi *(institutional performance)* utaanzishwa na kuanza kutangazwa hadharani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kupima utendaji kazi kwa uwazi ulianzishwa mwezi Julai, 2004 ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kutekeleza Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1998 kama ilivyohuishwa mwaka 2008 pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi wa Umma ilifanya Tathmini ya Uzingatiaji na Utekelezaji wa Mfumo wa *OPRAS* katika taasisi za umma. Tathmini hiyo ilihusisha taasisi za umma 110 katika kipindi cha awamu tatu. Katika tathmini hiyo, lengo lilikuwa ni kufuatilia taasisi zilizokuwa na utekelezaji wa kiwango cha juu. Napenda tu kuliarifu Bunge lako kwamba matokeo ya tathmini hiyo yalionesha kwamba utekelezaji uko katika asilimia 51.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kwamba mfumo huu unatekelezwa na watumishi wote, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora iliagiza waajiri kuhakikisha kwamba mtumishi atapandishwa cheo tu kwa kuzingatia matokeo ya *OPRAS*. Hatua hii imesaidia sana kuongeza kiwango cha utekelezaji kwani sasa kila mtumishi anatekeleza mfumo huu kama sharti la kupandishwa cheo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lini Serikali itaanzisha na kutangaza mfumo wa kupima taasisi (*institutional performance)* hadharani, napenda kuliarifu Bunge

lako Tukufu kwamba Serikali inatarajia kuanza utekelezaji wa Mikataba ya Utendaji kazi katika mwaka wa fedha 2016/2017. Mikataba hii itatekelezwa na taasisi zote za umma ikiwa ni pamoja na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine za umma. Mfumo huu utaiwezesha Serikali kupima utendaji kazi kwa kila taasisi ya umma kwa kila mwaka.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Vwawa swali la nyongeza.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa imeonekana taasisi nyingi hazifuati mfumo huu wakati Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2008 iliweka ni lazima kwa kila mtumishi kujaza hizo fomu na kutekeleza mfumo huu. Je, ni hatua gani ambazo Serikali imekusudia kuchukua kwa taasisi na watumishi ambao hawafuati huu mfumo ambao ni wa lazima kwa mujibu wa sheria?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa kutangaza hadharani taasisi ambazo zimefanya vizuri katika kutekeleza mfumo huu kungesaidia sana kuwapa motisha wafanyakazi wanaofanya kazi katika taasisi hizo. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba umefika wakati sasa taasisi zinazofanya vizuri na zile ambazo zinafanya vibaya zitangazwe moja kwa moja hadharani?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri Angellah Jasmine Kairuki, Utumishi na Utawala Bora.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza, kuhusiana na hatua gani ambazo Serikali inakusudia kuchukua kwa watumishi ambao hawazingatii mfumo huu, nipende tu kumwambia kwamba, kuanzia mwaka 2012, Katibu Mkuu Utumishi alitoa Waraka na ilielekeza kwamba kuanzia kipindi hicho hakuna mtumishi wa umma atakayepandishwa cheo endapo hajaweza kujaza fomu ya *OPRAS*. Vile vile tunakusudia kuweka tozo maalum kama adhabu kwa ajili ya watumishi ambao hawatazingatia sharti hili.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili alitaka kufahamu endapo Serikali iko tayari kutangaza hadharani taasisi zinazofanya vizuri. Nipende tu kusema kwamba, tunafikiria pia kuweka tuzo, lakini tunapokea ushauri na tutaangalia ni kwa namna gani suala hili linaweza kutekelezwa kwa kutangaza hadharani.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria.

Na. 26

Kuanzisha Mahakama ya Wilaya - Kigamboni

MHE. MARIAM N. KISANGI (K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE) aliuliza:-

Hivi karibuni Jimbo la Kigamboni limetangzwa kuwa Wilaya Mpya, hata hivyo wananchi wake bado wanapata huduma ya Mahakama kupitia Wilaya ya Temeke:-

(a) Je, Serikali itaanzisha lini Mahakama ya Wilaya ya Kigamboni?

(b) Je, utekelezaji wa hatua hiyo utaanza lini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la wana Dar es Salaam, Mheshimiwa Waziri wa Afya.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mahakama ya mwaka 1984, Sura ya 11, inaeleza kwamba baada ya kuanzishwa kwa Wilaya Mpya na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali uanzishwaji wa Mahakama ya Wilaya inabidi ufanyike. Hivyo, kutokana na Mheshimiwa Rais kuridhia kuanzishwa kwa Wilaya Mpya ya Kigamboni, Mahakama imeweka lengo la kujenga Mahakama ya Wilaya ya Kigamboni kwa kadri fedha za miradi ya maendeleo zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanzishwa kwa Wilaya, Serikali inaendelea na mpango wa kuboresha majengo na miundombinu ya Mahakama zilizopo Kigamboni. Kwa sasa ujenzi wa jengo jipya la Mahakama kwenye eneo la Mahakama ya Mwanzo Kigamboni unaendelea na unatarajiwa kukamilika mapema Aprili, 2016. Jengo hilo jipya litakuwa na ukubwa wa kutosha na hivyo litakidhi uwepo wa Mahakama ya Mwanzo na ya Wilaya kwa kuanzia.

SPIKA: Mheshimiwa Kisangi swali la nyongeza.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ahsante pia Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri uliyonipa. Kwanza naipongeza Serikali kwa ujenzi wa daraja la Kigamboni ambalo litatusaidia sana wananchi wa Kigamboni kiuchumi, kiutamaduni na kijamii vilevile. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niulize swali langu la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya Jimbo la Kigamboni kuhusiana na Mahakama ya Mwanzo yanafanana na yale ya Jimbo la Temeke na Mbagala. Mahakama ya Mwanzo ya Temeke ina hali mbaya sana, ni ya muda ina miaka zaidi ya 50 hakuna matengenezo yoyote. Pia Mahakama ya Mwanzo ya Mbagala, Magomeni na ile ya Buguruni zina hali mbaya sana. Lini sasa Serikali italeta mpango wa muda mfupi wa kuziboresha Mahakama zote ambazo nimezitaja hapa kwa sasa Mahakama hizi ziko katikati ya mji na hali ya majengo yale yanatia aibu, hayafanani na hadhi ya Jiji la Dar es Salaam? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba wasubiri wiki mbili zinazokuja Wizara ya Katiba na Sheria itawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu bajeti ya mwaka 2016/2017 ambapo itaainisha ujenzi wa Mahakama za Mwanzo zitakazojengwa katika Kata mbalimbali na Mahakama za Wilaya katika Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja, katika upande wa Mahakama za Mwanzo tunao upungufu wa asilimia 52 maana yake kuna Kata ambazo ni sawa na asilimia 52 hazina Mahakama za Mwanzo na kwa upande wa Mahakama za Wilaya ni karibia asilimia 81. Hata hivyo, nyie ni mashahidi, Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni 12.3 kwa Mahakama kwa ajili ya kujenga miundombinu ya Mahakama. Ukiangalia *trend* ya fedha, kwa mara ya kwanza Mahakama imepokea fedha za maendeleo kwa asilimia mia moja kwa mwaka huu wa 2015/2016. Kwa hiyo, tutajenga Mahakama zote kadri ya mpango wa ujenzi wa Mahakama utakavyoainishwa katika bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Ndassa, swali la nyongeza.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, lakini Serikali imekuwa ikiahidi kwamba itajenga Mahakama za Mwanzo kwa muda mrefu sana. Chikawe *one* aliahidi, akaja Chikawe *two*, mama Nagu, Kairuki, ahadi ni ile ile. Sasa

ningependa kujua Mahakama ya Nyamikoma, Kata ya Iseni, Jimbo la Sumve Wilaya ya Kwimba itakuwa lini kwenye mpango wa kujengwa?

SPIKA: Tunaomba jibu la swali hilo, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, ni kweli, nakubaliana na mawazo ya Mheshimiwa Mbunge kwamba tangu Mheshimiwa mama Nagu, Chikawe na Asha-Rose Migiro tumekuwa tukizungumzia suala la ujenzi wa Mahakama za Mwanzo ikiwemo Mahakama ya Mwanzo ya Sumve.

Mheshimiwa Spika, nioneshe tu katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mahakama ilipokea takribani asilimia 51 ya fedha kwa ajili ya maendeleo, mwaka 2013/2014 asilimia 18, mwaka 2014/2015 asilimia 7.5, mwaka 2015/2016 asilimia 100. Kwa hiyo, hoja ninayotaka kuijenga hapa chini ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli tutatekeleza mipango ya maendeleo kama tulivyoainisha katika program ya ujenzi wa Mahakama ikiwemo Mahakama za Mwanzo. Kwa hiyo, hili jambo linawezekana, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Ndassa kwamba tutamaliza kuijenga Mahakama ya Mwanzo ya Sumve kama tulivyoahidi kabla ya mwaka wa bajeti wa 2016/2017 haujakamilika.

SPIKA: Ahsante. Kwa sababu ya muda Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na. 27

Kufungua Kiwanda cha *General Tyre*

MHE. CATHERINE V. MAGIGE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafungua rasmi Kiwanda cha kutengeneza Matairi cha *General Tyre* ambacho kilikuwa ni mkombozi mkubwa kwa uchumi wa Taifa na ajira kwa wananchi wa Arusha?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Kutengeneza Matairi cha *General Tyre* Arusha kilisimamisha shughuli zake mwaka 2009 kutokana na Serikali kukosa fedha kwa ajili ya kukiendesha. Wakati huohuo, aliyekuwa mbia mwenza

(Kampuni ya *Continental AG*) hakuwa tayari kuendelea kuwekeza katika kiwanda hiki.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuona kiwanda hiki kinaanza kuzalisha matairi mapema iwezekanavyo. Hii inadhihirishwa wazi katika Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano 2016/2017-2020/2021 na tumepanga kuanza utekelezaji katika mwaka wa fedha unaoanza Julai 2016. Aidha, Serikali tayari imenunua hisa 26 zilizokuwa zinamilikiwa na mbia mwenza. Kiwanda hicho kwa sasa kinamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Vile vile, Serikali imeamua kuweka dhamana ya kusimamia na kuendesha kiwanda hiki chini ya *NDC* na Tangazo la Serikali *(GN)* juu ya uamuzi huo litatolewa wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Kiwanda cha Matairi, Arusha una maslahi mengi kwa Taifa kuanzia wakulima wa mpira, wafanyakazi kiwandani na maduka ya bidhaa hiyo, usalama wa vyombo vya usafiri vitumiavyo matairi, kodi kwa mamlaka mbalimbali na kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza matairi nje ya nchi. Kwa kuzingatia umuhimu wa mradi huo, Wizara imeiagiza *NDC* kuandaa andiko la kitaalam ambalo pamoja na kujibu masuala ya kiuchumi, kiufundi, kijamii, lazima lizingatie maoni ya wadau wa sekta.

Mheshimiwa Spika, mradi huo ambao ni kielelezi tunataka ujiendeshe kwa kuwa na menejimenti huru yenye watu wenye weledi katika shughuli na bila kutegemea ruzuku ya Serikali.

SPIKA: Mheshimiwa Catherine Magige swali la nyongeza!

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu kuanzia mwaka 2009 mpaka sasa ina maana Serikali ilikuwa inawekeza katika kiwanda cha *General Tyre* bila andiko la kitaalam? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kama kiwanda kitaendeshwa bila kuwa na ruzuku ya Serikali, je, maslahi ya wananchi wa Mkoa wa Arusha yatalindwa vipi? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Charles John Mwijage, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, ni kwamba tumekuwa tukiwekeza bila kuwa na andiko la kitaalam, hapana, lilikuwepo, lakini hii ni biashara, biashara siyo *static*. Kilichobadilika ni kwamba huwezi kuendesha kiwanda kile kwa kutegemea ruzuku. Ule mradi ni *bankable*,

ni rahisi ukaelezea kwamba una kiwanda kile, Tanzania kuna soko la matairi 44,000,000 kwa *span* ya miaka mitatu, soko lenye uwezo wa trilioni 1.18.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunataka andiko, *TIB* ihusishwe, pesa zikopwe kwenye benki za nje zinazotoa riba ndogo, twende kwa mtazamo huo. Ndiyo maana nataka kuitoa kwenye ruzuku, huwezi kuendesha kiwanda kwa ruzuku. Amezungumza Mheshimiwa Bashe jana hapa, ruzuku ya Serikali iende kwenye mambo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, namba mbili, maslahi ya watu wa Arusha. Maslahi ya Watanzania wote yatazingatiwa. Maslahi yanakuja wapi, kiwanda kikishatengenezwa kwa menejimenti ni mali ya Serikali. Tunakolenga maslahi ya Watanzania wote yatapatikana, moja kwa ajira lakini pili kiwanda kile kinaweza kuuza hisa Watanzania mkaki-*own* kama mnavyo-*own TBL*, mnavyo-*own cement*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Swali fupi la nyongeza, nilikuona Mheshimiwa Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Mkoa wa Arusha una kiwanda hicho ambacho kinafahamika zaidi cha *General Tyre* lakini ni ukweli kwamba Mkoa wa Arusha pia una viwanda vingine vingi ambavyo vimebinafsishwa ikiwemo Kiwanda cha Maziwa, Kiwanda cha *Phillips*, Kiwanda kilichokuwa cha Nguo. Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua viwanda vyote vilivyopo katika Mkoa wa Arusha?

SPIKA: Majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paresso. Napenda niseme ukweli, sipo hapa kudanganya watu. Sina kumbukumbu kwamba Kiwanda cha *Phillips* kilikuwa cha Serikali lakini hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni kuona Arusha inapata viwanda.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anawahisha shughuli, nimekuwa Arusha mara tano tangu niwe Waziri, nimeupendelea Mkoa wa Arusha. Napenda kusema kwamba viwanda vitaanzishwa na vitaanzishwa kwa Watanzania kuhamasishwa kushiriki katika viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Maziwa ni kiwanda kidogo na tunao mkakati wa kuanzisha Viwanda vya Maziwa, Viwanda vya Ngozi na Viwanda vya Viatu. Kwa hiyo, wakati utakapofika kila mkoa utapata dozi yake na viwanda vitaanzishwa kiuchumi. Bahati mbaya kuna watu hawataki viwanda, hatutapeleka viwanda pale wasipovitaka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Hapo kazi tu. Tunahamia Wizara ya Maji na Umwagiliaji. *(Makofi)*

Na. 28

Mkoa wa Pwani kuwa na Mamlaka yake ya Maji

MHE. MARY D. MURO aliuliza:-

Je, ni kwa nini Mkoa wa Pwani usiwe na Mamlaka yake ya Maji kuliko ilivyo sasa kuwa chini ya *DAWASCO* ambapo hakuna huduma ya uondoaji maji machafu na bei ya maji iko juu kuliko ile ya Dar es Salaam?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Pwani huduma ya maji safi na usafi wa mazingira inatolewa na Halmashauri za Wilaya na Mamlaka za Miji Midogo isipokuwa kwa Miji ya Kibaha na Bagamoyo ambayo inahudumiwa na *DAWASA* kwa kupitia Shirika la Usambazaji Maji la *DAWASCO*. Muundo huu ni kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Miji ya Kibaha na Bagamoyo imewekwa chini ya *DAWASA* kwa sababu za kijiografia na kiuendeshaji. Vyanzo vikuu vya maji yanayotumika kwa Kibaha, Bagamoyo na Dar es Salaam viko Wilaya za Kibaha (Ruvu Juu) na Bagamoyo (Ruvu Chini). Aidha, wakati mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini inajengwa, Miji ya Kibaha na Bagamoyo haikuwa na watu wengi wanaokidhi kuanzishwa kwa Mamlaka inayojitegemea.

Mheshimiwa Spika, bei ya maji kwa wananchi wa Kibaha na Bagamoyo ni sawa na ile inayotumika Dar es Salaam. Hakuna huduma ya uondoaji majitaka katika miji ya Kibaha na Bagamoyo hivyo wananchi hawalipii huduma hiyo. Kwa sasa *DAWASA* imepangiwa na *EWURA* kutoza bei ya majisafi kwa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo, Mkoa wa Pwani kiasi cha Sh.

1,663 kwa lita 1,000 na bei ya majitaka kwa Jiji la Dar es Salaam ni Sh.386 kwa lita 1,000. Hivyo kwa mteja aliyeunganishiwa mtandao wa majitaka na majisafi Jiji la Dar es Salaam analipa jumla ya Sh.2,049 kwa lita 1,000 za majisafi na majitaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa uondoaji majitaka kwa Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Utaratibu wa kumpata Mhandisi Mshauri atakayesanifu mradi huo umekamilika na usanifu unatarajiwa kuanza Mei, 2016 na kukamilika Oktoba, 2016. Mshauri atatayarisha mpango kazi pamoja na nyaraka za zabuni zitakazotumika kutangaza zabuni ya ujenzi.

SPIKA: Mheshimiwa Mary Muro ameridhika.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri…

SPIKA: Amesimama, *okay*.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa kwenye majibu yake ya msingi amesema kwamba Mkoa wa Pwani ulikuwa na wananchi wachache, lakini kwa kuwa Mkoa wa Pwani sasa hivi una ongezeko kubwa la wananchi. Je, haoni kama ni wakati muafaka kwa Mkoa wa Pwani kuwa na Mamlaka yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pamoja na majibu yote ya Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba kunatakiwa kuwepo na mpango wa kati kabla ya mpango huu ambao anasema kuna upembuzi ili kuondoa maji machafu katika Mkoa wa Pwani? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Isack Kamwelwe, umeulizwa maswali yote mawili, je, huoni kwamba…

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilisema kwamba wakati Mamlaka ya *DAWASA* inaanzishwa, Miji ya Bagamoyo na Kibaha haikuwa na watu wengi. Kwa sasa nakiri kabisa kwamba ni miji ambayo imekomaa ina watu wa kutosha.

Mheshimiwa Mbunge, kupitia Sera ya Maji na Sheria ya Maji Na.12 ya mwaka 2009 unaweza kumwomba Mheshimiwa Waziri mwenye mamlaka akaidhinisha uanzishwaji wa Mamlaka katika Mji wa Kibaha. Ijulikane kwamba au utambue kwamba Mamlaka zinazoanzishwa zinatakiwa kujitegemea. Kwa

hali hiyo, italazimika ziwe na chanzo chake cha maji. Kwa hiyo, unapoleta hilo ombi ni vyema mkatafakari na kujiweka sawa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu suala la huduma ya majitaka kwamba kuwe na mpango wa kati wakati tunaendelea kusanifu uondoaji wa majitaka kwa Miji ya Bagamoyo na Kibaha, mpango wa kati upo. Tunaweza tukajenga mfumo wa mtandao wa majitaka lakini mpango wa kati ni kujenga *septic tanks* kwa kila nyumba ambazo zinasaidia kuondoa majitaka kwa kipindi cha kati.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Wasaniii na Michezo.

Na. 29

Kujengwa kwa Jumba la Sanaa
***(Theater Center)* Kigoma**

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO aliuliza:-

Mkoa wa Kigoma unaongoza kwa kuwa na vijana wengi wanamichezo na wasanii mfano Shaaban Robert, Diamond, Ali Kiba, Banana Zoro, Linex, Mrisho Mpoto na kadhalika:-

(a) Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika Mkoa wa Kigoma kwa kujenga Jumba la Sanaa *(Theater Centre)* ili vijana wa aina hii wawe na sehemu nzuri ya kuendesha shughuli zao?

(b) Kama Serikali inakubaliana na hoja hiyo, kituo hicho kitaanza kujengwa lini?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua mchango mkubwa wa wasanii mashuhuri wenye asili ya Mkoa wa Kigoma kama vile Diamond, Ali Kiba, Banana Zoro, Mrisho Mpoto japokuwa nimepata taarifa kwamba huyu Mrisho Mpoto *origin* yake ni Mkoa wa Ruvuma na wengine ambao wameiletea sifa na kuitambulisha nchi yetu katika fani ya muziki na sanaa.

Mheshimiwa Spika, katika Sera ya Utamaduni ya mwaka 1999, Sura ya 4, kipengele Na.4.1.9 inasema, Serikali itahakikisha kuwa panakuwa na jengo la kisasa la sanaa za maonesho katika ngazi ya Taifa. Aidha, wananchi watahamasishwa kuhakikisha kwamba wanatenga maeneo ya maonesho.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kuhimiza Halmashauri na Manispaa zote nchini kutenga maeneo ya kujenga vivutio vya sanaa. Kuhusu Mkoa wa Kigoma, tunashauri Serikali ya Mkoa kwa kushirikisha Halmashauri zote za Mkoa huo ione umuhimu na namna bora ya kupanga na kutekeleza ujenzi wa Jumba la Sanaa. Aidha, tunatoa wito kwa Halmashauri zote nchini zione umuhimu wa kujenga majengo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi ya kujenga miundombinu katika Halmashauri mbalimbali nchini ni jukumu la Halmashauri husika. Hivyo kila Halmashauri inashauriwa kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya Maendeleo ya Sanaa.

SPIKA: Mheshimiwa Nsanzugwanko, swali la nyongeza.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nipende kumkumbusha kwamba tunasema wasanii na wanamichezo wenye asili ya Kigoma, siyo wakazi wa Kigoma. Mrisho Mpoto mimi nazungumza naye, asili yake ni Kigoma ila amehamia Songea. Hata akina Diamond nao ni watu wa Kigoma lakini wanaishi Dar es Salaam. Nilitaka tuweke rekodi sawasawa maana huwezi kuwa msanii mzuri kama asili yako siyo Kigoma. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Aaaaaah!

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, hii Sera ya mwaka 1999 ambayo inatamka dhahiri kwamba hizi *Theater Centers* zitajengwa Makao Makuu ya nchi, je, Mheshimiwa Waziri huoni kwamba sera hiyo imepitwa na wakati kwamba vijana wengi wako kwenye Majiji, Halmashauri na Manispaa zetu? Ni lini Serikali itaiangalia upya sera hiyo ambayo kusema kweli imepitwa na wakati kabisa hasa Sura ile ya Nne ambayo inasisitiza kwamba hizi *Theater Centers* zitajengwa katika Makao Makuu ya nchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, niendelee kushukuru kwamba Mheshimiwa Waziri amekiri Kigoma imetoa mchango mkubwa na kwa kweli wasanii wale wengi wao wanatoka Kigoma, Kibondo na Uvinza. Napenda kujua ni kwa nini basi Wizara isitoe mwongozo *technical* kwa Wakuu wetu wa Mikoa na Ma-*RAS* wetu ili wajue kwamba sasa wakati umefika hizi *Theater Centers* zijengwe katika Halmashauri na Manispaa zetu zote katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Anastazia Wambura.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Nsanzugwanko kwa jinsi anavyoshirikiana vizuri na wasanii. Vile vile tunathamini mchango mkubwa wa Waheshimiwa Wabunge wote katika kuitetea na kuwa mstari wa mbele kuboresha tasnia ya sanaa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ambalo linasema kwamba sera hii imepitwa na wakati, ni kweli tunakubali kabisa kwamba sera hii kwa namna moja au nyingine imepitwa na wakati. Kwa hiyo, kwa hivi sasa napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imeshaandaa Rasimu ya Utamaduni na imeshaiwasilisha katika ngazi za juu za maamuzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inapongeza sana kazi za wasanii na hasa kwa jinsi wanavyojishughulisha na masuala ya kijamii. Tumekuwa tukiwaona wasanii kama Mrisho Mpoto na wenzake wakijishughulisha na kampeni za kuhamasisha usafi katika Majiji yetu. Kwa sababu hiyo basi tumeona pia kuna umuhimu wa kufanya maandalizi ya Sera ya Sanaa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ambalo linataka Serikali itoe mwongozo kwa mikoa, tunakubaliana nalo kabisa kwamba tutatoa mwongozo huu. Pia napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kupitia Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), Wizara inaendelea kutoa wataalam waliokamilika katika fani za sanaa na utamaduni ikiwemo utaalam wa uandaaji wa Majumba ya Sanaa. Hata hivyo, Wizara hii pia ipo katika mazungumzo na TaSUBa ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza kutoa mafunzo nje ya kituo hiki.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuziomba Halmashauri zote ziajiri Maafisa Utamaduni. Ahsante.

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo ni la Wizara ya Fedha.

Na. 30

Ahadi ya Kupandishwa Pensheni kwa Wastaafu

MHE. CONCHESTER L. RWAMLAZA aliuliza:-

Katika bajeti ya mwaka 2015/2016 Serikali kupitia Waziri wa Fedha iliahidi kupandisha pensheni kwa wastaafu wanaolipwa Sh.50,000 ili walipwe Sh. 100,000/=.

Je, Serikali imetekeleza ahadi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchester L. Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumfahamisha Mheshimiwa Rwamlaza na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali ilitekeleza ahadi yake ya kuongeza kima cha chini cha pensheni kutoka Sh.50,114.43 kwa mwezi hadi kufika Sh.100,125.85 kwa mwezi, kuanzia Julai 2015 ikiwa ni ongezeko la asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Jibu zuri sana, la mfano kabisa hili. Ahsante sana Dkt. Ashatu Kijaji. Mheshimiwa Conchester bado una swali?

MHE. CONCHESTER L. RWAMLAZA: Ninalo Mheshimiwa.

SPIKA: Haya swali la nyongeza.

MHE. CONCHESTER L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Msingi wa swali langu ni malalamiko ya wastaafu wanaopokea pensheni kwamba hawajawahi kuongezewa fedha hizi. Kwa kuwa kuna malalamiko hayo na kwa kuwa Serikali sasa imetoa tangazo hili kupitia swali langu, je, inasema nini kuhusu wale wastaafu ambao hawajalipwa kiwango hicho kipya na wanaelekezwa vipi namna ya kudai fedha zao hizo pamoja na *arrears*? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Fedha, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Rwamlaza. Alichokisema na Serikali inafahamu kipo, lakini naomba niseme yafuatayo:-

Katika ongezeko hili ni Mfuko wa *PSPF* pekee ambao umeweza kulipa sh. 100,000 kwa mwezi mpaka leo. Mifuko mingine iliyobaki kwa mujibu wa vifungu vya 25 na 36 vya Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii Na. 8 ya mwaka 2008 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 5 ya mwaka 2012, kima cha chini cha pensheni kwa mifuko yote inatakiwa kupandishwa na Mamlaka hii ya *SSRA*. Kwa sasa Mamlaka hii inamalizia kufanya *actuarial valuation* kwa Mifuko yote hii na Bodi za Mifuko hii pia zipo katika mchakato baada ya *actuarial valuation* kukamilika ili waweze kuanza kulipa rasmi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kulipa *arrears* zao, wastaafu wote watalipwa *arrears* zao baada ya *actuarial valuation* kukamilika na Bodi za Mifuko hii kukamilisha mchakato huu kuanzia Julai 2015. Kwa hiyo, wasiwe na wasiwasi watalipwa *arrears* zao zote. *(Makofi)*

SPIKA: Swali la mwisho la nyongeza Mheshimiwa Peter Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Pamoja na majibu ma… yasiyoridhisha sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kumekuwa na malalamiko mengi sana ya hawa wastaafu. Mmetutangazia kwamba hapa kazi tu, unaweza ukatuambia ni lini hawa wastaafu watapewa hizo hela kwa sababu sasa ni muda mrefu umepita? Tunataka tupate muda kwa sababu kwa kweli wanakuja kwenye maofisi yetu na wanatusumbua. Naibu Waziri ametangaza kwamba wamelipwa lakini hawajalipwa wakati waliahidiwa? Ni lini sasa Serikali hii ambayo inasema hapa kazi itatoa hizo pesa? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Fedha, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Peter Msigwa kwa swali zuri lakini kwa kukiri japo ameishia njiani kwamba kwa majibu yangu mazuri, nakushukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba bodi hizi zinaendelea na mchakato ili waweze kutangaza baada ya *SSRA* kumalizia *actuarial valuation.* Leo hii mchana nitakuwa na kikao na Mkurugenzi Mkuu wa *SSRA* kuhusu suala hili. Naomba niwaahidi wastaafu hawa kwamba pale tu tutakapomaliza, Serikali imeshaji-*commit* kwamba tutalipa malipo yao yote kuanzia Julai 2015. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maneno mengine magumu *actuarial valuation* hapa sijui kama kila mtu anajua ni kitu gani. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, nawashukuru wote mliopata nafasi na ambao hamkupata nafasi kwa kweli muda wetu ni mdogo, tuendelee kuvumiliana muda tutakaokuwepo hapa ni mrefu tutapata tu nafasi ya kuuliza maswali.

Matangazo niliyonayo ni ya wageni walioko ndani ya ukumbi wa Bunge nao ni wafuatao:-

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika ambao ni wanafunzi 48 wa kidato cha sita na Walimu wa wanne kutoka shule ya Sekondari ya Huruma inayomilikiwa na Masista wa Misericordia Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Mkuu Ndugu Chrispiana Ikaku - Mkuu wa Shule. Karibuni sana. Mnapendeza kwelikweli na inaonekana hata kwenye masomo mmekaa vizuri. Karibuni sana Bungeni watoto wetu. *(Makofi)*

Pia mgeni mwingine wa Mheshimiwa Naibu Spika ni Ndugu Christopher Kalaja, Katibu wa Uchumi na Fedha kutoka Muleba. Karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Silvestry Koka, Mbunge wa Jimbo la Kibaha ni Ndugu Dkt. John Calist kutoka Ufaransa. karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini ambao ni Viongozi wa Kikundi cha Wakulima cha Mwalyego *AMCOS* na Utengule Usongwe, Ndugu Edson Mwalukasa na Emmanuel Mwanjuguja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Matangazo ya kazi, Mheshimiwa William Ngeleja, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo mkutane saa 7.40 mchana, Jengo la Utawala, ghorofa ya pili, ukumbi 229.

Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Masuala la UKIMWI anawaomba Wajumbe wa Kamati yake saa 7.00 mchana mkutane Jengo la Utawala, ukumbi 227. Wajumbe wa Kamati yangu ile ya UKIMWI mnaombwa mkutane kama nilivyosema hapo juu. *(Makofi)*

Liko tangazo linatoka kwa Mheshimiwa Upendo Peneza, sijui kwa nafasi ipi lakini ni tangazo, anasema anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni vijana kuwa kutakuwa na kikao cha pamoja kwa lengo la kupanga masuala mbalimbali ya vijana hapa Bungeni saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni vijana katika Bunge hili mnaombwa kufika bila kukosa. Sasa sijui *definition* ya vijana ni nini maana yake

hata mimi najiona kijana hapa. Siku nyingine mtupatie *definition* ili watu wajielewe wako wapi. *(Kicheko/Makofi)*

Mwisho, Mwalimu Kasuku Bilago, Mbunge wa Buyungu anaomba Wabunge wote ambao ni Walimu kutoka pande zote bila kukosa mfike Msekwa saa 7.00 mchana baada ya kuahirisha shughuli hapa, mtagawana vijana waende upande fulani walimu waende upande fulani, Msekwa ni kubwa sana wote mnatosha. Kwa hiyo, anawaomba Walimu wenzake mkutane pale ili muweke mikakati inayoendana na haki za Walimu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea, Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha Miaka Mitano kuanzia mwaka 2016/2016 – 2020/2021

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Kuna tangazo la mwisho, samahani, Waheshimiwa Wabunge ambao hajaenda kusajili alama zao za vidole kwa ajili ya mfumo wa *biometric* mnatangaziwa kufanya hivyo. Zoezi litafungwa leo na tunategemea kuanza majaribio ya matumizi ya *biometric* kesho Ijumaa tarehe 22 Aprili 2016. Yeyote ambaye hatajiandikisha kesho hataweza kuingia ukumbini.

MWONGOZO WA SPIKA

WABUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Haya miongozo miwili, nafunga daftari, tuanze na Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni 68(7) sambamba na ile ya 46(1).

Mheshimiwa Spika, wakati Naibu Waziri wa Fedha na Mipango anajibu swali la Mheshimiwa Conchester kuhusiana na ongezeko la pensheni kwa wastaafu amelieleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inawalipa hao wastaafu kuanzia Julai, 2015. Baada ya maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Conchester alirudi na jibu ambalo ni kinzani kabisa akatueleza sisi Watanzania kwamba wanaolipwa ni wale waliokuwa kwenye Mfuko wa *PSPF* na akasema hiyo mifuko mingine inasubiria *actuarial valuation,* hii ni *contradiction.* Tulivyopitisha na walitueleza hapa Serikali kwamba wanaenda kuwalipa hawa wastaafu Sh.100,125 kuanzia Julai. Hivi tunavyoongea kuna watu ambao

wanatakiwa kulipwa na *PSPF* mpaka leo hawajalipwa na kikwazo kikubwa kikiwa ni Serikali ina madeni mengi haijapeleka *PSPF*? Naibu Waziri anatujibu majibu ambayo hayakidhi na yenye dhihaka kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kujua kabisa kwamba Mwongozo wako ni upi wakati tukiuliza maswali kwa ajili ya Watanzania Mawaziri wanakuja na majibu mepesi sana. Hata pale wanapoulizwa maswali ya nyongeza wanaweka dhihaka kwamba wameeleza majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha, tunaomba Mwongozo wako.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Esther Matiko. Ninachoweza kusema jambo hili si jambo ambalo linaweza likatolewa ufafanuzi wa kutosha kwenye muundo wa kikanuni wa uulizaji maswali ndani ya Bunge na utaratibu wa majibu ndani ya Bunge. Ninachoweza kusema ni kwamba Serikali itatafuta nafasi nzuri ya kuwapa Waheshimiwa Wabunge ufafanuzi mzuri jinsi *PSPF* walivyolipa na mafao yote kwa ujumla kwenye sekta hii ya hifadhi ya jamii yanavyofanyika na utaratibu uliowekwa. Katika tatizo hili la wastaafu wa *PSPF* waliolipwa na ambao hawajalipwa na nini kitafanyika, wakati tutakapokuwa tunaendelea na bajeti zetu, basi Serikali itapata nafasi pia ya kutoa ufafanuzi wa kina. *(Makofi)*

SPIKA: Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mwongozo wangu ni kwamba tuwe na subira, Mheshimiwa Naibu Waziri amejieleza vizuri sana hapa, huenda tu ni sintofahamu ya kuelewa nini kimezungumzwa. Hata hivyo, itakuja Wizara ya Fedha tutaibana hapa, itakuja Wizara ya Kazi na Ajira tutaibana hapa hata Wizara nyingine ambazo zinaendana na mambo haya tuna nafasi pana sana ya kushughulika na jambo hili Mheshimiwa Esther Matiko na Waheshimiwa wengine ambao mngependa jambo hili lifuatiliwe kwa uhakika, hatutafunika chochote. Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) lakini nikienda sambamba na Kanuni ya 39(7) ambayo inahusu muda wa maswali. Katika Mkutano wa Pili nilikuwa na swali siku mbili kabla ya Mkutano wa Pili kwisha na Kanuni inasema kwamba maswali ya siku ile kama muda haukutosha yataenda siku zinazofuata lakini *within* kile kipindi cha Mkutano ule lakini mpaka Mkutano ule umekwisha swali langu halikuja na siku ya mwisho niliomba Mwongozo Mheshimiwa Naibu Spika alikuwa kwenye Kiti hakunipa nafasi. Hivyo, ni kwamba, Kanuni ilikiukwa na mpaka leo swali langu halijaletwa leo ni siku ya tatu na bado maswali yanaendelea kiasi kwamba swali langu linaweza lisiwe la msingi tena.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kujua ni kwa nini mara nyingi tunaposimama kuomba miongozo ambayo ni ya Kikanuni hatupati nafasi kiasi kwamba Kanuni zinavunjwa? Kwa hiyo, naomba kujua sasa swali langu litaletwa lini kwa sababu lilikuwa la msingi sana na nilikuwa nataka liulizwe kabla ya kipindi cha bajeti. *(Makofi)*

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Susan unasema mnapoomba miongozo hampati nafasi na nimekupa nafasi ya Mwongozo. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge kiko kitini ambacho kina orodha ya maswali yenu yote kwa tarehe mbalimbali na kipindi hiki tutauliza maswali yanayokaribia 500. Kwa hiyo, naomba kabla mtu hajalalamika afike kwanza kwenye Ofisi yetu ya Bunge atazame kama swali lake lipo au halipo? Kama halipo pia muoneni Katibu wa Bunge kwa vyovyote vile kutafanyika utaratibu wa kuona nini kifanyike. Inawezekana labda swali lina matatizo, kutakuwa na kitu fulani. Ofisi yangu haina utaratibu wa kuficha swali la aina yoyote ile. Kwa hiyo, naomba muwasiliane na Ofisi na ukiona Ofisi haikupi ushirikiano wasiliana na Ofisi ya Spika moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Spika, naomba kuleta mbele ya Bunge lako maelezo ya Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 28(3), Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

KWA KUWA, Mkutano wa Tatu wa Bunge ambao ulianza tarehe 19 Aprili, 2016, umepangwa kumalizika tarehe 1/7/2016.

NA KWA KUWA, kutokana na matakwa ya Kanuni ya 105(4) na Makubaliano ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki bajeti ya Serikali itasomwa siku ya Alhamisi tarehe 9 Juni 2016.

NA KWA KUWA, muda uliopo wa kujadili na kupitisha bajeti za Wizara mbalimbali kabla ya kusomwa kwa bajeti ya Serikali ni mfupi takribani siku thelathini kuwezesha kila Wizara kupata muda wa kutosha kuwasilisha bajeti yake na pia kupata michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge.

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) na (4) vikao vya Bunge huanza saa 3.00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana na kurejea saa 11.00 jioni hadi saa 1.45 usiku.

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(15) Bunge haliwezi kukutana siku za Jumamosi, Jumapili au siku za mapumziko.

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(8) na (13) muda wa Waziri anayewasilisha hotuba ya bajeti na anapohitimisha hotuba yake ni dakika zisizozidi sitini.

NA KWA KUWA, Kamati ya uongozi katika kikao chake kilichofanyika siku ya Jumamosi tarehe 16 Aprili, 2016 iliona umuhimu wa kuongeza muda wa kujadili na kupitisha bajeti za Wizara na hivyo iliazimia kuliomba Bunge likubali kutengua Kanuni zinazohusu muda wa vikao vya Bunge na muda wa Waziri kuwasilisha na kuhitimisha hoja.

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Tatu, Kanuni za 28 na 99 zitenguliwe kwa mujibu wa Kanuni ya 28(3) na 153(1) ili kubadili muda wa vikao vya Bunge na uwasilishaji wa hotuba za bajeti za Wizara kama ifuatavyo:-

(i) Kanuni ya 28(2), (4) na (5) ambazo kwa ujumla wake zinaelekeza kwamba muda wa kurejea kwa vikao vya Bunge ni saa 11.00 jioni na muda wa kuahirisha vikao vya Bunge ni saa 1.45 usiku zitenguliwe na badala yake Bunge lirejee saa 10.00 jioni na kuendelea hadi saa 2.00 usiku litakapoahirishwa. *(Makofi)*

(ii) Kanuni ya 28(15) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza pamoja na mambo mengine, kwamba Bunge halitakutana siku za Jumamosi itenguliwe na badala yake Bunge likutane siku za Jumamosi kwa kadri mahitaji yatakavyojitokeza kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 8.00 mchana. Isipokuwa kwamba katika siku hizo hakutakuwa na kipindi cha maswali.

(iii) Kanuni ya 99(8) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba muda wa Waziri anayewasilisha hotuba ya Bajeti ya Wizara ni dakika zisizozidi sitini itenguliwe na badala yake Waziri awasilishe hotuba yake kwa muda usiozidi dakika hamsini.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 99(13) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba muda wa Waziri anayehitimisha hoja ni dakika zisizozidi sitini itenguliwe na badala yake Waziri ahitimishe hoja yake kwa muda usiozidi dakika hamsini.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu mpya uanze kutumika tarehe 22 Aprili, 2016 tutakapoanza shughuli za bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono sana, sasa naomba niwahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja ya Kutengua Kanuni iliridhiwa na Bunge)

SPIKA: Kwa hiyo, kwa kifupi sana tumekubaliana kwamba itakuwa kila siku ya kazi kwa kipindi cha jioni tunaanza saa 10.00 jioni hadi saa 2.00 usiku, itatupatia muda zaidi wa kufanya kazi. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kukubali hilo, kweli Bunge hili ni la Hapa Kazi tu.

Tumekubali kwamba tutafanya kazi siku za Jumamosi kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 8.00 mchana. Naomba Watanzania wafanye kazi na waige jinsi Bunge hili linavyochapa kazi.

Mawaziri watawasilisha hotuba zao kwa dakika arobaini na tano…

WABUNGE FULANI: Hamsini.

SPIKA: Narudia tena, Mawaziri watawasilisha hotuba zao kwa dakika arobaini na tano, tumekubaliana hivyo. Pia tumekubaliana kwamba Mawaziri watahitimisha hotuba zao kwa dakika hamsini. Hayo ndiyo makubaliano yetu.

Katibu alishasoma shughuli inayoendelea kwa hiyo naomba sasa tuendelee na uchangiaji. Mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, dakika kumi tafadhali.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo wametuletea Mpango huu wa Miaka Mitano ambao umezungumzia mambo ya msingi na muhimu kabisa kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la muhimu kabisa ambalo napenda kuisisitiza Serikali ni kwamba iwekeze zaidi katika suala la nishati. Tumeona jinsi ambavyo Serikali katika miaka mitano iliyopita imeweza kuwekeza kwenye nishati na

tumeona jinsi ambavyo kuwepo kwa nishati hii kwa asilimia 30, wananchi wengi wameweza kunufaika kwa kutumia umeme ambao upo mpaka vijijini. Kwa hiyo, napenda kusisitiza sasa kwamba Serikali iongeze uwekezaji katika suala zima la umeme hasa vijijini ili tutakapokuwa na umeme wa uhakika vijijini, itawezesha wananchi wetu kuweza kujiajiri katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaona jinsi ambavyo Awamu ya Tano tumekusudia kujenga viwanda, kwa hiyo kwa kuwa na umeme maeneo yote ya vijijini na mijini tutaweza kuongeza uwekezaji kwa suala zima la viwanda na vijijini wawekezaji wataweza kuwekeza katika viwanda. Kwa hiyo, niombe tu Serikali katika suala zima la umeme iongeze fedha nyingi katika Mpango huu wa miaka mitano ili tuweze kuona wananchi wengi hasa wa vijijini ambao kwa kipindi kirefu walikuwa hawana umeme waweze kunufaika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala la madini, Serikali imesema kwamba itawezesha sekta muhimu za kiuchumi ikiwepo sekta ya kilimo na madini. Napenda kuomba Serikali iwekeze katika suala zima la madini hasa kwa wachimbaji wadogo kwa kuongeza mitaji ili kuwawezesha vijana wengi waweze kujiajiri. Wapo vijana wengi sana ambao wanatumia nguvu zao katika shughuli mbalimbali za kiuchumi hasa katika uchimbaji wa madini, lakini wanakosa vifaa muhimu kwa ajili ya uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeona iangalie sekta hizi za kiuchumi kuweza kuziboresha zaidi, napenda kutoa msisitizo kwamba Serikali iongeze fedha hasa kuwawezesha wachimbaji wadogo kuwapa zana bora za kuweza kufanyia shughuli za kiuchumi ili vijana wengi waweze kujiajiri katika sekta hiyo ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mapendekezo pia katika suala zima la maji. Ni muhimu sana Serikali iangalie uwezekano wa suala la maji hasa vijijini. Kwa miaka iliyopita tumeona jinsi ambavyo wananchi wengi hasa vijijini hawana maji safi na salama. Kwa hiyo, ili wananchi tuweze kufanya shughuli zetu vizuri na yaweze kupatikana maendeleo endelevu, tunapenda pia katika Mpango huu tuongeze fedha nyingi sana katika suala zima la upatikanaji wa maji safi na salama hasa vijijini ili akinamama ambao wamekuwa wakitumia muda mrefu kwenda kutafuta maji umbali mrefu zaidi ya kilomita tano wapate nafuu. Wakiweza kupatiwa maji safi na salama na kuwa karibu zaidi nina uhakika nguvu zao nyingi wataweza kuwekeza katika shughuli za kiuchumi zaidi na wengi wataweza kuongeza pato la Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile katika maeneo ambapo tumezungukwa na maziwa kwa mfano katika Kanda ya Ziwa tumezungukwa na Ziwa Viktoria. Napenda kutoa msisitizo kwamba Serikali iweke mpango mkakati wa kutosha ili

tuweze kuvuta maji kutoka Ziwa Viktoria na maziwa mengine kwa maeneo ambayo yamezungukwa na maziwa. Hii itawezesha wananchi walio wengi kuweza kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona kwamba nchi hii ya Tanzania tumezungukwa na mito, maziwa kama nilivyosema Ziwa Viktoria limetuzunguka lakini wananchi hawana maji safi na salama. Kwa hiyo, niombe sasa katika Mpango huu wa Miaka Mitano, Serikali hebu iwekeze vizuri, iweke mkakati mkubwa wa uhakika wa kuhakikisha kwamba inavuta maji kutoka Ziwa Viktoria na maziwa mengine ili wananchi waweze kufikiwa na maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka iliyopita tumeona jinsi ambavyo Serikali wameweza kuvuta maji kutoka Ziwa Viktoria mpaka Kahama sasa yanaelekea Shinyanga yanaenda mpaka Tabora lakini Mikoa ambayo tumezungukwa na ziwa kama Geita wananchi hawana maji safi na salama. Kwa hiyo, nichukue tu fursa hii kusisitiza kwamba kwa kuwa imeweka kwenye Mpango wake hebu sasa iangalie uwezekano wa kupata fedha za kutosha iwekeze katika suala zima la upatikanaji wa maji ili maji haya yawezeshe shughuli mbalimbali kwa sababu huwezi ukawa na viwanda bila ya kuwa na maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie suala la maji kwa uhakika kwa sababu maji ni changamoto kubwa. Tumeona jinsi ambavyo kila mmoja hapa anasimama anasema naye ana changamoto hiyo ya maji. Kwa hiyo, suala la maji liwe kipaumbele katika mpango mkakati wa miaka mitano hii ili wananchi wetu waweze kunufaika na kuweza kufanya shughuli zao vizuri kwa sababu wana maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua pia suala la maji ni uhai, tukiwa na maji safi na salama hata afya za wananchi zitakwenda vizuri. Ndiyo maana napenda kusisitiza sana Serikali ijikite katika kuhakikisha kwamba maji safi na salama yanapatikana kwa wananchi wa Tanzania wakiwemo wa Mkoa wa Geita ambapo tuna changamoto sana ya maji. Tumezungukwa na ziwa lakini hatuna maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la msingi kabisa katika Mpango huu ambalo limenigusa, nimeona jinsi ambavyo Serikali imejipanga kuwekeza katika suala zima la reli ya kati. Ili tuweze kuwa na uchumi imara, ni vyema Serikali ikawekeza zaidi katika reli. Nami naunga mkono kabisa iweke mpango mzuri kuwekeza katika reli ya kati kwa *standard gauge* ili kuwezesha usafirishaji wa bidhaa muhimu kutoka bandari ya Dar es Salaam kwenda katika mikoa ya pembezoni ambayo iko mbali na bahari ya Dar es Salaam ambako ndiko kwenye bandari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tunajua nchi yetu ya Tanzania imezungukwa na nchi mbalimbali ambazo hazina bahari. Nina uhakika kwamba tukijenga hii reli kwa sababu kupitia hii reli ya kati ambayo inakwenda Mikoa ya Kigoma na mikoa mingine mpaka nchi za jirani Burundi, Rwanda na sehemu mbalimbali uchumi utaimarika. Kwa hiyo, katika miaka mitano hii Serikali ikiwekeza katika mpango mzima wa reli ya kati na kuiwezesha vizuri kabisa nina hakika uchumi wetu wa Tanzania utaweza kuimarika vizuri zaidi na tutaongeza mapato ya Taifa kwa sababu wenzetu wa nchi za jirani wataweza kutumia bandari yetu ya Dar es Salaam na kuweza kuongeza pato letu la Taifa katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo vilevile na sisi ambao tunatokea mikoa ya pembezoni tutaweza kupata bidhaa katika bei nafuu zaidi. Kwa sasa hivi unakuta bei ya simenti Dar es Salaam inauzwa kwa bei ndogo mfuko Sh.15,000/= lakini ukifika Geita mfuko huo huo unauzwa Sh.22,000/= mpaka 25,000/=. Kwa hiyo, tunaona jinsi ambavyo maisha ya wananchi yanakuwa ni ya gharama kubwa sana, lakini Serikali ikiwekeza katika reli nina uhakika hata usafirishaji wa bidhaa muhimu kama simenti na vitu vingine itawezesha bei ya bidhaa kuwa bei ambayo inamwezesha Mtanzania hata wa hali ya kawaida kuweza kufanya shughuli zake za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile katika suala la reli, napendekeza kama kuna uwezekano tuweze kujenga hata bomba la mafuta kwenye njia hiyo hiyo ya reli kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka Mikoa ya Kanda ya Ziwa hiyo ya Tabora kuelekea Kigoma hata katika nchi za jirani. Hii itasaidia kupunguza bei ya mafuta kwani kwa sasa hivi Dar es Salaam lita moja inauzwa Sh.1,400/= lakini ukifika Mikoa ya Geita, Mwanza bei inakuwa imepanda zaidi inakuwa zaidi ya Sh.2,000/=.

Mheshimiwa Spika, haya yote yatawezekana ili kuboresha uchumi wetu pale ambapo tutafikiria kuwa na bomba la mafuta kutokea Dar es Salaam kwenda katika mikoa ya pembezoni, Mikoa ya Kanda ya Ziwa na mikoa mingine ambapo itatuwezesha kuinua uchumi halisi wa wananchi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile katika suala zima la miundombinu, ni vizuri sasa Serikali iangalie katika mkakati wake ambao umekuwa nao na Sera ya Taifa ya kuunganisha kati ya mkoa kwa mkoa, wilaya na wilaya kwa barabara za lami. Napenda kuunga mkono kwamba Serikali iendelee kuwekeza fedha ili tuweze kuunganisha kwa barabara za lami mikoa kwa mikoa, wilaya kwa mikoa na wilaya kwa wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tuangalie hata ile mipango mikakati iliyopita pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliyopita. Kwa mfano, katika Mkoa wangu wa Geita katika Ilani tulikuwa tumekusudia kujenga barabara ya lami kutoka Geita kuelekea Kahama kupitia Bukoli lakini vile vile kujenga barabara ya lami kutoka Geita kwenda Bukombe ambayo ni wilaya mpya katika Mkoa wa Geita. Kwa hiyo, niombe Serikali pia iangalie yale mambo yaliyokuwepo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliyopita ihakikishe inayafanyiwa kazi ili wananchi tuweze kunufaika zaidi. Kwa sababu tukiwa na barabara za lami Mkoa kwa mkoa, wilaya kwa wilaya, wilaya kwa mkoa, nina uhakika wananchi wengi wataweza kunufaika kwa sababu wataweza kusafirisha mazao yao vizuri na watafanya biashara zao vizuri na kwa uhakika na mwisho wa siku pato la Taifa litaweza kuwa la uhakika na litainuka na tutakuwa na uchumi ulio bora katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, kwa kuwa Serikali hii imekusudia kuwekeza katika suala zima la viwanda na mimi kila nikisimama nimekuwa nikizungumzia suala la viwanda na mikoa mingine kama ya Geita ambayo ni mipya haina viwanda. Niiombe Serikali kwa kuwa imeamua kuwekeza katika masuala ya viwanda, tuiangalie mikoa hii kwa kuanzisha viwanda kutokana na rasilimali zinazopatikana kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, naomba ikiwezekana tujengewe hata kiwanda cha simenti. Katika Kanda ya Ziwa hatuna kiwanda cha simenti hata kimoja. Wananchi wanahangaika sana kupata simenti, bei ni ghali sana ndiyo maana watu wanashindwa kujenga nyumba bora kwa sababu bei ya simenti ipo juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano ni ya viwanda, niombe awamu hii tuhakikishe Kanda ya Ziwa tunakuwa na kiwanda cha simenti ili wananchi waweze kunufaika kutokana na rasilimali ambazo tuko nazo katika maeneo yetu. Sambamba na hilo, tuangalie pia kwa kikanda kwamba kanda hii inazalisha mazao fulani tuwekeze viwanda vya aina hiyo kulingana na mazao yanayopatikana katika maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, napenda kutoa msisitizo kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuwekeza zaidi katika masuala ambayo nimeyazungumzia, suala la umeme na viwanda katika maeneo yote ili wananchi wetu waweze kushiriki katika kuhakikisha kwamba uchumi wao unaweza kuinuka kwa sababu bila ya ushiriki wa wananchi wa kawaida haiwezekani uchumi kuinuka zaidi. Niombe tu Serikali itilie mkazo katika kuona kwamba yale ambayo imezungumzia katika Mpango ya Miaka Mitano yafanyiwe utekelezaji maana wakati mwingine tunapanga mipango lakini utekelezaji wake unakuwa ni asilimia ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe yale ambayo tumeyapanga kwa miaka mitano hii tuhakikishe basi tunayafanyia kazi kama ni fedha tutafute fedha ili tuweze kuyatekeleza na kuhakikisha kwamba uchumi wetu unainuka kwa sababu ya uwepo wa mambo ambayo tumeyapanga katika miaka hii mitano na kwamba yametekelezwa hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nikiomba Serikali ihakikishe inayafanyia kazi mambo yote niliyoyazungumza. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

Waheshimiwa Wabunge, nifafanue tu kidogo kwamba uchangiaji wetu ni dakika kumi na tano kwa sababu hatujafika wenye bajeti, kule kwenye bajeti ndiyo tutachangia dakika kumi kumi kadri tulivyotengua Kanuni. Kwa hiyo, mtakaopata nafasi kwa kweli ni wachache lakini basi jitahidini hivyo hivyo kwa hizo dakika 15 maana ingekuwa dakika kumi kumi mngechangia wengi zaidi basi watakaopata nafasi ndiyo hao hao na leo lazima tuhitimishe hoja hii. Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega atafuatiwa na Mheshimiwa Costantine Kanyasu.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa nafasi hii niliyopata ya kuchangia Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao unaenda kuleta matumaini makubwa ya Tanzania yetu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kwa haraka haraka kumshukuru na kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kasi kubwa na nzuri anayokwenda nayo na hasa hii ya kutumbua majipu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunasema kwamba Mheshimiwa Rais aendelee kusonga mbele na sisi tupo pamoja naye maana katika nchi hii kama kuna watu ambao wametuangusha kwa kiasi kikubwa na kwa muda mrefu ni watumishi. Wametuangusha kwa muda mrefu na watu walikuwa wanahisi kwamba labda wao ni watu wasioguswa. Napenda kusema Mheshimiwa Rais anaendelea kuwapa hata Waheshimiwa Mawaziri wetu ujasiri wa kufanya kazi na sisi Wabunge na Watanzania kwa ujumla wake tunawaunga mkono. Lazima twende mbele zaidi ikiwezekana tuiangalie Sheria yetu ya Utumishi maana huko watu ndipo walipokuwa wanajificha wakihisi kwamba hawana namna ya kuweza kuguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya, naomba sasa nielekee katika kuzungumzia Mpango wetu wa Maendeleo wa

Miaka Mitano ambao unakwenda sambamba na uchumi wa viwanda ili kuelekea katika uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, jana nimesikitika sana katika Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani rafiki yangu mwasilishaji kaka yangu Mheshimiwa David Silinde alikuwa anakatisha tamaa suala la viwanda na akafika mahali akazungumzia mpango ule wa Serikali wa kuanzisha *industrial business hub* pale Kurasini kwa kusema kwamba kwa kufanya vile ni kama tunakaribisha Wachina sisi tunajigeuza kwenda kuwa wachuuzi, nadhani hajaelewa vizuri jambo hili.

Mheshimiwa Spika, namwambia Waziri wa Fedha aharakishe sana ile *Kurasini business hub* ipatikane kwa haraka. Wachina kule kwao wanafunga vile viwanda wanakuja kufungua hapa Tanzania. Namkaribisha aanze kuona namna Wachina wanavyokimbilia hapa Tanzania kufungua viwanda pale Mkuranga, tuna viwanda vingi na vinajengwa kila siku ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kiwanda kikubwa *cha tiles* kinajengwa pale Mkuranga katika Kijiji cha Mkiu. Kile kiwanda cha marumaru kitalisha *East Africa* nzima. Tutakapopata *business hub* pale Kurasini maana yake ni kwamba watu watakuwa wanajua *one business stop center* ipo pale Kurasini na watakwenda kupata bidhaa zinazozalishwa pale. Sisi leo pale tuna viwanda vya *cement* wenzangu wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa wanaomba viwanda vya *cement*. Tuna kiwanda cha *cement* cha *RHINO*, tuna kiwanda cha *cement* cha *Diamond* pale, tunatengeneza mpaka yeboyebo pale Mkuranga.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati njema sana bomba la gesi lipo pale na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda Mheshimiwa Mwijage kwa namna ambavyo ananipa *support* kubwa ya kuwaleta wawekezaji waje kuwekeza katika lile bomba la gesi ambalo lina toleo lake katika vijiji vyangu vya pale Mkuranga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niendelee kuunga mkono…

SPIKA: Unajua nilikuwa najiuliza huyu Mheshimiwa Ulega aliyemtoa Adam Malima ni nani huyu, sasa ndio nimejua, Mheshimiwa Ulega endelea bwana. *(Kicheko)*

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema Serikali iendelee na mpango huu wa viwanda na sisi tumejipanga vizuri sana. Katika eneo moja ambalo tumejipanga vizuri pale Mkuranga ni hilo la viwanda, tuna hekari zaidi ya elfu kumi ambazo zipo tayari kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nipongeze sana Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano ule wa kuboresha miundombinu yetu. Katika hili naomba nimwambie rafiki yangu Mheshimiwa Silinde na Kambi Rasmi ya Upinzani namna alivyopotoka tena amemtaja mpaka kipenzi chetu Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika ukurasa wa tisa eneo la barabara, eti Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuwakumbusha Watanzania kwamba aliyekuwa Waziri wa Ujenzi wakati wa utekelezaji wa mpango uliopita ndiye Rais wa sasa, kwa hiyo hakuna matumaini. Nataka nimwambie matumaini ni makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza katika takwimu zake nataka nimwambie amekosea jambo moja kubwa. Waziri wa Fedha alipokuwa anasoma Mpango ule ametuelekeza kwamba mpango wa Serikali ulikuwa ni kujenga kilometa za lami 5,775 lakini mpaka tunafika Desemba 2014 zilikuwa zimeshajengwa zaidi ya kilometa 2,775. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa Waziri wa Fedha hakuweka mwaka wa 2015, kuanzia Desemba, 2014 mpaka 2015 na kufika hapa leo, Wizara ya Ujenzi katika muda huo ambao haukutajwa imejenga zaidi ya kilometa 500 za barabara za lami. Naomba nizitaje, Ndundu - Somanga kilometa 60, Tunduma - Sumbawanga kilometa zaidi ya 200, Lwanjilo - Chunya kilometa zaidi ya 36 na Iringa - Dodoma zaidi ya kilometa 259. Kwa namna ya kipekee kabisa naipongeza Serikali yangu namna tulivyojenga barabara za lami za kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba niitaje barabara ya Ubungo *Bus Terminal*…

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mpaka Mabibo na Kigogo zaidi ya Kilometa 6.4, barabara ya kutoka Uwanja wa Ndege pale Jeti kwenda Vituka mpaka *Devis Corner* kilometa zaidi ya 10, barabara ya kutoka Ubungo Maziwa - *External* zaidi ya kilometa 2.25, barabara ya kutoka Kibamba - Mloganzila zaidi ya kilometa 4. Halafu watu hawa namna wasivyokuwa na shukrani tazama ukipita leo katika Jimbo la Ubungo unatoka Goba mpaka unakwenda kutokea Chuo Kikuu ni lami tupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Fedha katika Mpango huu aoanishe na Waziri wetu wa Ujenzi sasa twende katika kuijenga barabara ya kutoka Mkuranga - Kisiju ambapo eneo hilo linakwenda kuwa la viwanda. Hii ni katika kukamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuja kuwaomba kura Watanzania wale wa Mkuranga

aliwaambia barabara ile itajengwa. Nina hakika kwa mwendo ambao tunakwenda nao barabara ile itajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nielekee katika maji…

TAARIFA

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Spika, nasikitika sana kusema kwamba muda wote huo ….

SPIKA: Mheshimiwa Ulega kuna taarifa ngoja uipokee.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Haya ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Silinde kifupi sana.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Ulega, Mbunge wa Mkuranga ni rafiki yangu sana lakini ni vizuri tu nikampa taarifa kwamba takwimu hizi tumezitoa upande wa Serikali. Tulichokuwa tunakieleza hapa ni yale yaliyofanyika ndani ya miaka mitano. Kwa hiyo, tulikuwa tunaoanisha miaka mitano iliyopita ya mpango jinsi ambavyo haukufikiwa yale malengo na tunakoelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimueleze Mheshimiwa Ulega tulichokuwa tunakionyesha ni kwamba Rais wa sasa alifanikisha kwa kiwango cha asilimia 53 sasa Waziri wa Ujenzi wa sasa atupe mkakati kwanza kumalizia ile asilimia 47 ili twende kwenye ule uchumi wa viwanda tunaoutarajia. Kwa hiyo, rafiki yangu Mheshimiwa Ulega pamoja na kwamba ulimshughulikia Malima, nakupongeza sana kwa hilo ni vizuri ukaendelea kutumia takwimu za Kambi ya Upinzani ili hotuba yako iendelee kuwa nzuri. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Mheshimiwa Ulega, taarifa hiyo unaipokea?

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Spika, sijaipokea kwa sababu rafiki yangu Mheshimiwa Silinde nimemkumbusha kwamba ujenzi wa barabara uliendelea katika mwaka wa 2015, asisahau na madaraja ambalo na yeye atakwenda kupigia picha pale Kigamboni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kwamba wenzetu hawa hata masuala ya maji hawakuyazungumzia. Tazama Serikali yetu ina mpango mzuri sana wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili la maji, napenda niipongeze sana Serikali. Napenda niseme kwamba nina hakika katika miaka mitano hii ile ajenda yetu ya kumshusha mama ndoo kichwani itafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo unaelekeza kwamba katika miaka mitano iliyopita takribani asilimia zaidi ya 60 ya Watanzania walipata maji safi na salama. Katika Jiji la Dar es Salaam, watu wanabeza tazama Jiji la Dar es Salaam lilivyopata bahati kubwa sana tena kwa pesa zetu wenyewe za ndani. Maji ya kutoka Ruvu Chini yamepita Bagamoyo yamekwenda mpaka Chuo Kikuu kule cha Dar es Salaam, bomba lile limelazwa kwa pesa ya Serikali yetu. Kwa kweli napenda sana niipongeze Serikali. Pia kuna mpango wa maji wa Dar es Salaam wa Ruvu Juu ambao sasa hivi unaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Mkuranga upo mradi mkubwa wa maji ambao utahudumia Dar es Salaam kwa maana ya maeneo ya Kigamboni, Mbagala na Kisarawe, mradi ule wa Kimbiji na Mpera. Naiomba Serikali sasa ihakikishe kwamba mradi ule unawanufaisha na watu wa Mkuranga katika vijiji vya Mkuranga, Dundani, Mwanambaya, Mwandege, Kipala Mpakani vyote viweze kupata maji yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali katika Mpango huu wa Miaka Mitano ihakikishe kwamba inatoa maji kutoka katika Mto Rufiji kwani zaidi ya asilimia 50 ya maji ya Mto Rufiji hayana matumizi yoyote. Kilometa hata 200 hazifiki kutoka Mto Rufiji kuja Dar es Salaam. Tuyatoe maji yale tuyalete Dar es Salaam, maji haya ya visima hayana hakika hata Naibu Waziri wa Maji jana alieleza hapa, *Engineer* Kamwelwe yeye mwenyewe amesema kwamba maji haya ya visima hayana hakika.

Mheshimiwa Spika, tutakapotoa maji kutoka Mto Rufiji yatanufaisha Wilaya za Rufiji, Kibiti, Mkuranga na yatanufaisha Dar es Salaam yote ya Kusini bila kuisahau Kisarawe. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweke mpango huu madhubuti wa kuhakikisha tunatatua kabisa kero ya maji katika Wilaya zetu na nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nizungumzie suala la kilimo. Katika Mpango wa Maendeleo imeelezwa kwamba kutoka 2010 kurudi nyuma ilikuwa ni karibu asilimia mbili na *point* lakini kutoka 2010 kuja 2015 zilizidi kidogo asilimia ikaja mpaka asilimia 3.4 bado ukuaji huu ni mdogo. Pamoja na ukuaji huu kuwa mdogo bado nchi yetu imekuwa na chakula cha kutosha na mpaka tukawa na chakula cha ziada.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tuna tatizo kubwa la mabadiliko ya hali ya hewa, naiomba sana Serikali katika mpango wake wa bajeti hii tunayokwenda nao sasa ihakikishe kwamba mambo makubwa mawili, matatu yafanyike.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni kuipa nguvu zaidi Wizara yetu ya Kilimo ili tuweze kujielekeza zaidi katika kilimo cha umwagiliaji. Hata pale kwangu Mkuranga ipo miradi ya umwagiliaji ya Changanyikeni, Yavayava na Kisere. Miradi ile yote haiendi vyema ni kutokana na ukosefu wa fedha. Ninayo matumaini makubwa kwamba katika mwaka huu tunaokwenda nao tutapata pesa ya kutosha na hatimaye miradi ile inaenda kutekelezwa na kukamilika na kuwanufaisha wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ili kuhakikisha kilimo chetu kinaenda vizuri ni pembejeo. Ni lazima tuipe pesa ya kutosha pembejeo ili kilimo chetu kiwe na tija. Kwangu naomba sana pembejeo ya *sulfur*. Pembejeo hii ya *sulfur* nashauri iuzwe kama inavyouzwa cocacola dukani. Sisi wakulima wa korosho tukikuta *sulfur* inauzwa kwa wingi madukani tutaridhika sana. Nataka nikuhakikishie wakulima wote wa korosho baada ya hapo tutakipa chama chetu Chama cha Mapinduzi kura zote za ndiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna matumaini mkubwa sana, tazama mfumo wetu wa stakabadhi ghalani, Waziri Mkuu juzi amekwenda kule Mtwara na Lindi ameboresha mfumo huu. Tunayo matumaini kwa kasi tunayokwenda nayo kero zote zinazotusumbua katika mfumo wa stakabadhi ghalani zitatatuliwa. Mwaka huu korosho imeuzwa zaidi ya Sh.2,500 kwa kilo katika Wilaya yangu ya Mkuranga. Watu wamepata pesa nyingi na mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja ya Mpango huu wa Maendeleo. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Huyo ni Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge wa Mkuranga, tunakushukuru sana. Naona jamaa zangu kushoto hapa walikuwa wanatoa macho hivi, rafiki zangu. Sasa zamu yenu, Mheshimiwa Esther Matiko. *(Kicheko)*

KUHUSU UTARATIBU

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Kuhusu utaratibu.

SPIKA: Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Sabreena.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Napenda kutumia Kanuni ya 59(d) kwa ufinyu wa muda naomba nisiisome.

Mheshimiwa Spika, nimetumia Kanuni hii kutaka ufafanuzi, kumekuwa kuna malalamiko mengi sana kuhusu uchangiaji. Jana jioni sikuwepo nilipata

dharura kuna mpiga kura alifariki Manyoni kwenye treni wamemrudisha tunamzika kesho. Nimetoa udhuru jina langu limepelekwa namba ishirini na tatu, jana nilikuwa namba kumi na tano lakini kuna mwenzangu hapa Mheshimiwa Anna alikuwa namba kumi na sita na aliomba udhuru kwenye Meza hiyo lakini kapelekwa namba hamsini na tano.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Meza ya Makatibu katika Bunge letu hili inashindwa kutenda haki mpaka Wabunge tumekuwa tunalalamika mara kwa mara, kwa nini mnashindwa kuwa *fair?* Wote ni Wabunge na tuna hadhi sawa. Tumeona baadhi ya Wabunge wa upande wa pili jana walikuwa hawapo lakini leo wamepewa nafasi za mwanzoni wanazungumza, kwa nini kwetu sisi inatokea mambo haya? Tunaomba utaratibu kuhusu suala hili na tuache kuchakachuliwa wote ni Wabunge tuna hadhi sawa. *(Makofi)*

SPIKA: Niwahakikishie kabisa hakuna uchakachuaji, lakini mlichotoa ni maoni kwa ajili ya Meza yangu ili iwe inaweka mambo sawasawa, nina hakika Meza yangu itajipanga vizuri zaidi. Meza hii haiegemei kambi yoyote ile au upande wowote ule. Hawa ni watumishi wetu wote na wanajitahidi kutenda haki kadiri inavyowezekana. Tuwe na uvumilivu, twende na orodha yetu jinsi ilivyokuwa. Mheshimiwa Matiko nilikupa nafasi.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Na mimi Mheshimiwa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, umeni-*preempt* lakini nitaenda tu.

SPIKA: Ajiandae Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia kwanza kwa kuangalia ni nini kimetekelezwa kwa Mpango wa Kwanza. Ukiangalia kiuhalisia Mpango wa Kwanza haujatekelezwa kwa asilimia 60 kama ambavyo mmeandika. Ni kwa nini nasema hivi? Mfano mdogo tu kwenye hotuba ya Waziri anatuambia kwamba maji vijijini yameenda kwa zaidi ya asilimia 72 kwamba wananchi wa vijijini zaidi ya milioni ishirini wamepata maji.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nikawa nauliza ni Tanzania ipi imepata maji safi na salama? Mkoa wa Mara, Wilaya ya Tarime, Mji wa Tarime siyo tu vijijini hata mjini hakuna maji. Ile Sera ya mwaka 2002 kwamba maji unapata ndani ya mita 400 ni ndoto. Kwa hiyo, kama takwimu zenyewe ndiyo hizi ni dhahiri

mtakuja mtasema mmetimiza kwa asilimia 60 lakini kiuhalisia hakuna kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo mme-*document* hapa kwamba fedha za maendeleo sasa hivi zitakuwa zinaenda kwa asilimia 40 ya bajeti. Mkumbuke Mpango wa Kwanza tulisema asilimia 35, lakini mtu asimame aniambie kama Serikali hii na naomba sana msiwe mnasema Serikali ya safari hii ya Awamu ya Tano imedhamiria *as if* sasa hivi ni chama kingine, ni Chama hicho hicho cha Mapinduzi ndiyo mlikuwepo miaka yote…

MBUNGE FULANI: Na watu wale wale.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Msitake kutu-*fake* Watanzania mnakuja hapa mnasema ooh, sasa hivi tumedhamiria, nikiangalia *cabinet* iliyopo sasa hivi *over sixty percent* ni ile iliyokuwepo Awamu ya Nne. Mkumbuke kwamba hata Awamu ya Nne tulikuwa tukiongea hapa tukiwashauri, baba yangu Mheshimiwa Wasira alikuwa anakuja hapa anatubeza kwenye Mpango, nilikuwa Waziri Kivuli wa Mpango na bahati nzuri aliyekuwa kwenye Mpango ndiyo Waziri wa Fedha na Mpango sasa hivi. Halafu mkikaa mnasema sasa hivi hii Serikali ina dhamira ya dhati, *come on, are you serious*? Watu wale wale, chama kile kile tumekishauri, *over sixty percent* Mawaziri mliokuja madarakani ndiyo wale wale labda mmebadilishwa tu, ulikuwa Waziri wa Katiba na Sheria sasa hivi ni Waziri wa Afya, ulikuwa sijui wapi sasa hivi umeenda pale. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa leo tukisema kwamba tulidhamiria kuimarisha miundombinu ya barabara ambayo ndiyo inaenda kuchochea uchumi wetu na mtu aka-*document* tukasema Rais, Mheshimiwa Magufuli ndiye aliyekuwa Waziri kipindi hicho na nakumbuka katika vitu ambavyo vilipewa kipaumbele ni ujenzi wa barabara, lakini ndiyo mmejenga kwa asilimia hamsini na tatu.

Mheshimiwa Spika, hivyo ambazo hatukuvipa kipaumbele sana asilimia 20, asilimia sijui ngapi! Asilimia tatu! Halafu tunaishia kuwa na mipango. Kwanza nilikuwa najiuliza, kuanzia jana na-*postpone tu*. Maana yake nasema nachangaia nini? Tunatoa ushauri, tunasema *but nothing is going to be done*. Tunachangia nini?

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, naomba sana, tukisimama tuwe kama Wabunge, acha Mawaziri watakuja watajibu kama Serikali. Nashangaa Mbunge anasimama anatetea kweli! Kaka yangu wa Mkuranga, *documents* za Kambi ya Upinzani, tulicho-*document* kimetokana na alichokiandika Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, sasa ukianza kusema, nikasema anajidai aah, sijui zimeongezeka 500. Ongeza hizo 500, zinakuwa ni 3000. Sasa 3000 kwa miaka mitano, leo unazitekeleza vipi?

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, taarifa!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, naomba nishauri na naomba...

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, taarifa!

SPIKA: Taarifa iko upande gani?

MBUNGE FULANI: CCM.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Kulia kwako.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwa mujibu wa Kanuni ya 68, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu na maneno mengine yanaendelea.

Naomba nimpe utaratibu mzungumzaji, anasema juu ya CCM ile ile. Nataka nimsaidie afahamu, ndiyo maana Chama cha Mapinduzi kila baada ya miaka kumi kina utaratibu wa kupata Mwenyekiti mpya na Uongozi mpya. Ndiyo maana kwa taarifa Watanzania wameendelea kukiamini Chama cha Mapinduzi kwasababu ni Chama kinachozaliwa upya kila baada ya miaka kumi.

Kwa hiyo, afahamu anapozungumza na Serikali ya Awamu ya Tano ni Chama cha Mapinduzi kilichozaliwa upya na kazi yake na *speed* yake ni ya Hapa Kazi Tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Huyo ni Mheshimiwa Mabula, kiboko ya Ezekiah Wenje. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Matiko, unapokea taarifa? *(Matiko)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, kwa heshima zote kabisa mdogo wangu katika hili Bunge, hajitambui. Ikumbukwe CCM ikichukua

takwimu za Urais wanapataje, imeanzia 81% imeshuka mpaka Mheshimiwa Magufuli amepata 58%, tena *questionable! Questionable! (Kicheko/Makofi)*

Kingine, huyo huyo wakati Uenyekiti unabadilishwa badilishwa, wakati Mheshimiwa Mnyika anasema kwamba ule uongozi wa Mheshimiwa wa Kikwete ni dhaifu, ninyi mlisimama na kusema na kufedhehesha kila kitu! Leo yaani mnajikosoa ndani yenu wenyewe. Tunafurahi sana na wananchi wanawaona na wanasikia kwamba hamfai! Niendelee! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kwenye nishati ambacho ni kichochezi kwenye viwanda. Mpango uliopita, yaani mlikuwa mmedhamiria mnaleta *Megawatt* 2,780, lakini mpaka tunavyoongea miaka mitano ni *Megawatt* 496 tu. Hivi viwanda tunavyoongea tunaenda kuvipataje, kama nishati yenyewe bado ni goigoi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo kule kwetu Tarime ni wakulima na wafugaji. Tunahitaji hata viwanda, tuwe na umeme. Kwa mwendo huu, tutafikaje? Halafu tukiishauri Serikali hapa kwamba tuwe na vitu ambayo tukiviongea vina tija, watu wanaweka… nyie Wabunge, mmekuja kama Wabunge, wajibikeni kama Wabunge, acha Mawaziri watende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani kiuhalisia nikipitia sekta zote, kwenye elimu ndiyo kabisa! Siku ile Mheshimiwa Rais alisema hapa kwamba viwanda ambavyo anadhamiria na ambavyo vitaajiri Watanzania, vitatumia nguvu kazi zaidi kuliko teknolojia ya kisasa. Kwenye Mpango, matarajio yetu kwenye *VETA* tu hayajafikiwa kwa kiwango kikubwa sana. Sasa leo tuseme tuna Mpango mkakati upi ili uweze kutuaminisha kwamba hii dhamira ya dhati tuliyonayo tutafikia? Mimi mwenyewe natamani sana Tanzania tuweze kukua kiuchumi, wananchi wengi hawana ajira. Tuna rasilimali nyingi, lakini zilikuwa zinakumbatiwa tu na wachache huko, zinatumika vibaya.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kweli hiyo awamu ya tano ina dhamira ya dhati na kwa sababu bajeti hii tunaenda kuongea mambo mengi Wizara mbalimbali, tutaenda kuipima kama ina dhamira ya dhati. Kweli kama ina dhamira ya dhati ya kuwasadia Watanzania, Mheshimiwa Waziri tunaomba hayo uliyoyaandika utuainishie kwamba tunamaanisha. Asilimia 40 zinaenda kwenye maendeleo, tumejizatiti vipi kwenye kodi?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 wakati nachangia bajeti hapa nilimweleza mfano tu, Mama Sada. Nenda hapa kwenye *supermarket* moja Dodoma, umenunua vitu, hakupi ile risiti ya *TRA,* akaenda, akafuatilia akapata.

Mheshimiwa Spika, hawa Usalama wa Taifa, leo ukinunua vitu hawakupi risiti za *TRA*. Juzi tu nimenunua kitu Kariakoo Sh. 620,000/= nikawaambia wanipe

risiti ya *TRA,* ooh, risiti ya *TRA* tukikupa inaenda zaidi ya hapo. Sasa si hii ndiyo bei umeweka kwenye duka lako? Ndiyo! Unajua aliniambia basi naomba nikupe sh. 100,000/= halafu sh. 520,000/= nikuandikie ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Usalama wa Taifa, ninyi kama Wizara mnadhibiti vipi hilo? Tunapoteza mapato mengi sana. Hii mnayosema sijui risiti za *electronic,* hazifanyi kazi, wanaziweka kando. Mtanzania akienda, anamwambia nitakupa hiki, fanya punguza, *shell*, yaani kote tunapoteza mapato *and then* mnakuja tu mme-*document* ma-*paper;* tupe *sign* mnakusanya vipi kodi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haitoshi tu Mheshimiwa Rais kusimama kwenye *TV*, Tanzania lipa kodi. Mmeweka *mechanism* gani kuendeleza hii ya Mheshimiwa Rais anayosema kila siku kwenye *TV* kwamba kodi itakusanywa kweli? Wekeni watu waende kwenye maduka! Ajidai kama ananunua kifaa, aone kama atapewa hiyo risiti au atapewa lugha gani? Kamata, fanya vyote nchi nzima, watu walipe kodi, siyo kuwanyanyasa watu wadogo wadogo, wajasiriamali wenye vimbogamboga, wenye miradi midogo midogo ndio wanaoleta fedha kwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisema mwaka 2015 kwamba, *worthiness* ya mtu i-*reflect* ulipaji wa kodi yake. Sijui hata wamefanya nini? Mnatangaza watu wawe na *TIN,* sijui kila mtu awe na *TIN:* Je, kweli kila Mtanzania ana-*TIN?* Mimi kwa mfano, Esther Matiko, *worthiness* yangu ina-*reflect* nalipa kodi vipi? *Do you trace that?* Kama hamtaweza kukusanya mapato ya ndani na wafadhili wenyewe ndiyo hivyo, hii mipango, miaka mitano tunakuja hapa, patupu! Tena leo bora tunaambiwa zimepikwapikwa ziko asilimia 60. Tukija mwaka 2019 hapa tunaelekea 2020 tutaambiwa *story* zile zile.

Mheshimiwa Spika, nimalizie. Tuwe na nishati, tuboreshe miundombinu ya barabara kama mnataka hivi viwanda kuanzia kule kwa mkulima, barabara zipitike. Tuboreshe reli.

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye *Air Tanzania,* aibu! *National Carrier,* aibu! Ukisafiri, ukaenda na hizi ndege, ukifika Nairobi, wanashuka watalii wote mnakuja Tanzania wachache. Wakishafika pale, ina maana zile hoteli za Kenya ndio wanafaidika. Wanaletwa na magari kuja kwenye mbuga zetu za Tanzania. Hata juzi niliona wanasema, hata daraja la Kigamboni ambalo mmelizindua jana, watasema liko Kenya. Mlima Kilimanjaro Kenya, mengine yote Kenya. *We are not branding our Nation. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Samatta ni mchezaji sijui wa wapi huko, *what are we doing?* Tuwe *serious!* Tutafute vyanzo ambavyo vinatuletea mapato. Sekta ya Utalii, *let's have our National Career.* Hatuna *National Career!* Ni wafanyakazi tu

wamebaki na jengo pale *city center* tena ambalo lipo kwenye *prime area,* mliendeleze basi! Tunabaki tu na vijistori, tutaleta, tutaleta. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa Jimbo langu la Tarime. Kwanza kabisa, naomba kabisa kipekee nimshukuru Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Najua kama wanavyojinafasi humu ndani, mkijivua kweli, ile ambayo tumekuwa tukiwashauri miaka yote, mnasema kelele za chura hazimnini sijui nini; sasa kweli mkiamua kufanya hivyo, siyo kama maigizo kwa sababu mnaona Mheshimiwa Magufuli anavyofanya, mtafika mbali.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu pale huwa anavaa zile *scarf* za Kitanzania na nini, kweli yule ni mzalendo sana. Amekuja Tarime, ameongea mambo mengi sana na Wanatarime.

Kama kweli hiyo dhamira itaenda kutendeka kama ni ya Serikali hii, rasilimali tulizonazo zikageuzwa kuwasaidia Watanzania, maana yake tumekuwa tukiongea, pale kuna Soko la Kimataifa, tumekuwa tukipiga kelele humu mimi na Mheshimiwa Nyambari, limechukua miaka mingi kumalizika, liko Lemagu; lile soko lingemalizika, ingekuwa ni kipato kikubwa sana kwa nchi yetu. Liko *border* pale! Mnachukua muda mwingi sana kumaliza lile soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu Kenya wanachukua hiyo *opportunity,* ukienda upande wa pili wa Kenya ni tofauti kabisa na Tanzania. Lile soko likikamilika, ule mnada ukafunguliwa, kipato ndani ya Mji wa Tarime, kipato ndani ya Wilaya ya Tarime kitaongezeka na Taifa linaenda kupata fedha ambazo leo zitatumika kusaidia hayo madawati na kujenga Maboma. Maana yake mmesema elimu bure, kule kwetu hakuna vipato. Havipo Tarime Mjini! Sasa mnahangaisha watu kujikusanya maskini wale wajenge viboma; watoto wanasoma 200 kwenye darasa moja. tupeni lile soko lifunguliwe, mnada ufunguliwe, kipato kiongezeke.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kipekee kabisa namshukuru ndugu yangu, kaka yangu pale, naomba na Mawaziri wengine, mmepewa ridhaa na Watanzania, mnatumikia nchi. Maana kuna mwingine nilisikia ooh, pale sijui *CHADEMA,* sijui *CUF* hatupeleki maendeleo. *What?*

Mheshimiwa Spika, hizi rasilimali ni za kwetu wote. Wale Watanzania wote wametuweka wote madarakani. Ninyi mmepewa ridhaa ya nchi, kuna wengine wamepewa ridhaa za Majimbo na Halmashauri. Tunatakiwa tuwatumikie wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nafikiri ushauri wangu mkiuzingatia, vichochezi vya kuanzisha viwanda, viwepo; nishati, miundombinu ya barabara na kilimo mkiboreshe, Sekta ya Elimu ili tuweze kupata hao watu ambao

tunasema tunaenda kuwatumia, reli na usafiri wa anga. Ndoto ya Waziri wa Fedha na hii Mipango mnayotuletea, itatimia. Kinyume cha hapo, tutakuwa tunacheza vidogoli tu siku zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko. Mheshimiwa Constantine Kanyasu!

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nami naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwanza kwa kunipa afya na kunijalia kufika siku ya leo niweze kuchangia kwenye huu Mpango.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwanza kwa kasi kubwa ambayo ameanza nayo. Kasi hii inawatisha watu wote. Ukiona maadui zako wanaendelea kukusifia, basi lazima ujue kuna tatizo. Kwa hiyo, wale ambao wanaona hawafanyi kazi, nadhani wanaogopa kivuli chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais kwa kurudisha nidhamu ya Watumishi wa Serikali. Nchi yetu ilikuwa inarudishwa nyuma na mambo mengi sana, likiwemo suala la Watumishi wa Serikali kutokuwa na nidhamu; nidhamu ya muda, lakini hata nidhamu ya utendaji. Hili kama litasimamiwa vizuri, tunaanza kujenga *spirit* ambayo mtu akiingia ofisini, anafahamu kwamba yuko pale kwa ajili ya kufanya kazi ya wananchi. Hili ni lazima lisimamiwe vizuri pamoja na viongozi wengine walioko ngazi ya chini.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kurudisha nidhamu ya matumizi. Naamini tulikuwa ni nchi ambayo tunaweza angalau kujitegemea kwa kiwango fulani lakini matumizi yetu yalikuwa yanakiuka baadhi ya mambo na kuonekana ni nchi maskini sana. Nampongeza pia kwa zoezi lake la kuhakikisha kwamba Watanzania wanalipa kodi.

Mheshimiwa Spika, suala la kodi ni suala ambalo Tanzania ilikuwa inaonekana anayelipa kodi ni mshamba. Watu wengi walikuwa wanajisifu kwa kutokulipa kodi. Sasa hivi utasikia malalamiko ya watu wengi kwamba wamebanwa. Watumishi wa Serikali tulikuwa tunalipa kodi kubwa zaidi kuliko wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, ombi langu tu hapa ni kwamba, zipo lugha ambazo zinatuchonganisha; zinamchonganisha Mheshimiwa Rais. Wapo Watumishi wa Serikali wanakwenda kulazimisha watu walipe kodi kuliko ambayo inatakiwa kulipwa anasema na ni kwa sababu ya Serikali yenu. Naamini watu hawa wakifuatiliwa, kodi ni kwa manufaa ya umma.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Fedha kwa kuja na Mpango wake huu. Naamini kwamba hivi vipaumbele ambavyo vimewekwa kwenye Mpango huu kama vitasimamiwa, tunaweza tukaifikisha Tanzania sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, tunalo ongezeko la mapato ya *TRA*, mapato yetu ya kodi. Nawapongeza sana! Wasiwasi wangu ni mmoja tu hapa, yapo malalamiko sana kwa wafanyabiashara; hakuna *uniformity* pale bandarini. Leo atakuja mtu ana *container, declaration* inaonesha vifaa vilevile ataambiwa Shilingi milioni 20, lakini mtu yuleyule akirudi *next time* ataambiwa Shilingi milioni 50, lakini jana yake utaambiwa mtu mwingine amelipa Shilingi milioni tisa.

Mheshimiwa Spika, nadhani iko haja ya kuweka utaratibu, badala ya kuacha hii *freelance* ambayo mhusika anaweza aka-*gamble* nayo na kuhamasisha rushwa, uwekwe utaratibu ili kila mtu kabla ya kufanya *importation,* ajue kwamba mzigo huu nikiufikisha Tanzania anakwenda kulipa kodi ya shilingi ngapi.

Mheshimiwa Spika, bila kufanya hivyo, tutaendelea kuruhusu watu kukaa mezani na kujadili na matokeo yake yatakuwa kama aliyosema Mheshimiwa Keissy jana kwamba gari ile ile unanunua Dola 10,000, ukija pale, mtu wa *TRA* analazimisha iwe Dola 50,000, anakadiria kodi anayoitaka. Matokeo yake, watu wanakimbia gari pale bandarini, halafu Serikali inauza gari zile kwa bei rahisi zaidi kuliko ambayo alikuwa ameisema mhusika. Mimi nasema Serikali inafanya kazi nzuri, tunaipongeza, lakini ni lazima itoe macho zaidi katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Mpango ambao Mheshimiwa Waziri ameuleta. Kwanza nianze na suala hili la elimu. Nimekuwa napata tabu kidogo kuona Tanzania ina *output* ya wasomi wengi sana, lakini kila kona wasomi wanalalamika ajira. Tatizo ni kwamba hata anayemaliza Chuo Kikuu akimaliza hawezi kujitegemea, akimaliza hawezi kujiajiri, hata yule aliyesomea ufundi, ukimwingiza ukampa kiwanda leo, akifika mle ndani hawezi kufanya kazi aliyosomea. Nasema kwamba, katika kipindi hiki cha miaka mitano, ni lazima mfumo wetu wa *output* katika vyuo vyetu usimamiwe vizuri ili watu wanaotoka waweze kuwa ni *material* ambayo inakwenda kupata kazi kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, niende mbali, tuna *output* kubwa sana ya darasa la saba na *output* kubwa sana ya *form four* na *form six* ambao hawapati bahati ya kwenda kwenda kwenye Vyuo. Nataka kushauri, katika nchi zote ambazo zimefanikiwa kupambana na tatizo la ajira hasa kwa vijana, wameimarisha sana kwenye *Polytechnic Colleges* ambazo ndiyo zinaweza zikasaidia kupunguza tatizo la ajira. Kama tunaweza tukaweka katika Mpango wetu huu wa miaka mitano, tuweke mpango kuhakikisha kila mtoto aliyemaliza kidato

cha nne, anakwenda Chuo cha Ufundi na iwe ni lazima. Hawa watu wataweza kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tumepeleka umeme katika kila kijiji, lakini mafundi wa umeme wanatoka Makao Makuu ya Wilaya. Hii sasa ilikuwa ni wajibu wa Serikali kuona kwamba tunaweka vyuo vya kutosha. Tunavyo Vyuo vya *VETA,* bado vyuo hivi ni gharama kubwa sana kwa wananchi wa kawaida. Chuo ambacho ulidhani angeenda mtu kusoma akapata ufundi, bado vyuo hivi vinachukua watu kwa kuchagua, wanakwenda watu 100 kati ya watu 10,000. Matokeo yake, bado kundi kubwa la vijana limezagaa mitaani, halina ujuzi wowote na Serikali nina uhakika hata tukizungumza kuwapa ajira, hawa sio sehemu ya kundi tunalofikiria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kushauri, pamoja na kuzagaa kwa vyuo, pamoja na mpango mzuri wa Serikali, tuweke mpango kabambe wa kuwa na vyuo vya ufundi ambavyo vitamlazimisha kila mtoto anayemaliza kidato cha nne, aende Chuo cha Ufundi ili apate kazi mbadala.

Mheshimiwa Spika, huwa nawaambia rafiki zangu tunaokwenda China; kule China ziko simu watu wanatumia hapa, zinatengenezwa mitaani tu, kwenye nyumba ya mtu. Ziko nguo zinashonwa mitaani, viko vitu vinatengenezwa hata ukitafuta kiwanda, huwezi kukipata kwa sababu kuna msambao wa viwanda vidogo vidogo katika kila kona na ndiyo namna tunavyoweza kupambana na tatizo la ajira kwa vijana, lakini na tatizo la viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwenye Mpango kuna suala la viwanda. Tatizo langu ni kubwa. Hivi tunazungumzia viwanda vya namna gani? Viwanda hivi vitapata *raw material* wapi? Sehemu kubwa ya viwanda tunavyozungumza ni viwanda vya kilimo. Wilayani kwangu tuna Kiwanda cha Pamba cha *Ginnery,* kipo pale Kasamwa. Kile kiwanda hakijafanya kazi karibu miaka 15 sasa. Ukitazama uzalishaji wa zao la pamba umeshuka kwa kiwango ambacho kinatisha. Tatizo, kwa nini uzalishaji unashuka? *Productivity* ya uzalishaji inapungua wakati gharama za kilimo zinaongezeka! Viwanda tunavyozungumzia vinakwenda kupata *raw material* wapi?

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri kwenye suala la kilimo, kwanza tu-*invest* kiasi cha kutosha kuhakikisha kwamba uzalishaji unaongezeka maradufu ili watu watakaoanzisha viwanda wapate *raw material.* Leo watu wanalima pamba wanapelekewa mbegu feki, halafu mwisho wa siku kwenye uzalishaji mdogo waliopata, wanakwenda kudaiwa na kulazimisha walipe. Matokeo yake ni watu wote wameacha kulima pamba, wanahamia kwenye mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri katika Mpango huu tuwekeze kiasi cha kutosha kuhakikisha kwamba uzalishaji kwenye mashamba, uzalishaji wa mazao katika viwanda ambavyo tunafikiria tunakwenda kuvipeleka, lazima tufikirie namna ya kuongeza mazao yawe makubwa zaidi. Uzalishaji uwe mkubwa zaidi; na njia hapa ni rahisi tu!

Mheshimiwa Spika, cha kwanza ni kuwa na wataalam wetu katika kila kijiji na kuhakikisha wanafanya kazi; lakini kuhakikisha pembejeo zinapatikana kwa wakati. Tulikuwa na tatizo la pembejeo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anajua. Pembejeo zinafika kwa wakulima mwezi wa kwanza. Wakulima wamekwishalima, wameshapalilia ndiyo pembejeo zinafika. Hawa watu wanalipwa!

Mheshimiwa Spika, tumeiambia Serikali kwamba kuna watu wanadanganya kwenye pembejeo, Serikali inatumia pesa nyingi sana, lakini haziwafikii wakulima; zinachelewa kufika. Ndiyo maana mtu analima heka tano za pamba anapata kilo 300. Ni kwa sababu pembejeo zinachelewa kufika. Kwa hiyo, nasema suala la viwanda liangaliwe vizuri kwenye suala la kilimo. Vile vile twende pia kwenye namna ambavyo tunaweza tukawaimarisha wananchi wa kawaida

Mheshimiwa Spika, sina tatizo sana na masharti ambayo yanayowekwa na watu wa Mazingira na kadhalika, lakini nadhani tume-*copy* sana mambo kutoka Ulaya kiasi kwamba tunashindwa kufikiria katika mtazamo wa Kitanzania, ni viwanda gani vinaweza vikasaidia wananchi wetu? Unaona kila siku tunapambana na watu wanaotaka kujikwamua.

Mheshimiwa Spika, kule Ulaya ukienda, mtu mwenye ng'ombe wanne anaweza kuanzisha Kiwanda cha Siagi nyumbani kwake na akapeleka mazao yake kwenye *Supermarket*. Sisi kila siku tukienda kwenye mtu aliyeanzisha kiwanda, tunamfungia, huyu tunamfungia. Badala ya kuwasaidia hawa watu waimarike na wakue, tunawapunguzia uwezo. Utaona Serikali inapambana na watu wapunguze ng'ombe, lakini haiwambii hao ng'ombe wanaowapunguza itawasidiaje wabadilike kuwa na maisha tofauti.

Mheshimiwa Spika, mfugaji wa ng'ombe anafanana sana na mtu mwenye mabasi kumi. Siku zote mtu mwenye mabasi kumi anataka afikishe mabasi 20. Hivi tuliwahi kumfuata mtu mwenye mabasi 20 tukamwambia apunguze idadi ya mabasi? Kwa nini tunafikiria kumwambia mwenye ng'ombe apunguze, lakini hatumwambii apeleke wapi hizo fedha zake?

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwenye hili suala la viwanda, tutafute namna ya kuwasaidia wananchi wa kawaida kuimarisha viwanda vidogo vidogo. Haijulikani *SIDO* ilifia wapi? Haijulikani kama ipo, inafanya kazi gani?

Nilitarajia tuone Tanzania ina Viwanda vya Sabuni kila Mtaa, Viwanda vya Nguo kila Mtaa na Viwanda vya kila kitu kila Mtaa. Sasa haya mambo hayafanyiki kwa sababu ya masharti mengi yanayowabana Watanzania na kuwafanya waendelee kutegemea bidhaa za kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze suala linguine. Kwenye Mpango naona kuna mpango wa kuongeza nishati. Nilisema wakati nachangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, nikasema naipongeza sana Serikali na mkakati wake wa kuimarisha njia ya umeme inayokwenda Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa na wasiwasi sana ya kuwa na njia moja kuu ya umeme ya kupelekea robo tatu ya nchi. Napenda kushauri, katika Mpango huu, ile njia iliyotajwa katika Mpango; ya Nyakanazi, ni njia ya muhimu sana. Nchi nyingi zinapata majanga! Linaweza kutokea janga katikati hapa, nusu ya nchi ikawa giza na nchi hii inakwenda kuwa nchi ya viwanda. Ina maana tutasimama uchumi wetu siku hiyo hiyo. Ni lazima tutafute namna ya kuimarisha njia ya pili ya umeme.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wangu wa Geita, bado umeme unazimika na kuwaka muda wowote kwa sababu njia iliyopo ni ile iliyokuwa inapelekea umeme Sengerema. Umeme ni mdogo sana. Wananchi pale kukatika kwa umeme kwao ni suala la kawaida, lakini umeme mzuri upo jirani tu Katoro pale.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza na Waziri mara kadhaa na nimeomba sana katika mwaka huu wa fedha, umeme wa uhakika upelekwe Geita. Ni Mkoa mpya, Mkoa ambao tunatarajia utakuwa na viwanda vingi. Sisi katika Kanda ya Ziwa ni wakulima wakubwa sana wa nanasi, ingawa nanasi zile Mheshimiwa Mbunge mwenzangu alisema zinafaa kutengeneza madawa ya kienyeji, lakini tunapozungumzia viwanda, basi lazima wakulima waambiwe ni mananasi yapi yanayofaa kwa ajili ya kuuza kwenye viwanda, kwa sababu ardhi inakubali kulima nanasi, kahawa na mazao mengine. Ni lazima tukubaliane kwamba tunahitaji umeme ili huu umeme uweze kuwasaidia wananchi wa Geita.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango huu, naomba sana, sisi Kanda ya Ziwa kama walivyosema wenzangu, tunalo tatizo la bidhaa zote zinazotoka Dar es Salaam kufika Kanda ya Ziwa zikiwa zimepanda bei. Ukifika Geita leo, utakuta bandali moja ya bati inauzwa Sh. 280,000/= wakati bandali hiyo hiyo Dar es Salaam inauzwa Sh.160,000/=. Ni kwa sababu ya matumizi ya barabara. Tunaomba sana reli, reli ikiimarika, itasaidia kupungua gharama za vifaa vya viwandani ambavyo vinapanda bei kila siku Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata gharama ya mafuta iliyoko Geita ni kubwa kuliko iliyoko hapa, ni kwa sababu tatizo kubwa ni Usafirishaji. Hatuwezi kuendelea kujenga barabara zinazobomoka kila baada ya miaka miwili kwa sababu inabeba mizigo mikubwa. Tuwe wakweli! Kama barabara hizi zinatumia mamilioni ya shilingi, tunakopa, wenzetu wanakaa wanasema hawaoni faida ya mikopo na barabara hizo zinakufa, keshokutwa tutalazimika kuzijenga upya kabla ya kulipa madeni. Njia pekee ya kufanya suala hili ni kuimarisha sana mfumo wetu wa reli ili tuweze kuhakikisha kwamba tunakuwa na bidhaa zinazopungua bei.

Mheshimiwa Spika, nimeona kwenye Mpango, kuna mpango wa kujenga Uwanja wa Ndege Chato. Kutoka Geita kwenda Chato ni kilometa zaidi ya 150. Geita ni Makao Makuu ya Mkoa. Naomba sana Wizara hii itakapofika, tunataka kujua kama kutakuwa na mpango wowote kwa Geita kupata uwanja wake wa ndege. Watu hawawezi kutembea kilometa 160; tunakubali kwamba Mheshimiwa Rais anatoka Chato na sisi tunafurahi kuwa na Mheshimiwa Rais Chato, lakini Geita kama Makao Makuu ya Mkoa, tunataka uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Spika, Geita tunayo machimbo mengi sana ya dhahabu. Kwa bahati mbaya Serikali imekuwa inapambana zaidi na maskini kuliko inavyopambana na umaskini.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Kanyasu, kama unaunga Mkono hoja, dakika zako zimekwisha.

MHE. COSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

MBUNGE FULANI: Aaah! Halafu unaunga mkono! *(Kicheko)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Costantine Kanyasu. Sasa tuhamie upande wa *CUF*. Mheshimiwa Salma Mwassa. Karibu sana Mheshimiwa!

MHE. SALMA M. MWASSA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie Mpango wa Pili wa Maendeleo.

SPIKA: Jitahidi sauti kidogo, weka vizuri hiyo *microphone*.

MHE. SALMA M. MWASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nami nichangie Mpango wa Maendeleo. Kwanza kabisa naomba nichangie kuhusu masuala ya maji. Mpango umejikita zaidi kusema

kwamba utajenga miundombinu mipya kuhusu masuala ya maji, lakini haukueleza kipaumbele katika mikoa mingi ya Tanzania.

Kwa mfano, katika Jiji la Dar es Salaam, ni kweli Serikali imejitahidi kuanzisha mradi mkubwa wa maji kutoka Ruvu Chini Bagamoyo kwenda Dar es Salaam na kutoka Mtambo wa Ruvu Juu kuja maeneo ya Kibamba, Mbezi na mpaka katikati ya Jiji, lakini haikuangalia upungufu uliopo.

Mheshimiwa Spika, upungufu uliopo kwa Jiji la Dar es Salaam, tunahitaji lita milioni 450, lakini kwa sasa wakazi hao wa Jiji la Dar es Salaam wanapata lita milioni 180 na kama maji haya ya Ruvu Chini yatafunguliwa kwa mkakati wa huu Mpango mpya, wanatarajia kupata lita 270. Sasa najiuliza, Mpango unasema kwamba watahakikisha kabisa kwamba matatizo ya maji hayatakuwepo tena hasa katika Jiji la Dar es Salaam: Je, hizi lita milioni 130 hata kama huo mradi mpya utatekelezwa, zitakuwa *covered* wapi? *(Makofi)*

Vile vile, nije katika masuala ya miundombinu. Miundombinu ya maji katika Jiji la Dar es Salaam ni michakavu sana, lakini ukiangalia mradi ule mkubwa haukuangalia kwenye kusambaza miundombinu mipya, unasema tu kukarabati ile ya zamani. Ukiangalia, maji yanapotea kwa wingi mno kutokana na miundombinu chakavu.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi unakuta barabara nyingi hizo ambazo Mheshimiwa pale alisema kwamba zimejengwa kwenye Jiji la Dar es Salaam, lakini unazikuta mara kwa mara zipo kwenye madimbwi ya maji, mafuriko. Siyo tu kwa sababu ya mvua, bali ni haya mabomba ya *DAWASCO* ambayo mara nyingi huwa yanapasuka. Kwa hiyo, miundombinu ile ni chakavu, ni mibovu! Hivyo, hata kama yale maji yatafunguliwa, hizi lita milioni 270 hazitaweza kufika kule kutokana na miundombinu ile chakavu mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali kwamba, kabla ya kuyasukuma yale maji kwenye ule mradi mpya, ianze kwanza kutengeneza mikakati ya miundombinu mipya, iondoe kabisa ile miundombinu ambayo ni chakavu na siyo kukarabati, iondoe kabisa. Kule ambapo ni maeneo ya pembezoni kama Bunju, Mabwepande iendeleze kusambaza ile miundombinu ya maji mipya ili wananchi wote wa Jiji la Dar es Salaam wapate maji kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi kweli tunaongelea miaka 54 ya Uhuru, Jiji kama la Dar es Salaam, ndiyo Tanzania, lakini watu bado ni shida kabisa, yaani wakisikia maji yanatoka, wanalala kwenye mabomba. Sasa je, mtu kama wa Katavi huko sijui wapi, itakuwaje? Yaani bado sijaelewa kabisa! Maana yake ukiongelea Tanzania, ndiyo unaongelea Dar es Salaam; sasa kama Dar es Salaam hakuna maji ya kutosha, mpaka sasa hivi bado watu ni shida, wanaishi kwa kuchimba

visima, wanaishi kwa kuhangaika huku na kule, sasa maeneo kama hayo ya pembezoni yatakuwaje? *(Makofi)*

Kwa hiyo nashauri, Serikali ije na mpango mkakati mpya wa kuangalia je, maji yatapatikana vipi? Vilevile isitegemee tu Ruvu, kuna mito mingi inayozunguka Jiji la Dar es Salaam. Kuna Wami! Kwa nini tutegemee tu chanzo kimoja tu cha Mto Ruvu? Kuna mto Rufiji ambao unaweza ukaleta maji mengi zaidi kuliko sasa.

Mheshimiwa Spika, vilevile nijikite pia kwenye elimu. Serikali katika Mpango imeongea zaidi kuhusu kuongeza vijana wetu kwa ajili ya viwanda na Elimu ya Juu, lakini utaongeleaje Elimu ya Juu bila kuongelea Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari? Huko juu atafikaje? Ukiangalia miundombinu ni mibovu kabisa!

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mpango haujasema kabisa kuhusu Shule za Awali. Shule za Awali tunaona tu ni hizi tu za binafsi ndiyo zinazofanya vizuri, lakini hakuna mikakati ya kusema kwamba Shule za Awali itakuwaje, hakuna mikakati ya kusema kwamba miundombinu kama ya madarasa, vyoo kwenye shule zetu za msingi itakuwaje, hakuna mikakati ya kusema kwamba Sekondari itakuwa vipi? Kwa mfano, Sekondari za Kata, ukiangalia ndiyo zinazozalisha mabinti ambao wanapata mimba, kwa sababu hazina mabweni, hazina nini. Sasa unasema tu elimu itaboreshwa, lakini sioni miundombinu yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika Jiji la Dar es Salaam lina upungufu mkubwa, kwa mfano, sasa hivi kutokana na elimu bure, darasa moja watu wameandikishwa labda wanafunzi 1,000. Sasa kama hakuna mkakati wowote, hii ni mwaka huu tu; wanafunzi I,000, wengine 900; kuna shule moja huko Mbagala unakuta wameandikisha karibu 2,000. Sasa unajiuliza, je, mwakani itakuwaje? Nikiangalia huu Mpango hakuna kabisa mikakati ya kuongeza miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nisemee kuhusu *gender* kwenye hii hii elimu. Huko nyuma shule nyingi zilikuwa ni Kilakala, Msalato kwa ajili ya wasichana tu. Naomba tu tuangalie jinsia ya kike kwenye mambo ya elimu. Zijengwe tena zile kwenye mikakati tena, ziongezwe kama hiyo Msalato, Kilakala ziwepo na nyingine na nyingi ambazo ni za kikanda zinazohudumia wasichana tu. Siyo wanafunzi wa kike kuwapeleka kwenye Shule za Kata.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mtu anafaulu, wazazi wanakaa labda *let's say* Magomeni, mtu anasoma sijui Kimara huko Bonyokwa, kwa mfano katika Jiji la Dar es Salaam, sasa huyo mwanafunzi sijui apande pikipiki amalize, apande gari, mtoto wa kike itakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali ijikite tena kuangalia miundombinu hasa kwa mtoto wa kike kwamba tuwe na zile *Special School* kwa ajili ya wasichana tu kama ilivyokuwa awali hizo Shule za *Special School* unakuta ziko nyingi.

Mheshimiwa Spika, vile vile nijikite kwenye viwanda. Serikali inasema kwamba inaongeza uchumi wa viwanda, ndiyo kipaumbele cha Mpango, lakini bado napata tabu. Hapa inaongelea viwanda vikubwa zaidi, lakini kuna vile viwanda vya mikono *(handcraft),* haijaongelea kabisa kwamba itavifanyaje na ndivyo vinavyoajiri watu. Hivi ukiongelea viwanda vikubwa *(modern technology)* lakini hujaongelea viwanda kama *SIDO,* hivi vya mikono, unarukiaje kwenye vikubwa?

Mheshimiwa Spika, tukiangalia huko nyuma, viwanda hivyo vilikuwepo vingi, ni nini kimeua? Yaani utaendaje kusema kwamba viwanda vitakuwa vikubwa! Nakumbuka miaka ya nyuma *SIDO* ilikuwa ndiyo *solution* ya hawa vijana wetu kupata ajira na akina mama. Kwa hiyo, nilitegemea kwamba Serikali ingekuja na mpango kwanza wa vile viwanda vidogo vidogo kama *SIDO* viwekwe kila Mkoa kama ilivyokuwa huko nyuma, yaani wanawake walikuwa wanajifunza angalau kutengeneza batiki, wataweka vile vifungashio na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Mpango ungeangalia viwanda kama hivyo vidogo vidogo kwanza kabla ya kwenda kwenye Viwanda vikubwa. Unapoongelea viwanda vya nguo, mbona hujamwangalia mama anayetengeneza batiki utafanyaje? Kwa nini uiangalie *Sunguratex*, sijui *Mwatex* lakini hujamwangalia mama kama huyu anayetengeneza batiki? Kuna nguo za pamba za kienyeji, zipo tu. Katika viwanda vile, yaani wale watu wangepewa kipaumbele kwanza. Kabla ya kwenda katika hivyo viwanda vikubwa, tuangalie kwanza hivi vidogo.

Mheshimiwa Spika, vile vile niangalie tena kwenye mambo ya afya. Nashukuru kwamba Mpango umejikita zaidi kwenye hospitali kubwa, imeliona hilo, kwamba hospitali kubwa ndiyo zina mlundikano wa wagonjwa sana. Imeongelea Taasisi ya Mifupa *(MOI)*, imeongelea Muhimbili, ikaongelea hospitali za Kanda, lakini haikuongelea kabisa Hospitali hizi za Kata na Wilaya.

Sasa kwa mfano, unaiimarisha Muhimbili, lakini umeacha Hospitali hizi za Kata kwa mfano, labda Kata ya Mbezi, Mbagala na nyingine za pembezoni. Halmashauri zimejitahidi, zimejenga vizuri, labda kila Kata ina Hospitali yake lakini zile Hospitali hazina vifaa, kama ni *labour* unakuta ni chumba kitupu peke yake. Hivi mtu atajifunguaje kwenye chumba hamna kitanda, hamna nini? Kile kitanda unakinunua kwa Hospitali ya Muhimbili tu, lakini huangalii kabisa Hospitali kama hizo za Kata ambazo zingepunguza msongamano wa wagonjwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ijenge hospitali kila Kata. Labda kwenye mambo kama haya ya vifaa tiba, vile vile isijaze tu Muhimbili au *MOI,* tusiziangalie hizi kubwa, kwa sababu ndiyo tunaleta mlundikano wa wagonjwa. Unakuta kila mtu hawezi kwenda kujifungulia hospitali labda ya Manzese, sijui hospitali ya wapi huko yaani ile ya Kata, haiwezekani, kwa sababu kwanza haina wataalam, haina hivyo vifaa tiba, majengo yenyewe hovyo hovyo tu. Kwa hiyo, mtu anaona kabisa kwas ababu Muhimbili ndiyo kwenye vitanda vizuri, ndiyo kila kitu, kuliko nikalale hizi hospitali za kawaida, bora niende kwenye hizo hospitali kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia Serikali ingejikita kwenye hospitali hizi kwa ajili ya kuangalia mambo ya wanawake na watoto. Kwa mfano, nikiangalia Mpango ule uliopita, ulifeli kabisa ku-*control* vifo vya akinamama. Vifo vya akinamama na watoto vilikuwa vinaendelea kuongezeka.

Kwa hiyo, napendekeza kwamba Serikali ingejenga hospitali za Kanda *special* kwa ajili ya mama tu na mtoto na kuongeza Madaktari Bingwa kwa ajili ya mama na mtoto peke yao. Yaani hizo ziwe *special*! Ziwe kwenye kila kanda ambazo zitatibia watoto na akinamama na kuweka Madaktari bingwa, kuliko kwenda kuwachanganya akinamama kama labda kwenye hizo hospitali kubwa. Yaani haieleweki, huku kuna wagonjwa hawa; huku kuna wagonjwa hawa! Kwa kweli mama na mtoto anahitaji *special care* ili tuweze kupata Taifa endelevu na ili kupata Taifa endelevu na sahihi, ni lazima hizo hospitali za rufaa za akinamama na watoto ziwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nijikite kuangalia kilimo. Mpango huu umeeleza kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo na ndiyo kipaumbele. Toka Uhuru nasikia hivyo hivyo, toka nikiwa nasoma; uti wa mgongo wa Taifa ni kilimo, lakini cha kushangaza sasa kilimo hicho hakiwekewi mikakati. Hakuna wataalam, hakuna pembejeo! Kwa mfano, leo ukiangalia mtu ni mkulima kila siku ni kulalamika tu, hivi Vyama vya Ushirika ndiyo vilivyokuwa vinatetea haki za hawa wakulima; Vyama vyenyewe havieleweki lakini mpango haujaja kutueleza kwamba hivi Vyama vitakuwa vipi? Hawa wakulima wapate hizi mbegu wapi? Hawakuongea! Bado Serikali haijaona kuwa hili ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kuna *research* mbalimbali zilikuwa zinafanyika, kwa mfano, *research* kwa ajili ya kahawa, chai, lakini zote hizo sasa hivi hazieleweki kama zinaendaje. Haziko! Mkulima huyu anasaidiwa vipi? Yaani ukiangalia kwa mfano, pembejeo, ziko juu mno! Wataalam wa Kilimo, vitu kama mashamba darasa yangekuwepo kila Kata. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Salma.

MHE. SALMA M. MWASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Nakushukuru sana kwa ushauri wako. Anayefuata ni Mheshimiwa Hussein Nassor Amar na Mheshimiwa Omar Kigua ajiandae. Tuko upande wa CCM sasa, Mheshimiwa Hussein Amar! Mheshimiwa Amar, hayupo eh! Mheshimiwa Omar Kigua.

MHE. OMAR M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote kabla sijaanza kuchangia juu ya Mpango huu wa Serikali, napenda kwanza nikushukuru wewe na niwashukuru Wanakilindi walionipa fursa hii ya kuweza kuwa Mbunge wao wa Jimbo la Kilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepitia Mpango huu, una mambo mengi mazuri, nami naamini kabisa nia ya Serikali hii ni kuleta maendeleo ya dhati kwa wananchi wa nchi hii ya Tanzania. Mpango huu umeangalia mambo muhimu sana ambayo kwa muda mrefu yalikuwa hayaendi sawasawa, sasa basi ni mambo gani ambayo nayadhamiria kwa leo kuyazungumzia? Nitaanza moja kwa moja kwenye Sekta ya Mawasiliano tunapozungumzia barabara.

Mheshimiwa Spika, suala la miundombinu ni suala muhimu sana, nikiamini kwamba miundombinu ikiwa ni mizuri, basi maendeleo ya maeneo mbalimbali na ya nchi kwa ujumla yataweza kufanikiwa. Katika eneo la barabara, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuliwekea uzito unaostahili kwa sababu maeneo mengi yalikuwa hayapitiki hususan barabara katika kiwango cha lami. Hili limeweza kufanikiwa, nami naomba niipongeze Serikali katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, katika eneo langu ambalo nimetoka katika Jimbo la Kilindi, kuna mpango wa kuijenga barabara ile kwa kiwango cha lami ambapo barabara ile itaanzia Handeni kwenda Kibirashi hadi Kiteto kupitia Namrijo Juu pamoja na Jimbo la Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, nataka nilizungumzie suala hili kwa sababu kama nilivyozungumza awali kwamba mawasiliano ni kitu muhimu sana, katika eneo langu ninalotoka kuna mazao yanalimwa hususan mahindi na utakuta hata nchi jirani mazao mengi yanakuja kuchukuliwa Jimbo la Kilindi, lakini kwa sababu miundombinu siyo mizuri, unakuta mazao mengi yanaishia kuozea katika mashamba.

Mheshimiwa Spika, namshauri kaka yangu, Mheshimiwa Profesa Mbarawa pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri waliangalie hili, japokuwa najua kwa mwaka huu wa fedha unaoanza Julai hautakuwepo Mpango huu, lakini

barabara hii ipewe kipaumbele cha hali ya juu kwa sababu italeta maendeleo ya dhati kwa wananchi wa Kilindi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo ningependa kuchangia ni Sekta ya Madini. Nimeona imezungumziwa hapa; na tunapozungumzia madini, tunazungumzia Sekta ya Nishati. Ni kweli kwamba umeme ndiyo kila kitu na Mheshimiwa Waziri hususan Waziri wa Nishati na Madini, ameweza kuweka mipango mizuri sana juu ya nishati, lakini nishati hii haijafika maeneo mengi hususan katika vijiji.

Mheshimiwa Spika, nitolee mfano tu katika Jimbo langu la Kilindi. Tunavyo vijiji kama 102, lakini vijiji vichache sana ambavyo vimenufaika na huduma hii ya umeme kwa maana ya *REA,* ushauri wangu ni kwamba, yale maeneo ambayo kwa asilimia kubwa wameshapata huduma hii, basi waangalie maeneo mengine ambayo hayajanufaika na huduma hii, kwa sababu wananchi hususan wa vijijini wanahitaji umeme kwa ajili ya maendeleo, wanahitaji umeme kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Ni imani yangu kwamba Serikali italiangalia hili kwa umuhimu wa juu sana.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la maji. Maji imekuwa ni kilio, kila Mbunge anayesimama hapa anazungumzia suala la maji. Labda tu nizungumzie kwa eneo ninalotoka mimi. Ni kwamba eneo lile lina maji mengi sana lakini hatuna visima na miundombinu kwa kweli ni ya muda mrefu kiasi kwamba maji imekuwa ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji ni kwamba, maji yanapotea sana. Kuna Mpango kule wa bwawa katika Kata ya Kibirashi; utaratibu ule wa kuhifadhi maji kwa njia ya mabwawa ni utaratibu mzuri sana. Badala ya kuchimba visima tuwe na njia ya kuweza kuhifadhi maji kwa njia ya mabwawa. Nadhani utaratibu huu ni mzuri sana. Ni utaratibu ambao unaweza ukaisaidia Serikali kupunguza kero ya maji kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakuta sasa hivi mvua zinanyesha kule lakini maji mengi yanapotea kwa sababu hatuna utaratibu mzuri wa kuhifadhi maji. Nadhani muda umefika sasa, tuone namna ya kuwashirikisha wananchi pamoja na Serikali juu ya kuweka visima au kuweka mabwawa ambayo yanaweza kuhifadhi maji kwa muda mrefu. Kwa sababu ukiangalia katika eneo langu, siyo rahisi kusema labda maji yatoke Ruvu yafike Kilindi; lakini njia mbadala ambayo inaweza kusaidia kutatua tatizo hili la maji ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na mabwawa.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali yangu kwamba imeweza kuliona hili, tuna bwawa la mfano kabisa ambalo halijakamilika, liko Kata ya Kibirashi. Bwawa hili litawanufaisha wafugaji pamoja na wakulima, naishukuru sana Serikali yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kugusia ni suala la viwanda. Nimeona Serikali yetu ina mpango mzuri sana wa viwanda hususan kufufua viwanda vya zamani pamoja na viwanda vipya. Naomba niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kinachonishangaza hapa, ukiangalia upande wa Tanga ambapo tulikuwa na viwanda vingi sana; tulikuwa na viwanda vya matunda, lakini viwanda vile vimekufa. Nashauri kwamba muda umefika wa kuvifufua viwanda vile pamoja na kuanzisha viwanda vingine.

Mheshimiwa Spika, eneo ninalotoka kuna wafugaji wengi sana, lakini nikiangalia Mpango huu, sioni namna ambavyo wananchi hususan wafugaji wa Wilaya ya Kilindi wanaweza kunufaika na Mpango huu wa viwanda vidogo vidogo. Sasa najiuliza, mifugo hii ambayo Wanakilindi wanayo, watanufaika na nini katika hili? Namshauri kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Viwanda pale aangalie namna ambavyo tunaweza na sisi wananchi wa Kilindi tukaweza kupata kiwanda kidogo cha kuweza hata kutumia maziwa haya mengi ya mifugo ya Wilaya ya Kilindi ili wananchi waweze kunufaika na fursa hii ambayo wanapata wananchi wa sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la utalii kwa ujumla. Ni kwamba eneo la utalii ni eneo muhimu sana ambalo naamini Serikali yetu lazima itie msisitizo wa hali ya juu sana. Wengi wamezungumza hapa kwamba watalii wanafika Kenya, halafu wana-*cross* wanakuja Tanzania. Hili limeelezwa kwamba mpango mzuri wa Serikali ni kununua ndege kusaidia kufanya watalii waweze kufika nchini kwetu kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, napongeza mpango huu, ni mzuri na wale ambao wana-*discourage* suala hili, naona hawako pamoja na sisi. Naomba Serikali yangu iendelee mbele na utaratibu huu. Pia kuna maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri wa Utalii naona hawajafika maeneo mengi, labda nitoe mfano mmoja, katika eneo ninalotoka, kuna Mbuga ya Wanyama ya Saunyi. Mbuga ya Saunyi ina wanyama wa aina mbalimbali, lakini nina wasiwasi kama Serikali inajua kama kule kuna mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Spika, fursa ile inawezekana hata wanyama ambao wanachukuliwa kwenda nje ya nchi, wanachukuliwa kutoka kule kwa sababu sijawahi kusikia hata siku moja watu wanaizungumzia Mbuga ya Saunyi.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba ili tuweze kuimarisha utalii, ni kwamba Serikali iwe na utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba kila fursa ya utalii iliyopo, inatumika vizuri. Haya ni mambo ya msingi ambayo wenzetu wa nchi jirani wameweza kuzitumia na kwa hakika uchumi wao umeweza kwenda juu sana kwa kutumia utalii vizuri. Nina imani kwamba tunavyo vivutio vingi sana lakini Serikali haijatumia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua fursa hii kuzungumzia changamoto ambazo tunazipata katika madini. Ni kwamba nchi yetu ina madini mengi sana, maeneo mengi yana madini na Wilaya ninayotoka mimi, Jimbo langu la Kilindi lina maeneo mengi sana yenye madini, lakini wachimbaji wadogo hawajaweza kunufaika na Mpango huu. Hawajanufaika pengine kwa sababu ya sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja tu kwamba hawa wachimbaji wadogo wadogo ndiyo watu wa kwanza ambao huwa wanagundua wapi pana madini. Mchimbaji huyu mdogo akishapatiwa *license*, inapokuwa muda wake umepita, hapewi fursa mchimbaji huyu kwa sababu hana uwezo. Unakuta *license* hizi wanaopewa watu wengine wenye uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili limeleta malalamiko makubwa sana na namwomba kaka yangu Waziri wa Nishati na Madini aliangalie tena na atakapoleta Muswada wake hapa tuangalie upya sheria hizi zinazohusu wachimbaji wadogo wadogo kwa sababu naamini Serikali ina nia nzuri ya kuwawezesha wananchi wadogo ili waweze kusimama vizuri kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, haya mambo ni ya msingi sana kwa sababu sisi kama Wawakilishi wao tunapata malalamiko mengi sana hususan katika maeneo ambayo yana wachimbaji wadogo wadogo. Ni imani yangu kwamba itakapofika muda wa kuchangia Bajeti ya Nishati na Madini, hili tutalichangia kwa nafasi nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni elimu. Elimu ni kila kitu. Elimu imezungumzwa hapa na nashukuru kwamba Serikali imeliangalia kwa kulipa kipaumbele. Kama alivyozungumza Mheshimiwa mwingine aliyepita hapa, amezungumzia juu ya kuvipa kipaumbele hivi Vyuo vya *VETA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya *VETA* vimeweza kuinufaisha nchi hii kwa muda mrefu sana hususan wanafunzi ambao hawajapata fursa kwenda Sekondari. Nashauri kila Wilaya, kila Mkoa, ikiwezekana tuwe na *VETA* ili iweze kuwasaidia vijana wetu, kwa sababu tumezungumzia kwamba tunataka tuwe na viwanda. Viwanda hivi watendaji au wafanyakazi hawatakuwa ni ma-*graduate* peke yake, ni lazima tutahitaji kada za katikati ambazo zitazalishwa kutokana na *VETA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu nilikuwa nafuatilia kabla sijawa Mbunge, ni kwamba kulikuwa na ahadi ya kujenga Chuo cha *VETA* katika Jimbo la Kilindi Kata ya Kibirashi. Bahati mbaya ahadi hiyo imekuwa ni hewa, lakini naamini kabisa Serikali yangu ni sikivu, watanisikiliza na wataweza kutimiza wajibu wao katika hili, kwa sababu wananchi wanahitaji *VETA* kwas ababu watoto wengi hawapati fursa ya kupata mafunzo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia hili kwa uchungu mkubwa sana kwa sababu maeneo tunayotoka sisi, wananchi vipato vyao ni vya chini sana na sio wote ambao wana uwezo wa kupeleka watoto wao sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nikwambie tu, Wilaya yangu ya Kilindi kwa mwaka huu imekuwa ni Wilaya inayoongoza kimkoa katika matokeo ya Kidato cha Nne mwaka 2015. Naomba kwa niaba ya Halmashauri ya Kilindi, nimshukuru pia Waziri wa Elimu kwamba amefanya jitihada kubwa sana kuhakikisha kwamba pamoja na changamoto nyingi tulizonazo tumeweza kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Omar Kigua, Mbunge wa Kilindi. Sasa ni Mheshimiwa Augustino Masele atafuatiwa na Mheshimiwa Furaha Upendo Peneza. Mheshimiwa Masele!

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hii hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango inayohusu Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, mipango ndiyo msingi wa maendeleo. Kusipokuwa na mipango kutakuwa na ubabaishaji. Kwa maana hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuja na Mpango mzuri wa Maendeleo wa miaka mitano ambao ndiyo utatuongoza katika uhai wa Bunge letu la Kumi na Moja. Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake ameonesha vipaumbele mbalimbali ambavyo vinatuongoza katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa nchi ya watu wa kipato cha kati. Mikakati yenyewe utaiona katika ukurasa wa 25, ambapo amesema Serikali imeweka mikakati ya kujenga na kuboresha miundombinu wezeshi na mambo mbalimbali ambayo ameyasema hapo.

Mheshimiwa Spika, napenda zaidi nijikite katika suala la mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma na mradi wa chuma wa Liganga. Ulimwenguni pote maendeleo tumeyasoma katika historia na katika vitabu mbalimbali yanasema dhahiri kwamba mageuzi yalitokana na ugunduzi wa moto na ugunduzi wa chuma. Sasa makaa ya mawe yanahusika na uzalishaji wa chuma. Uzalishaji wa chuma hapo hapo tunapata chuma na umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sasa Serikali ikiwezekana ilitazame vizuri suala la mradi huu, kwa sababu inaonekana uko katika sehemu mbili; unaweza ukainufaisha Wizara ya Nishati na Madini na vilevile Wizara ya Viwanda. Kwa bahati mbaya sana, inaonekana mkazo hauwekwi katika kuhakikisha kwamba huu mradi wa chuma wa Liganga unafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa vipi Serikali imeweza kufanikiwa kujenga lile bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam ikaacha kitu muhimu cha kufanikisha uchimbaji wa chuma? Hiki chuma kinaweza kikatusaidia katika mapinduzi ya viwanda. Maana viwanda vinajengwa kwa kutuma chuma, reli tunaweza tukaijenga kwa kutumia chuma hicho hicho, bandari, madaraja na kila kitu, nondo mbalimbali zinaweza zikapatikana kutokana na chuma. Hata sasa hivi nchi hii ina maradhi na *cancer* mbaya sana ya vyuma chakavu. Watu wanachukua vyuma kutoka kwenye madaraja, kwenye kila sehemu na matokeo yake sasa kunakuwa na uharibifu mbaya sana kwenye miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kurahisisha na kuweza kuzuia watu kutoka kwenye eneo la kwenda kuchukua vyuma chakavu katika maeneo ya barabara; unakuta alama za barabarani zinaondolewa, madaraja yanabomolewa; ili watu waweze kuchukua vyuma kwenda kuuza kama vyuma chakavu, kwa nini Serikali isije na mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba chuma cha Liganga kinachimbwa na upatikanaji wa vyuma hivi ukawa ni mwepesi ili kuweza kurahisisha viwanda vya aina mbalimbali; vidogo, kwa vya kati na vikubwa viweze kujengwa katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la reli ya kati. Reli ya kati ni reli ambayo ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yetu na sehemu ya kupumulia kwa Bandari ya Dar es Salaam. Bandari yetu ya Dar es Salaam ina changamoto kubwa, kwa sababu ndiyo lango kuu la uchumi wa nchi hii pamoja na nchi jirani ambazo ni *landlocked,* kama nchi ya Congo, Zambia, Malawi, Rwanda, Burundi mpaka Uganda; watu hawa wanategemea Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, badala ya Dar es Salaam kutegemea tu barabara itakuwa kwa kweli inazidiwa kimashindano na bandari nyingine za nchi jirani. Kwa maana hiyo, naunga mkono kwa dhati kabisa ujenzi wa reli ya kati na reli

nyingine zote zinazokwenda kaskazini huko, Arusha na Kilimanjaro pamoja na reli mpya ya kutoka Mtwara kwenda Mbambabay. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ifanye kila linalowezekana hata kama ni kwa kukopa, pamoja na kwamba deni linaonekana linaongezeka kuwa kubwa, naamini kwamba hawa watakaokuja kuwepo, watakuja kulipa wakati utakapotimia, lakini fedha tunazozikopa tuziweke katika vitu ambavyo tuna imani kwamba vitakuja kuwa ni vya kudumu na wao watakaokuja kulipa walipe wakijua kabisa kwamba sisi tuliokuwepo tulisimama vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua Serikali inayo mpango mzuri wa kujipanga kukusanya mapato na tunaamini kwamba nia njema hiyo itaungwa mkono pamoja na Bunge letu Tukufu na naamini kabisa kwamba tutaweza kufanikiwa kwa kutekeleza hii mipango ambayo tumejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika suala la utalii. Habari ya utalii inaeleweka wazi kwamba ndiyo imekuwa ni chanzo cha fedha za kigeni. Kwa ujumla nashukuru kwamba, Serikali imefanikiwa kuwa inaboresha huduma hizi za utalii na matokeo yake watalii wanazidi kuongezeka. Vile vile nina changamoto katika mapori ya akiba ambayo yapo katika nchi hii. Mojawapo ya pori, lipo katika Wilaya yangu ya Mbogwe, pori la Kigosi Myowosi, tumechangia na Mkoa wa Kigoma pamoja na Wilaya nyingine za jirani za Kahama na Bukombe.

Pori hili Serikali ni sawa na kama imelitekeleza na matokeo yake sasa kunakuwa na shida, vurugu za kila aina kwa sababu wananchi wanapeleka huko mifugo kupata malisho, lakini ukiangalia Serikali yenyewe haijaweka miundombinu wezeshi ya kuweza kuwafanya wananchi waweze kuona kwamba kuwepo kwa hili pori kuna faida kwao, kwa maana ya utalii lakini badala yake wanaona ni bora waingize mifugo yao mle na wakati mwingine hata kulima kwa sababu Serikali yenyewe ambayo imelitenga hailiendelezi.

Kwa hiyo, nashauri tu kwamba, Serikali kama kweli ina nia njema, basi ile mamlaka ya mapori ya akiba ambayo tuliambiwa kwamba sheria yake italetwa hapa Bungeni, basi ije haraka ili iweze kutusaidia kujua kwamba kweli haya mapori sasa Serikali ina chombo kinachoyaangalia na kuyaendeleza.

Mheshimiwa Spika, niseme kuhusu suala la maji ya Ziwa Victoria, Wilaya yetu ya Mbogwe na Mkoa wa Geita tuko karibu na ziwa victoria na kwa maana hiyo nashauri kwamba uwepo mpango kabambe wa kuweza kuzipatia Wilaya zilizo jirani na hili ziwa huduma ya maji kutoka katika Ziwa Victoria. La mwisho, nizungumzie habari ya Wilaya na Mikoa mipya ambayo Serikali imeanzisha kama maeneo mapya ya utawala ili kuweza kuhudumia wananchi kwa karibu zaidi.

Mikoa hii na Wilaya hizi zinazo changamoto mbalimbali ambazo zinatakiwa ziingizwe katika mpango wa miaka mitano ili kuhakikisha kwamba wananchi hawa ambao wamesogezewa hizi huduma, wajisikie kwamba kweli Serikali inawatendea haki. Kwa ajili hiyo, basi kuwe na mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba zinatengwa fedha madhubuti kwa ajili ya ujenzi wa huduma mbalimbali zikiwemo majengo ya utawala, hospitali na miundombinu mbalimbali inayohusiana na utoaji huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Suala la madini pia liko katika Wilaya yangu. Wachimbaji wadogo wadogo katika Wilaya yetu ya Mbogwe tunayo madini ya dhahabu na kuna *Resolute* wanafanya utafiti lakini wamekuwa wakifanya utafiti muda mrefu sana matokeo yake sasa kunaanza kuwa na ugomvi kati ya wananchi na huyo mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Nishati na Madini ihakikishe kwamba kwa kweli huyu mwekezaji anaanzisha mgodi, la sivyo arudishe leseni yake wananchi wengine wagawiwe ili waweze kuchimba na kuweza kujinufaisha katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naomba nikupongeze kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. Ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele. Sasa kama nilivyosema mwanzoni, ni zamu ya Mheshimiwa Upendo Peneza na atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenisaidia na nimeweza kupata nafasi ya kuwa mwakilishi ndani ya Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nichukue muda huu pia kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa sababu katika kikao kilichopita niliuliza maswali kutokana na madhara mbalimbali yanayowapata wananchi wa Geita Mjini kutokana shughuli za mgodi na aliwajibika kama alivyoahidi ndani ya Bunge lako Tukufu kufika na kuongea na wananchi, kutembelea sehemu za waathirika.

Mheshimiwa Spika, nina imani hatua tuliyofikia hatimaye hawa wananchi yawezekana wakaondolewa katika eneo husika, lakini pia ataweza kuwasaidia vijana wengi waliojiunga na ushirika na wataweza kupewa maeneo ya kuchimba dhahabu katika maeneo ya Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika huu Mpango, tunazungumzia sana maeneo ya viwanda na katika kuangalia eneo kubwa la viwanda, katika Mpango wanaonesha ni jinsi gani ambavyo Serikali imejipanga na kuwekeza katika maeneo ya viwanda. Wameongelea maeneo ya *EPZ* na *SEZ,* wameongelea pia maeneo ya *industrial park.* Vile vile ukisoma ule Mpango wa mwaka mmoja ulikuwa unazungumzia ni namna gani hizi *EPZ* na *SEZ* hazijaweza kuchangia vya kutosha katika pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Spika, tukiongelea masuala ya viwanda, tunaongelea mambo ya *EPZ,* lakini tunawapa watu maeneo makubwa ya kuwekeza, hawa watu pia tunawapatia misamaha ya kodi. Kwa hiyo, tunawapa maeneo ya kuwekeza lakini bado kama Serikali tunapoteza kodi. Kwa hiyo, ni vizuri pia Serikali ikaliangalia hili suala kwamba tunasema kuweka viwanda lakini kitu cha kwanza tuboreshe vitu vya msingi ambavyo ndivyo vinavyohitajika ili kuweza kupunguza kutoa misamaha ya kodi.

Katika hotuba ya Kambi ya Upinzani, imeweza kuonesha ni jinsi gani katika upande wa nishati ongezeko lilijitokeza katika Mpango uliopita ni kidogo, lakini pia katika miundombinu kwa maana ya barabara na vile vile hata katika kilimo ukuaji bado ni mdogo. Hata hizi *EPZ* zenyewe, bado wanaagiza hata *raw materials* wanazozitumia katika viwanda vyao. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie kama Serikali kuweza kuwezesha kwanza nishati, tuwezeshe miundombinu na ndipo tukimbilie kwenye viwanda ili tuweze kuondokana na misamaha ya kodi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie upande wa mapato ndani ya Serikali. Serikali imeonesha kwamba kuna upungufu na tunashindwa kutekeleza mambo mengi kutokana na kutokuwepo na mapato ndani ya Serikali yetu. Katika Sheria ya *Local Government* ya mwaka 1982 inaonesha kwamba Halmashauri zetu *(local government*), zitaweza kukusanya fedha ya asilimia 0.3 ya *Service Levy* katika maeneo hayo kutokana na shughuli za mgodi ama shughuli za uwekezaji wowote ule unaokuwa katika maeneo ya Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, sheria hiyo pia imetoa kipengele ambacho Waziri ana uwezo wa kufuta kile kipengele cha 0.3 ya *Gross Revenue* na badala yake wanatoa kiwango ambacho wawekezaji hao wanalipa ndani ya Halmashauri husika. Kwa hiyo, tunapoteza fedha, tunapoteza mapato makubwa kutokana na sisi wenyewe kuzichezea sheria zetu na kutosimamia yale mambo ambayo tumeyapanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Service Levy* hata hizo kidogo ambazo zimelipwa, tunashindwa kuona ni namna gani, kama Serikali kuu inaweza kusimamia kule chini ili angalau hii *Service Levy* inayotolewa 60% ya hiyo *Service Levy* iweze

kutumika katika shughuli za maendeleo. Vile vile bado kama Serikali haiwajibiki kuhakikisha ya kwamba kiwango ambacho kinastahili kulipwa ili 0.3 ya *Gross Revenue* kuweza kui-*determine*, Serikali haiwajibiki kuwasaidia Halmashauri katika ku-*determine* hilo ili kuhakikisha kama Serikali na kama nchi tunapata mapato husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naomba nimpongeze kwa moyo wa dhati sana, kwa jitihada yake ya kusema ya kwamba watu walipe kodi. Binafsi kila nikienda sehemu, tunatafuta risiti tuweze kulipa kodi. Sasa kuna tofauti mbili kati ya Mwalimu Nyerere na Magufuli. Kuna tofauti moja tu, wote wanawapenda wananchi na tunawasikia na wanatamani kuona mabadiliko ndani ya wananchi, lakini Mwalimu Nyerere alianza kwake; kama ni kupunguza mshahara alianza kupunguza wa kwake akafuata wa wengine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, namwomba pia Mheshimiwa Rais kwa kushirikiana na Serikali yake, mshahara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haukatwi kodi ya aina yoyote ile. Kwa hiyo, nachukua pia fursa kuiomba Serikali iweze kuliangalia hili suala kwamba inawezekana kabisa kwamba labda fedha ambazo Mheshimiwa Rais anastahili kupata ni kidogo au hizo alizozitaja Shilingi milioni 9.5 ni kidogo, lakini siyo kukwepa kodi au kumwekea msamaha wa kodi kwa maana inaonesha kama ni upendeleo wa aina fulani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuwajibike kama Serikali, tuweke kodi kwenye mshahara wa Mheshimiwa Rais kwanza na kama ni kuboresha, iwe hatua inayofuata ili tupate ile *leading by example,* wananchi waweze kuwajibika kwenye kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna masuala ambayo yameongelewa katika Mpango, suala la *monitoring and evaluation.* Katika shughuli zetu za Kamati, mimi binafsi nimeona shida ambayo imejitokeza kule.

Kuna maeneo ambapo Wizara na katika Mpango inaonesha kwamba Waziri wa Fedha anasema, watashirikiana na Wizara nyingine kuhakikisha kwamba usimamizi huu au *monitoring and evaluation* inafanyika katika maeneo yote na Wizara zote. Hata hivyo, kuna shida ya hii *decentralization by devolution.* Binafsi naiona kama vile ina tatizo kwa sababu Wizara inashindwa kwenda kuwajibisha watu moja kwa moja kule chini. Kwa hiyo, naomba… *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Taarifa!

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Waziri TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze mchangiaji, anachangia vizuri sana, lakini kwa nia njema tu nimtaarifu juu ya anachokisema kuhusu mshahara wa Rais, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ukurasa wa 62 Ibara ya 43(2) inasema hivi: "Mshahara na malipo mengineyo yote ya Rais havitapunguzwa wakati Rais anapokuwa bado ameshika madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii." Kwa hiyo, kimsingi havitapunguzwa.

Mheshimiwa Spika, *essence* yake nini? Rais aliyepo leo anaweza akaweka masharti ya mshahara wa Rais anayekuja, lakini akishaanza yeye, hayawezi yakazunguMzwa. Jamani, hii ni Katiba, kwa hiyo, nilitaka tu kwa ajili ya ufahamu, pia nitoe taarifa nzuri tu, siyo kwa maana ya kuzusha mjadala, lakini nilitaka ku-*cite* ili kutokee uelewa wa jambo tunalolizungumzia. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Taarifa!

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Spika, hoja yangu ilikuwa ni kwenye mshahara wa Rais utozwe kodi, lakini pia vile vile kama Mheshimiwa Rais alituambia mshahara wake ni Shilingi milioni 9.5 sijui kama aliupunguza ama ilikuwaje, hilo mtatufafanulia ukoje, mimi binafsi siwezi kulisemea hilo. Hoja yangu ni kwamba mshahara wa Rais utozwe kodi, *leading by example,* yaani kuongoza kwa mfano. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee katika hoja zangu nyingine. Nilikuwa nimeishia kwenye upande wa *decentralization by devolution,* naomba pia hilo liweze kufanyiwa kazi. Huu mkanganyiko uliopo kati ya TAMISEMI na Wizara uweze kuondoka ili Wizara iweze kufuatilia mpaka kule chini tuweze kuona mambo yanaendaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna upande huu wa maendeleo ya watu. Naomba nizungumzie kipengele cha makazi bora. Naomba niishauri pia Wizara kama inawezekana ipunguze kodi kwenye vifaa vya ujenzi ili wananchi wapate kujenga nyumba nzuri na badaye Serikali iende ikatoze kodi kwenye kodi za majengo. Tuwasaidie wananchi wetu waishi kwenye nyumba nzuri, wasipate magonjwa wasipate kuumwa na wadudu mbalimbali na waweze kufanya kazi vizuri kwa sababu watakuwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, kuna mahusiano makubwa sana kati ya makazi bora na afya za watu, pia katika upande wa elimu, upande wa wanawake, naomba pia Wizara iangalie kutenga fedha kwa ajili ya wanawake, tuweke suala la *equity* kwenye elimu.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali, imeweka msamaha wa kodi kwenye *sanitary towels* kwa upande wa wasichana, lakini sasa Serikali iweke fedha ya kusambaza *pad* mashuleni ili watoto waweze kusoma na wasikose muda wa darasani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni kwenye upande wa *good governance*. Ili tuweze kuongoza vizuri kama Taifa, tunahitaji sana kuwa *transparency*, tunahitaji sana kuwa na *accountability*.

Mheshimiwa Spika, namwelewa Mheshimiwa wangu Rais John Pombe Magufuli ana nia njema sana, sana; lakini hiyo nia njema lazima iendane na *transparency*. Hatuwezi kuwa na Bunge ambalo linachuja taarifa! Yaani Bunge ambalo linafanya *parental control* ambayo inaenda kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuwa na Bunge ambalo hawataki wananchi waelewe Wawakilishi wao wanasema nini. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali mliopo hapa, mzingatie suala la *transparency*. *Transparency* ikiwepo, *accountability* itakuwepo na utumbuaji wa majipu hautahitaji Rais aende kila mahali, lakini wananchi wakiwa na taarifa husika, watawatumbua wao wenyewe katika maeneo yao, hata Wabunge wasiowajibika na wenyewe wataweza kushughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia hata Bunge lenyewe, tuchukue zamu zetu, tuwe wazi na tuweze kufanya kazi kwa uzuri na kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Upendo. Wabunge vijana hao! Ila nilikuwa najiuliza, hivi Bunge lisilo na *transparency* ni lipi? Hili la Ndugai au la Manzese huko? Mimi nadhani ni la sijui wapi huko!

MBUNGE FULANI: La hapa Dodoma!

SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh, tusikie kidogo kutoka Zanzibar.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nami napenda niungane na wachangiaji wenzangu, kwanza kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuwasilisha Mpango mzuri, Mpango ambao unaonekana una mwelekeo, Mpango ambao unatia bashasha Watanzania kutoka hapa tulipo kufikia malengo ambayo Mheshimiwa Rais ameyaweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vigumu sana kuzungumzia Mpango huu kwanza bila kutambua na kufahamu kwamba Mheshimiwa Rais ana nia ya dhati ya kuwapenda Watanzania ya kuwatoa Watanzania kwenye hali waliyonayo waende kwenye hali nzuri zaidi. Itakuwa ni kitu cha ajabu sana kuzungumzia mshahara wa Rais. *What is* mshahara wa Rais? Ni mtu ameajiriwa na Watanzania, anapata mshahara na ni Rais wa kwanza katika historia hapa nchini aliyetangaza mshahara wake hadharani. Napenda tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa hilo kwanza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda nilipongeze Bunge lako pamoja na Waziri wa Habari, Michezo na Utamaduni, kwa sababu suala la kuonekana kwenye TV, Watanzania lengo lao siyo kuona kwenye *TV,* wanataka kuona nini Wabunge tunafanya ili kuwatumikia wao. Hii inaonekana kwa vitendo, haionekani kwa maneno ya kuja hapa na kupiga porojo. Naomba Watanzania wote watuelewe kwa hilo na wameshaanza kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nikwambie, hapa Bungeni hata vijembe vimepungua kwa sababu hakuna anayewaona kule. Mbwembwe zote sasa hivi hakuna anayewaona kule! Ndiyo maana wamekuwa wapole. Nami nasema hivi, watulie tuwanyoe taratibu. Maana ukitaka kunyolewa, tega kichwa chako unyolewe taratibu. Tujengane hapa kwa hoja, tupingane kwa hoja na siyo kwa mbwembwe ambazo haziwasaidii Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wanaona majipu yanatumbuliwa! Mimi nasema hivi na bado, yazidi kutumbuliwa zaidi. Kwa sababu, Watanzania wanasema hivi, moja ya sekta ambayo imekuwa ikisumbua ni Sekta ya Utumishi wa Umma. Kuna baadhi ya watu walishajigeuza kuwa miungu watu, hawaguswi! Sasa majipu yameanza kutumbuliwa, wengine wanasema aah, msitumbue watu, msifanye hivi, mnakiuka haki, haki gani? Haki ya kuwanyima Watanzania haki yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema acha watumbuliwe majipu na vipele na matambazi na wao kama wanataka, waendelee kutumbuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mpango huu, napenda nimsifu Mheshimiwa Rais. Mpango wa Kwanza uliokwisha, ulikuwa wa Shilingi trilioni 44.5. Huu ni wa Shilingi trilioni 107. Uone jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais na Serikali yake amejipanga kuwatumikia Watanzania. Hivi mnataka nini zaidi hapa jamani? Mnataka tutoke hapa twende wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mtu ambaye atakuwa na matatizo au upungufu wa akili kidogo, kama ataona Mpango huu unakuwa na kichefuchefu kwake.

TAARIFA

MHE. MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Taarifa! Kanuni ya 68(8).

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Chegeni, kuna taarifa.

MHE. MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kumpa Taarifa Dkt. Chegeni kwamba majipu yote yanayotumbuliwa yametengenezwa na CCM na ni majipu ya CCM naye akiwemo. *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Chegeni, unapokea Taarifa hiyo?

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, wala siipokei kwa sababu ameeleza tu, amezungumza hapa, lakini tutaendelea kuyatumbua yawe yako wapi, yako kwenye shavu, yako wapi yatatumbuliwa tu. Hata wanaosema hawa na wenyewe wengine ni sehemu ya majipu! *(Kicheko/Makofi)*

MBUNGE FULANI: Wewe! *(Kicheko/Makofi)*

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, nao ni sehemu ya majipu! Kwa hiyo, wasione haya! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye mpango wa miaka mitano huu ujao kwa sababu haya ni mambo ya msingi. Nchi hii ili tuweze kutoka hapa tulipo, ni lazima kwanza tuangalie mfumo mzima wa kukusanya kodi yetu ili kila Mtanzania alipe kodi na ashiriki kwenye uchumi wa nchi hii. Huwezi kujenga uchumi wa nchi bila kuwa na mfumo mzuri wa kukusanya kodi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii; kwa kweli, ukiangalia sasa hivi licha ya Wahisani na baadhi ya watu mbalimbali wameshindwa kuanza kutupa pesa zao, lakini mapato yetu yameweza kupanda kutoka Shilingi bilioni 850 kwa mwezi mpaka Shilingi trilioni 1.3 kwa mwezi; hii ni *achievement* moja kubwa sana kwa nchi, lakini imepatikana siyo kwa sababu ya mambo ya rojorojo, ni kwa sababu moja tu ya kutumbua majipu. Haya majipu nayo yalikuwa ni tatizo! Ndiyo maana ukusanyaji wa kodi umeweza kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchumi huu wetu, naomba Mheshimiwa Waziri alielewe hili; tunahitaji tukusanye kodi kutoka vyanzo vingine mbadala. Tusiwe na msingi wa kudhani kwamba ni kupandisha tu kodi kwenye vitu vilevile, hapana! Tubuni vyanzo vingine mbadala vingi vya kuweza kutupatia kodi. Kwa mfano, haya wa Makampuni ya Simu. Makampuni ya Simu, watu wa *TCRA*

walishawaonesha watu wa *TRA* kwamba kodi yenu kwa mwezi ni kiasi fulani, sasa kwa sababu mpaka *Finance Bill* ije, ndiyo kodi iweze kubadilishwa; naomba tuanze kutafuta namna ya kufanya *adjustments!* Haiwezekani hawa watu wanafanya biashara hawalipi kodi stahiki na hili ni pato moja kubwa sana kwa nchi hii na hawa watu wanakwepa sana kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana kupitia Bunge lako hili, mfumo mzima wa ukusanyaji wa kodi kwa Makampuni ya Simu ni lazima sasa ubadilike, lakini hauishii pale. Hawa watu wamejenga minara kila kona nchi hii. Kuna Halmashauri hazipati *Service Levy* kutoka kwenye minara hii! Unakuta minara imetapakaa, lakini Halmashauri haipati chochote! Hivi hii inakwenda wapi? Ni lazima Halmashauri zetu ziweze kupata kodi kutokana na hii shughuli ya biashara ya minara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii ili tuweze kupanua uchumi wetu, ni lazima tuweke miundombinu iliyo sahihi. Huwezi ukazungumzia uchumi wa nchi hii bila kuzungumzia reli. Lazima reli ifufuliwe na kutengenezwa kwa kiwango kinachostahili cha *standard gauge* ili sasa mizigo iweze kusafirishwa kutoka bandari zetu, kutoka mikoa yetu, ukianzia Mtwara kwenda Mchuchuma, ukitoka Dar es Salam kwenda Kigoma, ukitoka Dar es Salaam kwenda Tanga, Mwanza na yote ile inaleta *connectivity* ya mawasiliano katika nchi na ili tuweze kupunguza gharama katika utengenezaji wa barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *repair* ya barabara ni gharama kubwa sana. Leo hii barabara ya Chalinze imekuwa kama chapati, kwa sababu magari mengi yanapita pale pale. Kila kukicha unakuta barabara inaharibika! Vile vile na magari ya mizigo mikubwa yanapita pale. Kwa hiyo, naomba sana hili suala la miundombinu na hasa reli tuweze kuipa kipaumbele katika mkakati wetu wa kufufua uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya maeneo, kwa mfano Kanda ya Ziwa. Wenzetu wa Mbeya wana Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe. Historia yake ukiingalia, ilikuwa ni hela za kujenga uwanja wa Mwanza, ikaonekana hazitoshi zikahamishwa kupelekwa uwanja wa Songwe Mbeya. Mwanza ile ni *hub,* Uwanja wa Ndege wa Mwanza naomba upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kutoka Mwanza kwenda Serengeti ni kilometa 140, umefika kwenye geti la Serengeti ambapo hata ndugu yangu Mheshimiwa Heche pale na watu wanaokwenda huko akina Mheshimiwa Esther Matiko, ndiyo barabara yao wanapokwenda kule. Unakuta unatumia kilometa 380 kufika kwenye geti la Serengeti kutokea Kilimanjaro, wakati Mwanza ni karibu. Kwa hiyo, naomba sana *Mwanza Airport* iweze kukamilika ili iweze kufufua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naamini kwa kuwa na uwanja wa ndege wa Mwanza itasaidia sana kuleta biashara, itasaidia sana kusukuma uchumi wa Kanda ya Ziwa. Leo hii kwenda Nairobi inabidi pengine upitie Dar es Salaam ndiyo uende Nairobi kwa sababu, ndege hakuna. Kwenda Kampala, inabidi uje Dar es Salaam ndiyo uende Kampala na kadha wa kadha. Naomba sana, uwanja wa ndege wa Mwanza uweze kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya vipaumbele ambavyo tunavyo, lakini suala la kilimo; unaposema tufufue uchumi wa viwanda, ni lazima iwe *based* na *agromechanics* na *agroeconomy*. Sasa hii yote itasaidia sana kufanya wakulima ambao ni wengi zaidi wa Tanzania waweze kuzalisha mazao yatakayochakatwa na kuongezewa thamani, itaondoa na tatizo la ajira kwa vijana, itaondoa na tatizo la kupata kipato kwa watu. Naomba sana suala hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la uvuvi na mifugo. Mimi najiuliza, tunachoma nyavu moto, lakini nani analeta nyavu hizo na zinapitia wapi? Kwa sababu huyu mvuvi yeye hana kosa! Amekwenda dukani, amekuta nyavu zinauzwa, ananunua. Sipendi kusema kwamba, tuwaambie watu wafanye uvuvi haramu, lakini hizi nyavu zinaingia hapa nchini na mnajua zinaingiaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi, wanaoingiza nyavu ambazo hazistahili, basi zipigwe marufuku ili kuondokana na tatizo la kuanza kuwatia hasara wavuvi. Mtu amewekeza kwa shilingi kadhaa kwenye mtaji wake pale, halafu mnakuja mnashika nyavu mnachoma! Hii siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali yetu tuliangalie hilo na hasa nikizingatia kwamba Mheshimiwa Rais amekuja na nia thabiti sana kuwatumikia Watanzania na naomba Waheshimiwa Wabunge wote tumuunge mkono. Kwa kupitia bajeti hii naomba kwa kweli, tujipambanue nayo kwamba ni bajeti ya kumsaidia kila Mtanzania. Kipindi hiki ni kipindi ambacho siyo kizuri sana kwetu, lakini lazima tukubali kwamba mabadiliko yoyote yanahitaji kidogo watu kuumia. Tuumie, lakini kwa nia njema ya kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watu wanaweza wakawa wanasema kwa kubeza eti kwamba Mheshimiwa Magufuli ni nguvu ya soda, nawashangaa sana! Mheshimiwa Magufuli ana nia ya dhati! Rais wetu tumemchagua kwa kura nyingi sana, Watanzania wamemwamini na niwahakikishie kwamba amekuwa siku zote anaonesha dhamira yake ya kuwatumikia Watanzania. Kama kuna watu wana mkakati wa kutaka kubadilisha au ku-*undermine* anachokifanya, tunasema washindwe na walegee! Mshindwe na mlegee kabisa! Mlegee kabisaa! Mjilegeze, mlegee, iwe sawasawa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi, lazima tumuunge mkono! Hataweza kupigana vita hii akiwa peke yake. Waheshimiwa Mawaziri mmeanza vizuri, endeleeni! Sitaweza kuwataja mmoja mmoja, lakini nikianzia kwa Mheshimiwa Lukuvi, kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa Mheshimiwa Mwijage mnamwona kila siku anaweka mambo yake hapa, mnaona! Ukija kwa mzee wa TAMISEMI, ukija kwa Mheshimiwa Mwigulu na wengine wote mnawaona hapa. Timu hii ni nzuri! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ila kuna tatizo moja la kimuundo. Tatizo hili Waheshimiwa Wabunge mlielewe. Leo hii Waziri wa Elimu kwa mfano, anazungumzia mambo ya Sera katika Wizara yake, shughuli zote ziko TAMISEMI. Msingi na Sekondari ziko TAMISEMI, yeye ni wa Elimu ya Juu na Sera. Ukija kwa Waziri wa Afya, yeye anazungumzia Sera. Ukienda kwenye Zahanati, Kituo cha Afya, Hospitali ya Wilaya mpaka ya Mkoa ziko chini ya TAMISEMI! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna haja kupitia Mpango huu. Unajua siku zote mnapoona kuna tatizo, mnatafuta namna ya kuweza kulitatua tatizo hilo. Mimi naona kama kuna tatizo hapa! Kwa hiyo, kuna haja ya kujaribu kuoanisha vizuri na kuhuisha vizuri mfumo wa utendaji kazi ndani ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba wale wote waliokuwa na nia mbaya, walegee na washindwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni. Mheshimiwa Ally Saleh!

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza hakuna mwenye nia mbaya, sote ni wananchi na sote hii ni nchi yetu. Tunachofanya ni wajibu wetu kuikosoa Serikali na kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwenye deni la Taifa. Jana wakati wa *presentation* ya Mheshimiwa Mama Hawa hapa, wakati ilipozungumzwa na Kambi ya Upinzani kwamba deni ni kubwa na kwamba kuna haja ya kufanya *auditing* ili tunapoingia katika Mpango huu ambao utagharimu Shilingi trilioni 107 tujue deni letu kabisa kabla hatujaingia huko, Mheshimiwa Mama Hawa alijaribu ku-*defend* akatoa vigezo vingi vya kuonesha kwamba deni hili bado ni *manageable*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba, wenzetu wengine pia walisema madeni yao ni *manageable*. Bolivia wana mafuta, walisema deni lao ni *manageable,* lakini baadaye wakaingia kwenye matatizo makubwa! Argentina wana uchumi mzuri na ndiyo wanaoongoza kwa uchumi wa ng'ombe duniani, walifikiri deni lao ni *manageable* na waka-*collapse!* Hali kadhalika na Greece! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naungana kwanza na Waziri Kivuli wa Fedha wa Kambi ya Upinzani kwamba ni vizuri Bunge hili likatoa Azimio au tukazungumza kwamba kuna haja ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutufanyia *auditing* ili tujue tunasimama wapi. Katika hizo Shilingi trilioni 107 za kuendesha Mpango, maana yake pia tutakopa. Tumefika hapa kwa ajili ya mikopo ambayo hairudishwi. Kwa hiyo, ni bora wananchi wetu wajue tuna madeni kiasi gani kabla hatujasonga mbele na vipi tutaya-*manage* madeni hayo. Hilo ni la kwanza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusiana na kipato. Tumeambiwa kwamba sasa hivi kipato chetu kwa Mtanzania ni wastani wa Dola 1,006. Kipato hiki tunaambiwa kwamba, ndicho ambacho Mtanzania anapata. Tumekuwa tukisema hapa kwamba kipato hiki hakionekani kwa Mtanzania wa kawaida, ni pesa za makaratasi zaidi; na tunaambiwa kwamba, tunaelekea kwenye kipato cha Dola 3,000, ndiyo lengo letu!

Mheshimiwa Spika, kama mwananchi, napenda tufikie huko na nchi iingie katika kipato cha kati, lakini Mpango haukueleza *base* kubwa zaidi; haujapanua *base* kubwa zaidi ya namna ya kuelekea kwenye kipato hicho kwa kuamini tu kwamba, viwanda ndiyo vitatuletea kipato, lakini ziko sehemu nyingine nchi hii hazihitaji viwanda wala Watanzania wote hawatafanya kazi kwenye viwanda. Kwa hiyo, rai yangu ilikuwa ni kupanua *base*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, naambiwa katika Wilaya ya Lushoto au Mtanzania yeyote anajua kwamba wao wanaongoza kwa mazao ya kilimo, mfano mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Lushoto wanatoka Wakomoro wanakuja pale wanachukua bidhaa wana-*pack* kabisa wanazipeleka Comoro na pengine zinafika mpaka Ufaransa! Sasa kwa nini tuwaachie Wakomoro wafanye kazi hiyo badala ya kuimarisha wananchi wetu tukawapa fedha wakaweza kufanya vitu kama vile tuka-*add value* katika bidhaa zetu za kilimo ili kufikia masoko kama hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, tumeacha *area* moja kubwa sana katika nchi yetu; *area* ya uvuvi. Uvuvi wetu ni wa ndoana, wa hapa karibu karibu. Uvuvi wetu haujawa mkubwa wa kutosha. Nimesema katika Kikao kilichopita kwamba tunashindwa na nchi ndogo ya *Seychelles* ambayo ina watu 100,000 lakini wanaongoza kwa uvuvi wa jodari! Kwa duniani wao ni wa pili!

Mheshimiwa Spika, tuna ukanda wa bahari wa kilometa 1,400 hatujautumika vya kutosha. Jana nilisikia hapa kwamba kuna taarifa kwamba kwenye benki kuna dirisha la kilimo katika mambo ya ukopaji, napenda nione

tunafungua Benki ya Uvuvi, iwe *specifically located* kwa sababu tuna sekta kubwa sana, uvuvi wa kutoka maziwani mpaka kwenye bahari kuu. Kwa hiyo, napenda Serikali ilizingatie hili ili tu-*take* fursa ambayo inaweza ikapatikana.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho nataka kusema, ni kuhusiana na *Mtwara Corridor* au sehemu ya Kusini. Kusema kweli, ingawa hapa Bungeni kwa *observation* yangu, mara nyingi watu wanajivutia Kikanda.

Mheshimiwa Spika, watu wanazungumzia habari ya Reli ya Kati na utaona wengi wanaozungumzia Reli ya Kati maana yake ni watu ambao wanatokea upande wa huko. Kwa fikra yangu nahisi Mtwara *is the next big thing in Tanzania, really!* Yaani kwa kanda ile kule! Hivi sasa kuna gesi, viwanda vinakuja na *capital chemicals* nyingi kutokana na *LNG* ambayo ukitoa gesi maana yake unapata *LNG* na viwanda vya aina nyingi.

Mheshimiwa Spika, pia, juzi juzi nimesoma kwamba yamegunduliwa madini ya *graphite*. Madini haya hivi sasa waliotangaza kugundua ni kampuni ya Marekani na mmoja katika *Board Members* (Stith) ni mtu ambaye alikuwa Balozi wa Tanzania…

MBUNGE FULANI: Wa Marekani!

MHE. ALLY SALEH ALLY: Anaitwa Stiff, anasema *graphite* iliyogunduliwa Tanzania inaweza kuwa ya pili baada ya China duniani, lakini pia inaweza kuwa ya kwanza kuliko hata China. Kwa hiyo, ina maana kuna *potential* kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, jana Waziri mmoja alituambia hapa kwamba kuna mpango wa kilimo cha mihogo ya tani milioni 200 kinakuja na soko lipo, lakini sioni uwekezaji unaofanana; kwa *communication,* unaofanana na rasilimali zilizoko Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumefungua *Corridor* ya Kusini kwa Uwanja wa Songwe. Tuna Uwanja wa Kilimanjaro. Kuna haja sasa hivi ya kuwa na Uwanja wa Kusini wa Kimataifa ili uelekee upande mwingine, tufungue *Corridor* nyingine, katika kila kona ya Tanzania tuwe tuna uwanja ambao unafanana na uwezo na hali tunayosema tunataka tuwenayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nashauri kwamba *the next big thing* kuitazama ni *Corridor* ya Kusini, tujipange vizuri tuweze kuitumia vizuri ili tuweze kufaidika na gesi na vitu vingine ambavyo vinaambatana na mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ninachotaka kuzungumzia ni kuhusu Shirika la Ndege la Tanzania. *Actually* mpaka tulipofika hapa ilikuwa ni aibu sana kwamba nchi hii tumekubali Shirika letu la *National Carrier* kufa na hatukuweza

kulitengeneza, mpaka hivi sasa tunataka kutengeneza kwa kuwa na ndege mbili. Tunasema kwamba tunatarajia kuwa na watalii wengi kwa sababu tutakuwa na ndege mbili. *Actually* kuwa na ndege ni kitu kingine na kupata watalii ni kitu kingine. Unaweza kuwa na ndege, lakini kama huna *routes* zinazofaa na kama hujapata kununua *route* kwa watu wengine na kama hujaweza kuiuza nchi upya, bado utalii hauwezi kukusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na kuwa na ndege mbili, ambazo sifikiri kama itakuwa ni kitu kikubwa sana, lakini kwa maana ya kuanzia angalau tumeanza, nashauri pia, kama tunataka kufufua Shirika la *ATC,* mbali ya kwamba tunatakiwa tufagie *ATC* yote, lakini pia tutafute *strategic partners* ambao wanaweza kutupa *routes* nyingine ambazo tutaweza kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa humu ndani *routes* zetu nyingi tumeshaziuza, tumempa *Fast Jet* kwa *routes* za ndani. Sasa utashindanaje na *Fast Jet* wakati ameshaweza kuji-*establish* kwa muda wa miaka mitatu ambayo yupo hivi sasa na wewe unakuja na ndege mpya? Kwa hiyo, ni lazima tuingie na Mashirika, tuwe na *strategic partners* ambao wataweza kutusaidia kutufungulia njia nyingine.

Mheshimiwa Spika, pia tutafute *model* nzuri ya kuwa na Shirika la Ndege. Ethiopia pamoja na kwamba walikuwa katika kipindi cha Haile Selassie, vita, udikteta, lakini bado ni shirika ambalo lilikuwa haliguswi na ndiyo maana limebaki kuwa shirika la mfano kwa Afrika na linafanya kazi na limekuwa likienda vizuri. Kwa hiyo, tusione aibu kuazima *management* au kuchukua *management* ikaja kutuwekea sawa mambo ili Shirika lile liende katika hali inayoweza kufaa na ikatusaidia sote kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka kusemea ni suala la usalama na utawala bora. Nina mifano michache sana ya nchi ambazo zimeweza kufanikiwa katika kuingia kuwa nchi za viwanda ambazo zimekuwa hazina utulivu au zimekuwa zikiendeshwa na madikteta. Nchi chache kama Singapore na Lee Kuan Yu mfumo wake wa uongozi ulikuwa ni wa kubana lakini ilifanikiwa.

Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo hatuwezi kuliachia hivi hivi. Hatuwezi kuwa na chaguzi ambazo kila mara sauti ya wananchi haisikiki, hatuwezi kuwa na chaguzi ambazo Serikali inapeleka majeshi na inalinda chama kimoja halafu tutarajie kwamba tutapiga hatua katika maendeleo. Kwa hiyo, suala hili ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ningependa ku-*cut across the board* ni suala la *disability,* watu wanaoishi na ulemavu. Hili ni eneo ambalo Mbunge yeyote humu ndani halizungumzi kama vile siyo kesho yeye litamtokea.

Mbunge yeyote hazungumzi, kama vile hatuna asilimia 12 ya Watanzania ambao wana ulemavu wa aina moja au aina nyingine. Kwa hiyo, napenda *program* yote ya Serikali tusiseme tu katika UKIMWI, lakini pia katika *disability,* ika-*cut across* kote ili tuweze kutengeneza mazingira na tuweze kufanikisha ili kuona watu wenye ulemavu wanaweza kuchangia na wanaweza kupata fursa za aina nyingine yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mwisho nataka kusemea juu ya kile ambacho Waziri Simbachawene alikitolea taarifa hapa juu ya mshahara wa Rais. *Actually* aliye-*raise* suala la mshahara wa Rais ni yeye mwenyewe Rais. Ame-*raise* mshahara wa Rais yeye mwenyewe kwa sababu pengine alitaka liwe *publicity stunts* kwamba yeye ni Rais ambaye anapunguza mshahara na kwamba yuko *pro-people* na hivi na hivi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili suala limekuja hapa siyo kwa sababu sisi tumelianzisha, ni kwa sababu yeye alianzisha. Kama itakuwa ilikosewa, ni kwamba waliomshauri walikuwa wamwambie kumbe hawezi kubadilisha mshahara wake akiwa yeye katika madaraka, lakini wanaofuata wanakuwa na madaraka. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa lakini wakati mwingine wananchi wanajua wapi pana *publicity stunts* na wapi ni sifa ya kweli. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh. Nilikuwa nafikiri Kamati ya Mheshimiwa Mwilima ingeangalia uwezekano; au hili niliache kwanza kwa sababu nafikiri lipo kwa Mheshimiwa Jenista. Nilidhani tungeweza kulipa jukumu la mambo ya *disability* kwenye ile Kamati yetu nyingine, lakini yako kwenye Kamati nyingine, lakini tutaangalia namna nzuri zaidi ya sisi kama Bunge kuangalia masuala ya *disability* vizuri zaidi. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo ni Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Mpango huu wa Miaka Mitano unaeleweka vizuri iwapo utasomwa katika *context* yake ya kwamba Mpango huu unatokana na Mpango Elekezi wa Miaka 15. Ukishauweka katika *context* ya miaka 15 unaelewa kwamba kilicholetwa hapa kwa miaka hii mitano ni hatua ya pili ya utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Miaka 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukishaelewa hivyo, unaweza ukapunguza sana kejeli ambazo zinatolewa na baadhi ya Wabunge humu ndani. Hatua ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huu ilikuwa kutanzua vikwazo vya uchumi; ni hatua nzuri ambayo imefikiwa kwa kipindi cha miaka mitano tunachokimaliza msimu huu wa 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, tunapokuja na Mpango wa miaka mitano inayoanzia mwaka 2016/2017, tunazingatia pia uzoefu tulioupata miaka mitano iliyotangulia. Ukiangalia katika Mpango huu, miaka mitano iliyopita ilieleza bayana, pamoja na kutanzua vikwazo vya uchumi, pia kipindi hicho cha miaka mitano iliyotangulia kilienda sambamba na kubaini maeneo ya vipaumbele. Maeneo ya vipaumbele yaliyobainishwa ni pamoja na Miundombinu, Kilimo, Viwanda, Rasilimali Watu, Huduma za Kifedha, Utalii na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapotoka kwenye awamu ya kwanza na tunapokwenda kwenye awamu ya pili ambayo itachukua tena miaka mitano, tumechagua eneo la viwanda kama eneo mahususi la kulifanyia kazi. Mpango huu ukiusoma kwa umakini na ukaulewa, utaelewa ni kwa nini sasa tumechukua viwanda na kwa nini Mpango huu umeitwa kama kipaumbele kujenga misingi ya uchumi wa viwanda? Tunapoongelea viwanda, tunaenda sambamba na miundombinu ambayo itafanya viwanda viimarike lakini biashara iimarike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango huu umebainisha vizuri maeneo ya ujenzi wa barabara, reli, bandari, lakini pia umeeleza miradi mahususi ambayo itaifanya Tanzania yetu iwe Tanzania mpya, Tanzania ambayo inakwenda kujibu kero za vijana, akinababa na akinamama wa Taifa hili. Ukiusoma katika *context* hiyo, unakubaliana nami kwamba Mpango huu wa miaka mitano kama sehemu ya utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Miaka 15, Mpango huu umekaa vizuri kwenda kutatua matatizo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Serikali nzima ya Awamu ya Tano kwa kujifunza kutokana na uzoefu wa miaka mitano iliyotangulia na kuja na Mpango madhubuti utakaolijenga Taifa letu vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninavyouangalia Mpango huu na namna ulivyokaa, nina maeneo machache ambayo ningependa nishauri. Ukiangalia Mkoa wa Ruvuma ambao lango lake lipo katika Jimbo ninaloliongoza, Jimbo la Madaba unaona kwamba Mkoa wa Ruvuma umejaa fursa nyingi sana ambazo kama zitatumiwa vizuri na Mpango huu, kwa hakika Tanzania itakuwa nchi ya neema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo barabara muhimu ambazo zitatakiwa zijengwe na ziimarishwe ili Mpango huu wa viwanda uweze kuwanufaisha wananchi wa Jimbo la Madaba na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla ambao kwa asilimia kubwa wanachangia sana pato la Taifa na wanachangia sana chakula kinacholisha Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Madaba linapakana na Wilaya ya Ulanga, lakini kufika Wilaya ya Ulanga nahitaji kufika mpaka Mikumi na baadaye niende Ifakara ndipo niende Ulanga. Wakati wananchi wangu wa Kijiji cha Matumbi wanatumia siku sita kwa mguu au nne kufika katika Wilaya ya ulanga, lakini wanatumia siku mbili kwa mguu kufika mpakani mwa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba na upande wa pili wa Malinyi.

Mheshimiwa Spika, hicho tayari ni kikwazo kikubwa sana cha uchumi kwa maendeleo ya maeneo yote mawili. Pamoja na kwamba Mpango huu bado haujabainisha nini kitafanyika, haujafafanua, nafikiri kwa sababu Mpango huu una sifa ya kujifunza kwa Mipango iliyotangulia, basi tuendelee kuangalia lile eneo ambalo linapakana na Jimbo la Madaba kama sehemu moja muhimu ambayo itachangia sana uchumi wa wananchi wa maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia imeelezwa vizuri sana kwamba Mkoa wa Lindi unapakana na Mkoa wa Ruvuma, nalo ni eneo muhimu sana kama tunataka kuimarisha uchumi wa wananchi wale kupitia viwanda kwa sababu tunazalisha malighafi ya kutosha, tunahitaji kusafirisha, lakini tutazalisha bidhaa nyingi za viwandani, tutahitaji ziende Lindi, Ifakara, Mahenge na maeneo mengine ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi sana Mbunge aliyemtangulia Waziri Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge Profesa Simon Mbilinyi, aliyestaafu, alianza kuongea sana kuhusu miradi ya *NDC,* hususan mradi wa Mchuchuma na Liganga. Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Peramiho, ambaye sasa kipande cha Jimbo lile kimekuwa Jimbo la Madaba, ninaloliongoza sasa, kwa miaka kumi amesimamia ajenda hiyo ya mradi wa Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Spika, mradi ule kama utafanikiwa kwa kiwango hiki ambacho umeelezwa katika Mpango huu, kwa hakika utatukomboa sana wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, utawakomboa sana wananchi wa Madaba na Jimbo la Peramiho. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, ni vizuri sasa, kwa vile maandalizi ya kuanza ku-*explore* ule mradi wa Liganga Mchuchuma, ni vyema sasa barabara inayotoka Wilaya ya Ludewa kufika Madaba iimarishwe ili kwamba wananchi wa pale waweze kunufaika na ule uchumi, lakini pia ndiyo barabara inayokuja kuunganisha na barabara ya Makambako kuja Dar es Salaam, kwa ajili ya kusafirisha mali na bidhaa zitakazozalishwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tuna usemi wa Kiswahili, Waswahili wanasema, "Siku ya kufa nyani, miti inateleza." Wakati nipo nje ya Bunge hili, kuna wakati nilikuwa naona kuna baadhi ya hoja zenye mashiko kutoka upande wa pili wa upande

wangu wa kulia, lakini kadri ninavyozidi kukaa ndani ya Bunge hili, katika hiki kipindi cha miezi kama sita hivi nimekaa hapa, nazidi kuona kwamba hoja zenye mashiko zinazidi kupungua. Naamini sasa kweli miti inateleza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wakati ambapo hoja ya ufisadi ndiyo ilikuwa mhimili mkubwa wa kushikilia. Leo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John Pombe Magufuli alipoisimamia hoja ya kutumbua majipu na kuondoa mafisadi, wale wale ambao walikuwa wameshikilia hiyo nguzo, wanamlalamikia na wanamlaumu. Ama kweli Waheshimiwa Wabunge ni lazima tujipime wakati mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inanisikitisha sana ninapoona mtu anaji-*contradict* mwanzo hadi mwisho wa hotuba yake. Anaanza na kusema Baraza la Mawaziri halifanyi kazi, halifai. Baraza hili ni lile lile la Awamu ya Nne, wanabadilishana nafasi, halafu baadaye anasema Mheshimiwa Waziri fulani umenifaa sana, unafanya sana kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuishi kwa *contradiction*. Lazima tuwe na *consistent* katika hoja zetu. Leo nimependa sana…

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa!

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, lazima ni-*declare interest*, *approach* aliyoitumia Mheshimiwa Ally Saleh, imetujenga sana na imemsaidia sana Waziri wa Fedha kuweza kuboresha Mpango huu wa Miaka mitano wa Maendeleo. Napenda sana tutumie *approach* hiyo ili kuisaidia nchi yetu na kuwasaidia Mawaziri waweze kutuletea majibu yanayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunalo eneo lingine muhimu sana kwa Jimbo la Madaba…

TAARIFA

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa kanuni ya 68 (8)!

SPIKA: Mheshimiwa Joseph, naona kuna taarifa ambayo haivumiliki.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nitoe taarifa. Naomba nimwambie mchangiaji, haya majipu ambayo wanajisifia, sisi hatujawahi kukataa yasitumbuliwe, lakini tumeongoza vita hii wakiwa wanatuzomea. Nimkumbushe mchango wa Mheshimiwa Wenje hapa…

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Kanuni gani hiyo?

MBUNGE FULANI: …akimzungumza Kabwe alivyozomewa na hawa hawa. Nyie ndio hamna *consistence!* Sisi tunataka tuone majipu yametumbuliwa, nyie ndiyo mnabadilika badilika.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Soma kanuni!

MBUNGE FULANI: Kanuni ya 68(8) ndiyo natoa taarifa hiyo.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Isome sasa!

MBUNGE FULANI: Nimemaliza.

SPIKA: Ahsante sana kwa taarifa yako. Mheshimiwa Joseph Mhagama, taarifa hiyo unaipokea?

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika ahsante. Taarifa hiyo siipokei kwa sababu wale ambao walileta ushahidi ndani ya Bunge hili, mimi nikiwa nje ya Bunge hili, kwamba Mheshimiwa Lowassa ni mmoja katika mafisadi wakubwa, ndio hao hao waliomkumbatia na kwenda naye katika kampeni ya Awamu hii ya Tano. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

MBUNGE FULANI: Wanafiki wakubwa!

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, kwa namna yoyote siwezi kuipokea hiyo taarifa. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mhagama, muda wako umekwisha. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

MBUNGE FULANI: Safi sana!

SPIKA: Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 6.55 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

Naibu Spika (Mhe Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

NDG. CHARLES J. MLOKA - KATIBU MEZANI: hoja za Serikali kwamba sasa Bunge lijadili Mpango wa Pili wa Maendeleo ta Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano, kuanzia mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021. Majadiliano yanaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano kuanzia mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mheshimiwa Vuma hayupo, Mheshimiwa Daniel Mtuka, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mheshimiwa Lucia Mlowe.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia Mpango huu wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitoe masikitiko yangu, kwa sababu nimeupitia huu Mpango lakini wanawake tumesahaulika katika Mpango huu. Wanawake ndiyo jicho la Taifa, ndiyo wachapakazi, lakini sijaona msisitizo au kipaumbele kwa wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na wanawake wajasiliamali, niki-*refer* Mkoa wangu wa Njombe, akina mama wajasiriamali wanahangaika sana, wanajitahidi kufanya biashara zao, wanajitahidi kuanzisha shughuli ndogo ndogo kwenye familia zao, lakini hawapati *support* au mwongozo ambao unaweza kuwasaidia wakasimama. Maana mwanamke akiwezeshwa na akijengewa msingi anaweza kulibadilisha Taifa, hivyo ninaomba kwenye Mpango huu akinamama vilevile waingizwe kwenye kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni juu ya miundombinu. Wabunge wengi wamechangia juu ya tatizo la miundombinu, niki-*refer* Mkoa wangu wa Njombe, sasa hivi mvua zinavyoendelea kunyesha, barabara zinazounganisha Mkoa na Wilaya ya Njombe hazipitiki, na huo umekuwa wimbo wa Taifa, kila kipindi zinapoandaliwa Bajeti naona watu wa Njombe wanasahaulika, na hapa kwenye Mpango sijaona Mkoa wangu wa Njombe kama angalau umefikiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la elimu bure. Elimu bure ni sera ambayo imewafurahisha watu wengi sana hasa wazazi. Lakini kuna changamoto kubwa sana kwenye hiyo sera ya elimu bure, sijaona hapa mkakati wa maandalizi ya walimu ambao watasaidia hasa kwa watoto wadogo, kwa sababu kutokana na hii elimu bure, mwaka huu watoto wengi sana wameandikishwa. Lakini maandalizi ya Walimu hakuna, vyumba vya madarasa hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifikiri hili lingefanyika baada ya kufanya utafiti, lakini hakuna utafiti uliofanyika, matokeo yake sasa hatutakuwa na msingi kwa hao watoto wadogo, watakwenda huko mashuleni watakaa chini, watacheza cheza watarudi nyumbani, mwisho wa siku watoto hakuna watakacho kipata, na hatimaye tunaharibu msingi wa watoto kutoka kule chini, kwa sababu kule chini ndiko kwenye msingi wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata tunapoongelea elimu ya juu lazima tuwe na msingi kule chini, kwa hivyo ninaomba mkakati uoneshwe hapa kwenye Mpango wa Miaka Mitano, kwa sababu ni miaka mitano, sasa miaka mitano maana yake hakuna kitakachofanyika kama hakijaoneshwa hapa, tunaomba Waziri wa Fedha ahakikishe anaingiza Mpango huu au mkakati huu, kwa ajili ya maandalizi ya walimu kwa ajili ya watoto wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu ada elekezi. Shule za *private* ndiyo zinazotupatia heshima katika nchi yetu, kwa sababu wanatafuta mbinu mbalimbali za kuhakikisha watoto wanafanya vizuri. Wanatumia mbinu mbalimbali kwa gharama kubwa, kutafuta walimu huku na huko hata kutoka nje, kuhakikisha wanaleta elimu kwa watoto wetu inayofaa na ndiyo maana shule za *private* ndizo zinazoongoza. Sasa tunapowaletea maelekezo juu ya ada kwamba watoe kulingana na maelekezo yetu tunawakosea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la afya ni tatizo kubwa kwa sababu miundombinu ya hospitali ni mibaya sana. Niki-*refer* Mkoani kwangu Njombe, mwezi wa pili Naibu Waziri wa Afya alitembelea Hospitali ya Kibena na akatoa maelekezo kwamba wahakikishe wanabadilisha au wanaleta mabadiliko na kurekebisha baada ya siku 90 wawe wamefanya kazi hiyo. Lakini ukienda sasa hivi pale Kibena ni majanga, hakuna hata *paracetamol*, hakuna *x-ray,* hakuna hata vipimo vile vingine kwa ajili ya maabara *reagents* hakuna, na miezi mitatu nafikiri tayari huu ni mwezi wa tatu sasa. Kwa hiyo niombe suala hili la afya liangaliwe kwa namna ya pekee, kwenye Mpango huu wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo, Serikali imekuja na sera ya viwanda, lakini huwezi ukawa na viwanda kama hujaandaa mazao. Wakulima wetu wamekuwa wakipuuzwa sana. Niki-*refer* Mkoa wangu wa Njombe, mwaka huu wameunguliwa viazi vyao, sikuona jitihada iliyochukuliwa kuwasaidia

wakulima hawa na ni kilio kikubwa sana kwa Mkoa wetu wa Njombe, sikuona Serikali inachukua jitihada ya pekee kuwasaidia wale wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima hawa wamekata tamaa, ningeomba tafadhali watu wa Njombe wafikiriwe, hasa wale wakulima wadogo wadogo, zaidi akina mama ndiyo hasa ambao wanateseka na kilimo, lakini mwaka huu wamepoteza pesa zao, na hawana tena mtaji wa kununua viazi kwa ajili ya mwakani. Niombe suala hili lichukuliwe kama inavyochukuliwa dharura sehemu nyingine au kwenye matukio mengine, mara nyingi yanapotokea mafuriko au nyumba zinaezuliwa, kuna pesa au kuna msaada wa dharula ambao huwa unatolewa kwa watu hawa, niombe hata Njombe wakulima wapate msaada kama huo kwa sababu hiyo kwao imekuwa janga.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mazingira hasa kwa Mkoa wangu wa Njombe kwa kweli yanatisha, hasa kwa upande wa takataka au karatasi *plastic*. Sijaona mkakati ambao unaonesha kwamba suala hili litaweza kushughulikiwa kwenye Mpango huu, imedokezwa kidogo sana, lakini mimi niombe suala hili liingizwe tena litiliwe mkazo, kwa sababu kweli takataka au makaratasi ya *plastic* pamoja na chupa za *plastic* ni majanga. Kila kona unakuta kuna chupa za *plastic,* siyo makaratasi tu lakini hata chupa za *plastic* za soda na *juice* zimetupwa kila kona. Hivyo ningeomba huku kwenye Mpango basi ioneshwe kwamba Serikali itachukua hatua gani kuweza kukomesha suala hili la *plastic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tuna tatizo kubwa la utoaji taka, kwenye mashimo ya takataka. Nili-*fight* na Mkoa wangu wa Njombe, takataka zinajaa, zinafurika, ukiuliza Mkurugenzi anasema gari ni moja kwa hivi inashindikana kutoa takataka hizi, hivyo basi ningeomba suala la mazingira litiliwe mkazo. Vilevile juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji, naomba vilevile lisisitizwe kwenye Mpango huu, kwa sababu ndio madhara hayo tunayoyaona sasa ambayo yanatuathiri, mabadiliko ya hali ya hewa, ni kutokana na mazingira yasiyo rafiki kwa binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushuru, wajasiriamali wengi wanakata tamaa kwa sababu ya ushuru na kodi mbalimbali au tozo mbalimbali, kwa mfano, wajasiriamali wa Njombe, hasa pale Njombe Mjini, kwa kweli wanatia huruma. Mtu ana nyanya anatembeza kwenye sinia ameweka kantini yake ndogo hapo, lakini anatozwa hela nyingi sana, naomba hili liangaliwe kwa hawa wajasiriamali wadogo, wasaidiwe na hii ningeomba ioneshwe kwenye Mpango, ni namna gani hawa wajasiriamali watasaidiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mlowe muda wako umekwisha.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatib Said Haji.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninamshukuru Mungu kunijalia na mimi leo kuwa mchangiaji katika hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu tumekuwa tukipanga mipango kadhaa, waswahili wanasema mpango siyo matumizi, tumekuwa tukipanga lakini hatutumii, ni vema tujiulize tunapokosea ni wapi katika mipango hii, bila shaka kuna makosa tunayoyafanya ambayo yanatupelekea tunapanga vizuri lakini hakuna matokeo mazuri ya mipango yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii katika Mpango kuna jambo zito kubwa sana ambalo linajielekeza kuifanya Tanzania iwe ni nchi ya uchumi wa viwanda. Kusema tumesema sana juu ya hili na siyo mwanzo leo kusema kwamba nchi hii haiwezi kuendelea bila kuwa na mpango madhubuti wa kuendeleza viwanda vyetu. Leo hii yalaiti mimi nataka niseme wazi CCM mmemsaliti Mwalimu Nyerere, mimi siko radhi na Watanzania hawako radhi, mmemsaliti Mwalimu Nyerere kwa nini, kwa sababu Mwalimu Nyerere nchi hii alijitahidi kuwaonesha mfano, kwamba viwanda ndiyo vitakavyotutoa hapa tulipo na kwenda mbele. Matokeo yake mmekuja na sera zenu za ajabu, mmeua viwanda vyote, sasa mnafufua viwanda kwa maneno matupu, neno tupu hakuna utekelezaji unaofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ndugu yangu Mheshimiwa Silinde, alizungumzia habari ya kusema lengo la Wachina kujenga pale Kurasini *Logistic,* ni kuifanya nchi hii kuendelea kuwa madalali, dampo ni kweli! Lakini imekosolewa vikali, hata mimi nataka niseme kwamba Mheshimiwa ndugu yangu Silinde mzoea udalali hawezi kazi ya duka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukubaliane nao hivyo hivyo, kwa sababu tukisema tunakataa Wachina kujenga pale, uwezo wa kujenga viwanda *kushnei*, hakuna! Tutasema tumekaa humu, tutapita, watakuja na watakaopita, kwa Itikadi hii na utendaji huu wa Sera za Chama cha Mapinduzi, hebu ndugu zangu igeni yale mazuri yetu, ambayo tunawapa mawazo ninyi muyafuate, nchi hii ni yetu wote, nchi hii hakuna kitabu chochote kitakatifu kilichotaja CCM wala CUF wala CHADEMA, vitabu vyote vimewataja waja wa Mwenyezi Mungu atakao waweka sehemu moja aliyopenda yeye, tumejichagulia majina tumejiita Watanzania, wa Afrika katika dunia hii, lakini hakuna hilo andiko liko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposhauri tuna malengo mazuri, nataka kusema kwamba ndugu zangu, tufuateni yale mawazo bila kujali anayeyatoa ni nani. Lile zuri na wewe Mheshimiwa Naibu Spika nimesikia huko, Bwana Mkubwa kamtumbua Wilson Kabwe, jamani tulisema hapa, Ezekiel Wenje alisema mpaka povu likamtoka, ninyi wenzetu huko mlifanyaje, sisi tulikuwa wabaya, leo mnatulaumu eti vyama vyetu hivi vya UKAWA vilimsimamisha Mheshimiwa Edward Lowasa kuwa mgombea wa Urais, Mheshimiwa Edward Lowasa akiwa CCM akitembea mnampokea kama malaika ninyi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninyi alienda Tanga nilikuwepo Katibu Mwenezi wa CCM alimpiga mtu kutaka kumuua kwa sababu kamkaripia Lowassa, kweli uongo? Mliimba nyimbo nzuri za kumpamba, mpaka mkatusadikisha kweli yaweza kuwa yale maneno yetu hatuko sawa, hebu tumuangalie. Leo tumefanya kosa kubwa, miaka yote mliokuwa naye alikuwa mzuri, mbaya kwetu, kwenu kizuri, tutakuwa naye na tutakufa naye Lowassa na Mungu akimuweka 2020 ndiye huyo huyo, mkipenda msipende dozi ni hiyo hiyo, mkinywa mkitema shauri yenu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie jambo moja lililonigusa sana. Mheshimiwa Zungu siyo mara ya kwanza, siyo mara ya pili, siyo mara ya tatu amekuwa akishauri toka Bunge lililopita. Makampuni ya simu yanaiibia nchi, hii nataka niwaulize yeye yule siyo mpinzani, Mheshimiwa Zungu ni Mbunge wa CCM. Mheshimiwa Zungu alichokisema ni kwa maslahi ya nchi hii, mlifanya yapi, mmetekeleza lipi, hamna! Tutawasifu wafanyao mazuri na tutawakosoa wanafanya mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliopewa jukumu la kusimamia suala hili hawajaitendea haki nchi hii, kama mu-watumbuaji wazuri wa majipu angalieni hili siyo jipu ni busha! Lazima tuangalie kile kinachokosesha mapato nchi hii, tukiangalia bila kuoneana haya, kuna tatizo gani kuandaa wataalam wetu makini, wakaona ni kwa kiasi gani Tanzania inapoteza mapato kutokana na makampuni ya simu. Yupo nani nyuma ya makampuni ya simu tuambieni, yuko nani? Siyo bure iko sababu. Siyo bure kwa sababu tafadhalini tunayoyasema hapa siyo kwa ajili ya ushabiki ni kwa ajili ya kuisaidia nchi hii, itoke ilipo iende mbele. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia juu ya maamuzi ya kukurupuka yanayochukuliwa na watendaji wa nchi hii. Nchi hii mmeingia mkataba wa himaya moja ya forodha kufanya mizigo ya Congo sasa hivi iwe inalipiwa kwao kabla ya kutoka katika Bandari ya Dar es salaam, jambo ambalo limechangia kushuka kwa makontena katika Bandari ya Dar es Salaam kufikia asilimia 50. Hebu niwaulize tumefanya yale kwa faida ipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nchi ya Congo, mimi niliwahi kuwa mjasiriamali nilikaa pale Congo katika Mji wa Lubumbashi, nchi ile haijasimama utawala wake sawa sawa, pale unaweza kupeleka *containers* akaja Kanali tu wa Jeshi akatoa amri pitisha hizo kontena tano na zinapita. Sasa wafanyabiashara wale wa Congo mnapoweka vile vikwazo ambavyo haviisaidii nchi hii, wametafuta bandari ya Beira, wametafuta bandari za nchi nyingine wameiacha Dar es Salaam imedoda, mnapata faida gani? Mambo ya Wacongo yanawahusu nini ndugu zangu, msiba wa Kichina Mmasai anaingiaje? Waacheni wenyewe sisi tukusanyeni kodi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesoma gazeti moja, nimeona taarifa Serikali inasema kwamba imeliona hili na mnalifanyia kazi, nawaomba sana ndugu zangu shitukeni mapema, kule Beira wakizoea utamu wa kule hakuna atakayerudi hapa, anzeni sasa kuchukua hatua msisubiri kesho na kesho kutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie suala la utawala bora. Suala la utawala bora lina mtazamo mpana sana. Mojawapo ikiwa ni wananchi wenyewe wafaidike na utawala bora wenyewe. Nasikitika kwa kituko ambacho kimefanywa na Serikali yenu ya kuzuia matangazo haya wananchi wa Tanzania wasione wawakilishi wao wanasema nini, amesema mwenzangu hapa mmoja kwamba ule umaarufu Dkt. Chegeni mliokuwa mkiupata kwenye *TV* sasa hamtoupata tena. Kila Mbunge aliyeingia hapa mpaka ukiitwa Mbunge tayari wewe ni maarufu tu, ukaonekana kwenye *TV* usionekane kwenye *TV* wewe tayari ni maarufu tu. Wengine tuna umaarufu wa ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe ni maarufu kwa sababu ni baba watoto nina familia na watoto wasiopungua 12, nina mke wangu ambaye naweza kumfanya Waziri Mkuu, mimi Rais wa familia na watoto wangu Baraza la Mawaziri, siyo umaarufu mdogo huo? Kila umaarufu una ngazi yake, leo umaarufu wangu siwezi kuufananisha na Mheshimiwa Magufuli lakini hata umaarufu wa Mheshimiwa Magufuli hauwezi kuwa zaidi ya Mheshimiwa Barrack Obama, hauwezi kuwa sawa! Kwa hivyo, humu hamna uwezo wa kutupunguzia umaarufu tulionao, mimi ni maarufu, mimi ni Rais kwenye familia yangu, watoto 12 ninao ni Baraza tosha kabisa la Mawaziri na mama watoto Waziri Mkuu wangu, ninataka umaarufu gani tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhalini sana fikirieni tena kwa makini, hatutafuti umaarufu tunataka Watanzania wajue wawakilishi wao waliowachagua wanasimamia vipi yale wanayoelekeza wawakilishe kwa Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo katika utawala bora kwa masikitiko tu ni kwamba leo hii nchi inayoitwa Zanzibar, nilisema kabla ya Bunge hili, kabla ya uchaguzi haramu uliofanyika mara ya pili Zanzibar, nilisema kwamba jamani tufikirieni maneno ya nchi wahisani wanayosema juu ya kuikatia misaada nchi yetu. Hili jambo misaada hii tusikae tukisema tutakula mihogo, mihogo ipo siku zote mbona hatukushiba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo jamani Watanzania wenzangu, Wabunge wenzangu, niwaambie wazi watu wasiozidi kumi Zanzibar wanaifanya nchi hii iingie katika historia nyingine ya kuonekana nchi isiyo na demokrasia, wakati tunajidai ni nchi ya demokrasia. Kisiwa cha Zanzibar ambacho Mheshimiwa Ally Keissy alisema ukiwaita kwa filimbi wanakusanyika tunapatikana, wanainyima mamilioni ya Watanzania misaada katika nchi hii, siyo haki na tusijidai. Tumekuwa na matatizo, madeni yameongezeka, muda wote wakati ambapo tulikuwa tukipewa misaada, kuondoka kwa misaada hii ni tatizo, fikirieni tena.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge hili, napenda kuwaambia wananchi wangu wa Jimbo la Konde, kwa sababu kule kwetu Zanzibar hata kufanya mikutano hatufanyi, ile nchi imekaa ndivyo sivyo, kile kisiwa kimekaa ndivyo sivyo, utawala bora haujulikani. Kwa mfano, leo akitokea CCM mmoja katika Jimbo akienda ku-*report* tu wale wana-CUF wameniangalia kwa jicho baya, kijiji kizima wanapelekwa askari wanakwenda kukisomba wanakiweka ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, siropoki! Tarehe 17 siku tatu kabla ya uchaguzi, mwana CCM mmoja katika Jimbo langu, alizua kwamba amechomewa nyumba hakikuungua hata kibakuli kimoja, walikuja kuchukuliwa wazee wa kijiji 30 wakaswekwa ndani kwa sababu tu ya amri ya kisiasa ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Utawala bora gani mnaoujadili nyinyi hapa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba alitoa tangazo la kupiga marufuku wananchi wa Mkoa ule wasitembee usiku, ana mamlaka gani kisheria na Kikatiba kutangaza hali ya hatari katika Mkoa? Nchi hii ina Majemedari Wakuu wa Majeshi, Amiri Jeshi Wakuu wangapi? Hebu niambieni maajabu hayo kuna Amiri Jeshi wangapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema na ninawaambia wananchi wa Jimbo la Konde kwamba dini zote zinakataza mtu kushirikiana na dhalimu, dini zote zinakataza kabisa mtu kushirikiana na mtu aliye dhalimu kwa njia yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, nawaomba wananchi wangu kuanzia mimi mwenyewe wasishirikiane na madhalimu muda wote wa uhai wa maisha yao, wasishirikiane nao. Kama wanauza watii masharti ya leseni kwa sababu inataka lazima kuuza, lakini kununua ni hiyari yao na hakuna

atakaethubutu kuwaingilia, waendelee kufanya wanaloweza kuhakikisha madhalimu hawakamatani nao, hawashirikiani nao katika lolote na hilo nawaunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape mfano tu mimi mwenyewe nimeanza, Mwakilishi wa CCM haramu aliyechaguliwa tarehe 20 alinipigia simu nikamwambia ukome kama ulivyokoma kuzaliwa mara ya pili kwenye tumbo la mama yako, na nilimwambia asinisogelee na akinisogelea hamtaniona tena hapa Bungeni, tutamalizana huko huko, hamtaniona. Haiwezekani, unakaaje na watu wanaodhulumu haki za watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii imejijengea historia sasa ya kuifanya ile Zanzibar ni kichaka, leo ninyi mnatafuta watalii wakija wakiwinda vitalu na kupiga wanyama badala yake ninyi mnachukua Jeshi lenu mnalipeleka Zanzibar kuwalinda mama zetu na baba zetu, haki iko wapi? Wameleta magari yote ya Tanzania Bara kuja katika Kisiwa cha Pemba; mnawawinda nini, mnawatakia nini mama zetu, ndugu zetu, watoto wetu, tuna lipi baya, kukataa tu kuiunga mkono CCM ndiyo kosa letu? Kama hilo ndiyo kosa niwahakikishieni hata dunia iundwe mara ya pili CCM hatutaikubali na hatuitaki! *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Taarifa

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Msemaji kwamba kwa mujibu wa tathmini ya dunia ya haki za binadamu na utawala bora, Tanzania ina *rank A* ya utawala bora na haki za binadamu. Naomba msemaji alitambue hilo.*(Makofi)*

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa tutamsikia Mheshimiwa Ali Hassan King.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwa hai na kuwa salama tukahudhuria kikao hiki kujadili Mpango wa miaka Mitano wa Maendeleo wa Taifa. Pili, ninashukuru kupata nafasi hii ili na mimi kutoa maoni yangu kuishauri Serikali juu ya Mpango huu wa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongo usiokanushwa hugeuka kuwa ukweli. Maelezo ambayo yametolewa hapa kwamba hawatotambua, hawatofanya nini, hayo yanazungumzwa na wengi, lakini kutotambua Serikali wamefanya

kama watu ambao wamekula soro ya kizamani, maana soro ya kizamani inavyoliwa huwa yule mlaji hufunikwa kanga haonekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wanasema hawatambui lakini sasa kinachotoka Serikalini wanasema ni haki yao, sasa ni wajibu wa nani? Ikiwa wewe kwako haki ina maana kwamba ni wajibu wa mwingine, sasa hapo tayari umeshatambua Serikali ukitaka usitake. Kama wewe kweli hutambui kama Mungu yupo kwa nini unavuta hewa yake, imetengenezwa na nani? Wewe unasema hiki kitu hakipo kwa nini wewe unatumia na unasema hakipo, sasa hayo ni maneno tu ya mtu ambaye tuseme ni maneno ya mfa maji. *(Makofi)*

Kuna maneno hapa yanazungumzwa kwamba labda CCM wangetuachia sisi, sasa ninyi mnataka kushindanisha nazi na machicha katika kutoa tui? Hata mkimsimamisha 2020 na 2025 yale ni machicha, machicha ni machicha tu, yamebakia kuanikwa sasa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo langu ni kuchangia Mpango huu na nimelenga kuchangia katika suala la *financing strategy* ambayo imeelezwa kama ni mpango wa upatikanaji wa fedha katika kugharamia huu Mpango. Wazungumzaji wengi wameeleza katika kuchangia kuinua maendeleo ya nchi hii lazima tukope, hata nchi zingine nazo zinakopa katika kufanya mipango yao, Marekani wanakopa China, Japan wanakopa China na wote hawa wanakopa ili ku-*finance* mipango ambayo ipo wameiweka ili kuendeleza mataifa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia suala ya deni la Taifa ambalo limewahi kuzungumziwa na wachangiaji, kuna msemo mmoja wanasema mcheza ngoma isiyo yake daima ataharibu, hawi sawa na wenzake kutwa huwa kwenye taabu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika,una mtu anazungumza deni la Taifa kwamba kutokana na ile *percent* ambayo ameizungumza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ni asilimia 36.8 ya Pato la Taifa, anasema ni kubwa na halitofaa, wame-*comment* mengi. Lakini niwafahamishe tu vile ni vigezo vya Kimataifa siyo vigezo ambavyo labda vimezaliwa hapa Tanzania peke yake, ni vigezo vya Kimataifa na kila nchi inatumia vile vigezo, hilo ni jambo moja kwanza lifahamike.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili watu wafahamu kwamba Deni la Taifa kuwa himilivu vile ndiyo vigezo vyake, watu wafahamu kwamba Japan ni nchi ambayo inaongoza hata hapa Tanzania kwa kutupa misaada, lakini deni lake la Taifa kwa Pato la Taifa ni asilimia 246. Marekani asilimia 105 mwaka jana, mwaka huu asilimia 104, sisi ni asilimia 36.8. Kwa hiyo, ili kuweza kufanikisha malengo ambayo yapo katika mpango huu ni lazima tukope, wanaita *leverage*, ukitaka kubeba kitu kizito ni lazima uweke *lever*. Kwa hiyo, *lever* ni huu

mkopo ambao utatusaidia kubeba mzigo wa maendeleo ambao tumejipangia wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kitu kimoja katika kukopa. Tumepanga kukopa ndani pia tumepanga kukopa nje, ninatoa ushauri kwa Serikali katika kukopa ndani bora zaidi tukope nje kuliko kukopa ndani, kwa sababu tutakapo kopa ndani mwenendo wa riba unaweza ukaongezeka, tulichopanga kwamba tuna sekta binafsi tunazitarajia nazo zishamirishe ukuaji wa uchumi. Kwa hiyo, mwenendo wa riba ukiwa juu ambao utasababishwa na kukopa ndani utainua riba ikiwa Serikali inakopa ina maana kutakuwa *free risk*, ile *free risk* kila mmoja atapenda aikopeshe Serikali, hatopenda kukopesha watu binafsi, hapa riba zitapanda juu kwa maana hiyo watu binafsi ama sekta binafsi zinaweza zikaanguka, hivyo nashauri tukope nje zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tukope nje zaidi tujaribu kutizama mikopo nafuu, mikopo nafuu ipo lakini pia Serikali inaweza ikaingia katika *International Financial Market* ikakopa, hiyo ipo, lakini tunasahauri pia tena kuwa jambo hili kwamba ile *sovereign credit rating* ifanyiwe haraka ya Tanzania imalizike ili riba tutakayokopa kutoka nje iwe chini. Hili jambo tunaishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakapokopa mwaka huu, utakapofanya maendeleo kama umekopa ni muhimu kwetu kuonekana kile tulichokopea kimefanyika. Kikiwa kimefanyika lile deni litakuwa halina shida kulipwa kwa sababu tayari kilichokopewa kimefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika aina za *financing strategies* ambazo zimeelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, moja ni kufanya *FDI (Foreign Direct Investment)*. Katika hili watu wa nje kuja kuwekeza mitaji yao moja kwa moja tujaribu kuchambua, tuchambue mapema ili tusije tukaja tukapata hasara kama inayowakuta watu wengine. Kwa sababu kuweka moja kwa moja *Foreign Direct Investment* bila ya kuchungulia chungulia au kaungalia tunaweza tukaja tukajitwisha mzigo ambao baadaye unaweza ukaja ukatugharimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi *Foreign Direct Investment* zinafanyika lakini tuangalie mazingira yatakayotupa nafuu katika kufanyika kwake. Kwa mfano, hivi sasa tunaweza tukawaita watu kuja kufanya hiyo *Foreign Direct Investment* kwetu, lakini baadaye ikaja ikawa mzigo wakataka kuweka mishahara wanayotaka wao, wakaweka mazingira magumu ya kazi, wanaweza wakawa wanabeba faida wanaenda nazo kwao, lakini jambo baya zaidi wanaweza wakaja wakafanya *transfer pricing* waka-*quote* bei kubwa kwa kupeleka kule kwao halafu sisi tukaja tukaathirika zaidi. Kwa hiyo, hili tujaribu kuliangalia ili tuweze kufaidika na hii *Foreign Direct Investment* tuchuje, kwa sababu wanaweza wakaja kutokana na hamu kubwa tuliyonayo tukawapokea haraka bila ya kuwachuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa niongelee ni kuhusiana na viwanda ambavyo Tanzania tumelenga kuviweka. Nchi yetu ya Tanzania siyo kisiwa, tuna ushirikiano wa Kimataifa, tuna ushirikiano wa Kikanda na kuna makubaliano mengine ambayo yamefanyika ya Tanzania na nchi nyingine, kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokusudia kufanya viwanda hapa kwetu tujaribu kufanya *comparative advantage analysis, k*wamba ni jambo gani tunaweza sisi katika kuzalisha kwetu likatunufaisha zaidi kuliko kitu kingine, ni viwanda gani ambavyo ni vya kuweka hapa kwetu kuliko kuweka viwanda vya aina zote, tusije tukaja tukakurupuka. Kwa mfano, alizeti inazalishwa Tanzania, wafanyabiashara wa mafuta ya alizeti au wazalishaji wa mafuta hayo hapa Tanzania wanahitaji nafuu fulani. Tunaweza tukasema kwamba tuna-*block* pengine bidhaa za kutoka nje, lakini ku-*block* kwetu bidhaa za kutoka nje tuna ushirikiano wa Kikanda, tuna ushirikiano wa Kimataifa, tujaribu kupima ile *comparative advantage* yetu na wenginge, tuzalishe kitu gani zaidi hapa ndani ili tuweze kutunufaisha zaidi, tujaribu kutazama kitu ambacho *technology* yake tunaiweza. Tujaribu kutazama kitu ambacho rasilimali zake zinapatikana hapa kwetu, pia kuangalia masuala mengine kama vile *demand*, kitu ambacho pengine kinahitajika sana na mambo mengine ya sera za kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la viwanda linahitaji sera. Watu wa viwanda wanasema wanahitaji sera, kwa hiyo, tuwawekee sera ambayo itaweza kuwapelekea wafanyabiashara wetu wa hapa waweze kuzalisha, watakapoweza kuzalisha basi itakuwa ni nafuu kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu alizungumza kwamba uchaguzi uliofanyika Zanzibar ni uchaguzi haramu. Mimi napata taabu sana kwa kitabu kipi? Wamesema hakuna kitabu kilichozungumza CUF na CCM ama CHADEMA hakuna! Sasa ni kitabu kipi kilichotaja habari za uchagzi huu haramu na huu halali?

Mimi ninavyofahamu uchaguzi uhalali wake na uharamu wake ni kwa Katiba na Sheria. Tuliwafundisha hawa ndugu zetu hapa wakatulia, wakajua kwamba uchaguzi unakwenda kwa Katiba na Sheria, leo unakuja kusema uchaguzi ni haramu! Ni haramu kwa sababu ya kukosa kwako wewe! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yote umeyataka mwenyewe, iliyobaki shauri yako. Kwa sababu kama kuna kitu ambacho kimefanyika nje ya utawala bora ni mtu kuwazuia watu haki yao ya kwenda kupiga kura. Hili ndilo kubwa ambalo limefanyika. Sasa mtu aina kama hii atachukuliwa kama nani wakati jambo la vyama vya siasa ni jambo la Muungano, unazungumza wewe kama

kiongozi, unawazua watu wasiende kupiga kura, matokeo yake unawakataza na wenzako wasishiriki, unawakataza wasigombee, matokeo yake watu wanalia huko! Hili ndilo ambalo wenzetu liliwasibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mtaka nyingi nasaba hupata mwingi msiba. Sasa huu msiba waache tu waende nao waomboleze, kwa nasaba kubwa walioitaka waache wapate msiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuzungumzia suala moja ambalo ni muhimu, ulinzi na usalama ni kitu muhimu sana katika nchi yetu. Utakapokuwa unatega mabomu sasa unataka watu wasifuatiliwe? Mabomu yanalipuka nchi nzima usifuatiliwe, usiguswe, wewe ni nani? Mimi ninaomba iwe hivyo hivyo. Mheshimiwa Mawe Matatu nenda nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mnafiki, tena mnafiki sana nisipoanza kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais na Baraza lake la Mawaziri kwa kuendelea kuchapa kazi kwa bidii na kwa weledi mkubwa na wananchi wa Tanzania wana matumaini makubwa sana na Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimepitia Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa 'A' mpaka 'Z', pia nimesoma Hotuba ya Upinzani maoni yao juu ya Mpango huu, kitu cha kusikitisha hotuba ya Mheshimiwa David Silinde rafiki yangu, yeye kama Msemaji Mkuu wa Upinzani, Nasikitika sana hotuba yake imetumia takwimu za kupotosha Bunge lako Tukufu na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda ukurasa wa tatu wa hotuba ya Kambi ya Upinzani juu ya utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano, kwa kutolea mfano, kuna sentensi inasema takwimu za Wizara ya Fedha zinaonesha kuwa kwa kipindi cha miaka mitano fedha ambazo zimetolewa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni wastani wa asilimia 26 tu, hiyo tunazungumzia historia. Watanzania wanataka kujua tunapokwenda mbele tumejipanga vipi? Ukiangalia Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano ijayo tunatoka kwenye hii asilimia 26 kwenda asilimia 40 ya bajeti ya maendeleo imetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika hotuba hii, kwa mfano, Kambi ya Upinzani wanadai kwamba Mpango wa Maendeleo wa Kwanza na huu wa Pili umeasisiwa na Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani na wahisani. Hii siyo kweli, mpango huu uliletwa Februari, 2016 katika Mkutano wa Pili tukaujadili, maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge yameingizwa katika Mpango huu wa Pili ambao uliwasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa jana. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba mpango huu unaasisiwa na Mashirika ya Kimataifa, huo ni upotoshaji kwa Bunge lako Tukufu na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashangaa sana ndugu zetu wa Upinzani kule kuna wasomi wengi tu nawajua, lakini nashangaa katika hotuba yao kuna mapendekezo kwamba Mpango huu utengenezewe sheria. Mimi sijawahi kuona Mpango unatengenezewa sheria kwa sababu sheria iko *fixed* Mpango ni *dynamic*. Sasa ukitunga sheria kwa Mpango ambao uko *dynamic* ina maana kila mwaka tutakuwa tunatunga sheria ya kutekeleza Mpango, hiyo inawezekana kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitaalam Mpango unakuwa na *monitoring and evaluation framework,* kazi yetu kama Bunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali, baada ya kuupitisha huu Mpango wa miaka mitano kazi yetu ni kila mwaka tunaletewa taarifa ya utekelezaji, tunapitia na kuangalia kama utekelezaji wa kila mwaka unaendana na Mpango wa miaka mitano, lakini siyo kusema tutunge sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda ukurasa wa nne pia kuna upotoshaji mwingine wa takwimu. *Paragraph* ya mwisho inasema Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulithibitishia Bunge hili na wananchi kwa ujumla kama shilingi 4,970.04 kwa siku zinatosha kuhudumia familia nzima. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri haijasema familia nzima, imesema *income per capita,* wastani wa pato la mwananchi, sasa humu wanatuletea taarifa za eti pato la familia, mmeitoa wapi hii? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa tano, deni la Taifa ukiangalia takwimu toka *National Bureau of Statistics* na Wizara ya Fedha, Deni la Taifa sasa hivi liko 20.9% na *maximum debt sustainability threshold* ni asilimia 50 ya *GDP*. Kwa hiyo, tukisema kwamba Deni la Taifa siyo stahimilivu hizo takwimu tunazitoa wapi na wakati nchi yetu ina takwimu ambazo tunazitumia hizi hapa? *(Makofi)*

Pia ukiangalia katika *debt sustainability threshold* pia kuna kuangalia asilimia ya deni *as percentage* ya *total export*. Takwimu zinaonesha ni asilimia 104.4 na ukomo ni asilimia 200, sasa hii hatari inatoka wapi Waheshimiwa Wabunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda ukurasa wa nane, kushuka kwa thamani ya shilingi. Mimi nashangaa hapa kuna hoja kwamba kushuka kwa thamani ya shilingi kutaathiri utekelezaji wa maendeleo, sijui ni *logic* ya wapi.

Ninavyofahamu kama nchi ikikopa kwa ajili ya miradi ya maendeleo tunakopa kwenye dola. Dola ikija hapa nchini inaweka *pressure* kwenye shilingi, kwa hiyo, shilingi inapanda *against* dola, sasa ukisema kwamba kushuka kwa shilingi kutaathiri maendeleo pia sioni *logic*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotegemea katika hotuba hii ya Kambi ya Upinzani ni kuuleta mpango mbadala kwamba Mpango wa Miaka Mitano mliouleta siyo mzuri, mzuri ni huu hapa ndiyo tuuangalie lakini siyo kuleta taarifa ambazo zinapotosha umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia kuhusu upotoshaji wa takwimu, hii inanikumbusha wakati niko chuo, Profesa wetu wa *Statistics*...

KUHUSU UTARATIBU

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bashungwa naomba ukae.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kanuni ya 68(8) naomba kumpa taarifa Mheshimiwa aliyezungumza kwamba…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa huo ni Utaratibu au ni Taarifa unataka kumpa?

MBUNGE FULANI: Mhesimiwa Naibu Spika, taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8).

NAIBU SPIKA: Sasa uliomba utaratibu, haya mpe hiyo Taarifa.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ndiye anayepotosha! Amesema sheria huwa ni *static,* ni *fixed,* siyo kweli ndiyo maana kunakuwa na *review* za mara kwa mara. Kwa hiyo, sheria nayo ni *dynamic*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kumpa taarifa kwamba yeye siyo Waziri wala Naibu Waziri, muda wa Serikali wa kujibu bado, arudi kwenye utaratibu achangie hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bashungwa Taarifa hiyo unaikubali?

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa siikubali kwa sababu tukisema kila mwaka tuwe tunaletewa sheria ambazo tunazipitia kwanza ni utumiaji mbaya wa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maslahi ya muda sasa naomba niende kwenye ushauri juu ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Karagwe ni sehemu ya nchi na pia linastahili kuwekwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Karagwe tuna tatizo kubwa la maji na Mheshimiwa Rais Mstaafu, Jakaya kikwete aliahidi mradi wa Lwakajunju, naishukuru Serikali ya Awamu ya Tano imeniahidi kwamba katika kipindi cha miaka mitano itahakikisha mradi huu unatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa jiografia ya Karagwe tuna miji mikubwa mitano ya Afrika Mashariki inayotuzunguka, ninaiomba Serikali katika Mpango wa Miaka Mitano watujengee barabara ya kuanzia Nyakasimbi kwenda Nyakakika, Nyabionza, Kibondo, Kiruruma mpaka Rwabwele, kwa sababu barabara hii itafungua fursa za kiuchumi kwa wananchi wa Karagwe na Kyerwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Mpango wa Miaka Mitano napenda kuiomba Serikali iweke mpango wa kujenga hospitali ya Wilaya kwa sababu sasa hivi tunagemea hospitali ya kanisa la *ELCT* ya Nyakahanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia pia kuhusu umuhimu wa kujenga reli ya Kati ambayo itatuunganisha na nchi za jirani ili tuweze kutumia bandari zetu na reli yetu kupata mapato kupitia *customs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni la muhimu sana na ninawaunga mkono Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuchangia katika kusisitiza umuhimu wa kujenga reli ya Kati na reli ambayo itatuunganisha na nchi za jirani ili iweze kutusaidia katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, ili Serikali isiendelee kukopa sana ninaishauri Serikali iangalie mikakati ya kupata wawekezaji kupitia *PPP framework* na pia kuangalia ni namna gani tunaweza tukakopa kwenye *International Capital Markets* badala ya kuweka *pressure* ya kukopa ndani na kukopa kwenye soko la nje ambalo riba zake ni za gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera hatuna Chuo cha *VETA* napenda kuiomba Serikali katika huu Mpango wa Miaka Mitano pia waweke mpango wa kujenga chuo cha *VETA* katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia asilimia kubwa ya Watanzania wako kwenye *bottom of pyramid*, inabidi mpango wa Serikali wa viwanda uangalie zile sekta ambazo zinaajiri Watanzania wengi kama sekta ya kilimo. Tuwekeze kwenye kujenga *value chain* katika sekta ya kilimo ili iweze kutengeneza ajira kwa vijana na kukuza uchumi wa nchi.

Pia inatubidi kuwa na *SME developments plan* sijaona mkakati wake, kwa sababu ukiangalia kampuni za *size* ya kati tukiweza kuzisaidia zitaajiri watu wengi na itatusaidia kutatua tatizo la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna haja ya kuunda *SACCOS* za vijana kwa sababu *SACCOS* hizi zikiwekewa mitaji zitasaidia kuwakopesha vijana ili waweze kujiajiri na kwa kufanya hivyo tutatatua tatizo la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bashungwa.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa Rais Dkt. John Magufuli pamoja na timu yake ya Mawaziri kwa kuleta matumaini ya Watanzania:-

Utumbuaji Majipu; Kuondoa wafanyakazi hewa; Kuondoa wafanyakazi wazembe; Kuondokana na uchumi tegemezi; Kuondokana na mikopo; na Kuweka mazingira ya kuongeza *FDI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Mpango wa Pili wa Maendeleo. Natoa pongezi kwa Rais Dkt. John Magufuli kwa:-

Utumbuaji majipu; Kuondokana na uchumi tegemezi, *FDI vs* Misaada; Uchumi wa viwanda; Kuboresha elimu; na Kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika huduma za Fedha:-

Mitaji ya benki za *TIB* na *TADB* 212 bilioni na 60 bilioni; Jinsi ya kunufaisha wakulima na wajasiriamali wadogo; Riba haziko rafiki na wakopeshe wadogo (Wajasiriamali na Wakulima); Matumizi ya *Mobile Money* – M Pesa; *Payment system* inahama kutoka ma-*bank* kwenda kwenye mitandao ya simu; usimamizi/ulinzi/*protection;* na *TR* na usimamizi wa mashirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kilimo (3.4%):-

Napongeza Mpango wa Serikali wa kutoa milioni 50 kwa kila Kijiji/Mtaa; Elimu ya kilimo na ujasiriamali; Mapinduzi katika kilimo; Kuongeza thamani ya mazao ya kilimo; Msisitizo wa viwanda vidogovidogo vijijini; na Msisitizo uwe kuongeza na kuboresha uzalishaji wa kilimo; *US$ against TZS* – itakuwa imara tukiongeza uzalishaji na kupunguza *imports.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Barabara/Reli/Miundombinu Vijijini:-

Barabara za Vijijini ziboreshwe kusaidia usafirishaji wa mazao; Kuboresha Reli ya *TAZARA;* Barabara za kupunguza msongamano; Barabara ya Tanzania – Zambia kupita katikati ya miji yetu mikubwa kama Jiji la Mbeya, hatari ya ajali/msongamano; Barabara za kuunganisha mikoa; Isyonje (Mbeya**)** Kikondo – Kitulo - Makete – Njomb; na Mbalizi – Galula, Mbalizi – Ilembo – Ileje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji:-

Changamoto za maji vijijini; Maji/afya ya wananchi na gharama ya tiba; na Miradi ya maji Kata ya Mjele, Mji Mdogo wa Mbalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika elimu, mitaala ya elimu iendane na mipango yetu; ujasiriamali wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nishati na Madini:-

Vyanzo vya umeme; jua, maji, upepo na gesi; Madini ya Songwe; na Umiliki wa wananchi

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia Mpango huu kwa kuunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kwa Mpango huu uliowasilishwa Bungeni kuhakikisha unaendana na hali halisi ya ukusanyaji kodi na udhibiti wa mapato hayo. Mpango huu ujikite kuwezesha Mashirika ya Umma kama *STAMICO, TPDC, TANAPA, TAZARA, ATC, TRL* na kadhalika yajiendeshe kibiashara ili kuchangia katika bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huu unapozungumzia miundombinu napenda kuona ni namna gani Serikali:-

(i) Itaboresha *TAZARA*.

(ii) Barabara ya kutoka Ifakara-Mlimba hadi Madeke Njombe ionekane kwenye bajeti hii ili wananchi ambao asilimia 90 ni wakulima na ni eneo linatoa mazao mengi kama mpunga, ufuta, ndizi, *cocoa*, miti, ng'ombe na kadhalika. Jimbo hilo ni jipya ndani ya Wilaya ya Kilombero ambapo barabara hiyo ikijengwa itaunganishwa na Mkoa wa Njombe.

(iii) Jimbo la Mlimba halina barabara, halina Kituo cha Polisi, halina hospitali ya uhakika, halina Mahakama isipokuwa moja ndani ya Kata 16. Halina maji safi na salama ingawa lina mito mingi mikubwa ukiwemo na Mto Mpanga. Hali ya shule za msingi, awali ni tete sana, hakuna Chuo cha Ufundi wala Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi Mpango huu na bajeti hii ione namna bora ya kuingiza hela kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishashauri Bunge lililopita na naendelea kushauri namna bora ya kuhamasisha Watanzania kusaidia Serikali kukusanya kodi. Ni hivi, Dar es Salaam uwe mkoa wa majaribio ili ukifanikiwa uende nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila anayenunua bidhaa ahakikishe anapewa risiti ya *TRA (electronic receipt)* ambapo ataitunza na Serikali itaweka kiwango maalum cha fedha alizotumia na mwishoni mwa mwaka mtunza risiti huyo atarejeshewa kiasi fulani cha fedha alizotumia kama motisha. Ni muhimu Serikali ikajifunza toka nchi za wenzetu mbinu za ukusanyaji kodi. Haitoshi kusema tu, Watanzania daini risiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliwezeshe Shirika la Umma *STAMICO* kwa kuwapa maeneo mapya ya kuchimba madini ya dhahabu na kadhalika ili ichangie pato la Taifa. Isiwe kama ilivyo sasa Shirika hilo la *STAMICO* linarithi migodi iliyoachwa na wawekezaji na kushindwa kuzalisha madini matokeo yake linapoteza pesa. Mfano, Mgodi wa *tanzanite*, Kiwira, Tulawaka na kadhalika, hata ukiangalia ni kiasi gani cha fedha zinazochangia kwenye bajeti ni sifuri, sana sana Serikali inazidi kulipa watumishi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Mpango huu umedhamiria kuboresha miundombinu ya barabara hivyo katika maboresho hayo kuwepo na msisitizo wa kujenga Barabara ya Ifakara-Mlimba-Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha , Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa ili tuweze kuujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo naomba Serikali iweze kunipatia ufafanuzi wake:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza viwanda; ni imani yangu kuwa kama viwanda vitaimarishwa nchini, Serikali itaongeza pato la Taifa na tutaongeza ajira kwa vijana wetu nchini.

Ningeomba kujua, nchi yetu ilikuwa na viwanda vingi sana, ambavyo vingi vyao vilibinafisishwa na wawekezaji wengine wamebadilisha matumizi ya viwanda hivyo. Je, nini mpango wa Serikali kwa viwanda hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tulikuwa na kiwanda cha kuchonga almas cha *Tancut* Iringa, ambacho kilikuwa kinatumia malighafi za ndani, lakini leo hii almas yetu inapelekwa nje kuchongwa. Tungependa Serikali iweke Mpango wa wazi unaoeleza jinsi ya kuanzisha viwanda vitakavyotumia kununua bidhaa za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, miundombinu ya barabara; ningependa kujua Serikali imejipangaje kuhakikisha barabara zote za kiuchumi zinapitika wakati wote ili kuweza kuchukua mazao na malighafi kama Mgololo kilichopo Iringa, hiyo ingejengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Iringa ni kati ya Mikoa ya kiuchumi. Kwa mfano, tunalima mahindi kwa wingi, vitunguu, nyanya, chai na tuna msitu mkubwa sana wa miti, lakini barabara zake zote zinazokwenda kwenye maeneo hayo zina hali mbaya sana! Ningependa jambo hili, Serikali itoe kipaumbele. Pia zipo barabara kama ile inayokwenda kwenye Mbuga ya Wanyama ya Ruaha *National Park* iwekewe lami ili tupate Watalii wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, umeme; Viwanda vitakapoanzishwa vitahitaji umeme wa uhakika, umeme usio katikakatika kama tulionao hivi sasa na kuwepo umeme, mijini na vijijini ambao ni wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kilimo; kwa kuwa nchi yetu, wananchi wake asilimia kubwa sana wanategemea kilimo na tunategemea Serikali yetu iweke mpango mahususi kwa ajili ya kusaidia wakulima. Wakulima wapatiwe elimu ili walime kilimo cha kisasa na chenye tija na kitakachoweza kusaidia malighafi katika viwanda vyetu pamoja na kupatiwa mikopo katika Benki yetu ya Kilimo. Je, ni kwa nini Serikali isifungue Benki ya Kilimo katika Mkoa wa

Dodoma ili Benki hii iweze kufikiwa na mikoa yote kuliko ilivyo sasa, Benki hii ipo Dar es Salaam tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, uimarishaji wa miradi ya vyanzo vya mapato; Serikali iwe na mpango madhubuti wa kumalizia miradi ambayo imechukua muda mrefu sana, ambayo inaweza kuongeza pato la Taifa kwa sababu tumekuwa tukianzisha miradi mipya wakati miradi ya zamani inasuasua!

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, ujenzi wa reli na viwanja vya ndege; bila Serikali kutoa kipaumbele katika ujenzi wa reli bado tutaendelea kusuasua sana katika ukuzaji wa pato letu la Taifa. Reli itaponya hata barabara zetu nchini na kupunguza hata bei ya bidhaa. Pia Serikali ieleze wazi mpango hata kuhakikisha viwanja vyetu vya ndege vinajengwa ili viweze kusaidia kukuza pato la Taifa.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri wa Fedha pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano, 2016/2017-2020/2011. Naunga mkono hoja kwa sababu Mpango huu wanaonesha kusaidia kupunguza umaskini kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri kwa Serikali kufanya utafiti kwa viwanda ambavyo havifanyi kazi ili kuangalia uwezekano wa kufufua, lakini kwa gharama ndogo, pia kuweka mfumo ambao utawezesha viwanda hivyo kuzalisha kwa faida. Viwanda vizalishe bidhaa ambayo inatakiwa kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ili kuhakikisha uzalishaji wa bidhaa za viwanda unakamilika lazima viwanda vitumie gesi kwa bei nafuu ili kupunguza gharama za uzalishaji. Pia kusimamia bei ya mafuta; petroli, diseli na mafuta mengine ya kuendeshea mitambo katika viwanda. Bei ya mafuta ikiwa ndogo au ya chini itasaidia kuendesha viwanda kwa gharama ndogo na kupata faida kubwa ya uzalishaji wa bidhaa. Kuboresha huduma za jamii kama vile, kuboresha miundombinu ya barabara, umeme, maji na Vituo vya Afya itasaidia sana kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mufindi Kusini ni Jimbo pekee katika nchi yetu lenye viwanda vikubwa na vidogo. Tatizo kubwa tunaomba barabara ya Nyololo - Mtwango hadi Mgololo ambayo imepita katika Viwanda vya Chai, Mbao na Kiwanda cha Karatasi, Mgololo. Barabara hii ni muhimu sana kwa kukuza uchumi wa nchi, naomba ijengwe kwa kiwango cha lami. Serikali ilishafanya upembuzi yakinifu na Mheshimiwa Rais wa Tanzania aliahidi kujenga kiwango cha lami. Pia iko kwenye Ilani ya Chama cha mapinduzi kuwa barabara ya Nyololo – Mtwango kilomita 40, Madinga – Mgololo Kilomita 82 zitajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba ahadi zote za Mheshimiwa Rais ziingizwe kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/2017 - 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PROSPER J. MBENA: Mheshimiwa Naibu Spika,, naunga mkono hoja. Kujenga msingi wa uchumi wa viwanda utawezesha nchi kukuza uchumi wake haraka na kutoa ajira nyingi kwa vijana wetu. Muhimu hapa ni kuangalia aina gani ya viwanda tunavyovihitaji, masoko yapi ya nje na ndani tunayalenga na lazima viwanda hivi visambazwe kwenye mikoa na wilaya mbalimbali kuwepo na uwiano tusifanye makosa ya upendeleo katika kusambaza viwanda. Fursa iwe sawa kwa wote, sasa tofauti iwepo tu kwenye upatikanaji wa malighafi husika kwa mahitaji ya viwanda, hapo uwekezaji utaangalia eneo lipi lina *comparative advantage* na hivyo kusukuma maamuzi ya wapi kiwanda kijengwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ili kujenga viwanda hivi, tunahitaji miundombinu ijengwe pale ambapo haipo na pale ambapo ipo, miundombinu hii iimarishwe. Miundombinu ya barabara, umeme, maji, simu na mawasiliano mengine ya usafirishaji. Jimbo la Morogoro Kusini lina *comparative advantage* kwa ujenzi wa viwanda vikubwa na vidogo vidogo vitakavyotumia malighafi zinazopatikana hapo hapo Jimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Morogoro Kusini kuna maeneo makubwa ya kilimo cha mazao mbalimbali ya chakula na biashara kama vile mpunga, mahindi, ufuta, alizeti, karanga, pamba na mazao mengine, matunda aina zote nanasi, maembe, papaya, machungwa, *avocado* na kadhalika, viwanda vya kusindika vyakula vinaweza kujengwa humo Jimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo pia lina mchango mkubwa wa kutoa kwa faida ya nchi kwenye eneo la madini, misitu, lakini barabara kutoka Bigwa hadi Kisaki kwa kiwango cha lami, ndio itakuwa mkombozi. Mradi huo wa kupanua barabara hiyo ya Bigwa – Kisaki na kuwekwa lami ni muhimu kutekelezwa na ni jukumu la Serikali kutoa fedha za kutekeleza miradi hii muhimu, sio suala la kukabidhi wahisani, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni fursa za nchi yetu kufanya biashara nje ya nchi. Mpango wa *AGOA* ambao Serikali ya Marekani imekubali kuongezea muda zaidi wa miaka 15? Sasa lazima nchi yetu inufaike na mpango huu. Utekelezaji wa miaka 10 iliyopita ya *AGOA*, haukuwa mzuri. Nchi yetu haikunufaika sana na *AGOA*. Sasa Serikali isimamie vizuri zaidi tuweze kunufaisha nchi angalau kwa asilimia 90 ya *AGOA*.

Mwisho, kuwepo na mpango maalum kwenye Mpango wa Serikali utakaowasaidia wananchi wetu wanaopatwa na majanga ya mafuriko ya mvua hususan vjijini. Msaada wa chakula, madawa unapaswa kupelekwa kwa waathirika haraka sana. Maeneo hatarishi kwa wananchi kuishi ni vizuri yasiruhusiwe wananchi kuishi humo, lakini liwe jukumu la Serikali kuwagharamia wananchi hao kuhamishiwa maeneo salama. Kata ya Selembala yenye vijiji vya (i) Magogoni (ii) Kiganila (iii) Bwira juu (iv) Bwira Chini (v) Kiburumo, katika Jimbo la Morogoro Kusini sasa ni Kata hatari ya mafuriko ya mvua kila mwaka na ni hatarishi kwa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuriko makubwa yaliyotokea tarehe 6 Aprili, 2016 na 16 Aprili, 2016 ni ushahidi tosha, vijiji vyote vitano sio salama tena. Serikali ilipe fidia na kuwaondoa wananchi wote wa vijiji vitano vya Kata ya Selembala (na siyo vijiji vitatu vilivyochaguliwa) ili wote wahamie eneo salama ili Kata yote ya Selembala sasa itumike kwa mradi wa bwawa la maji Kidunda. Napendekeza hata zao la miwa sasa lingeweza kupandwa eneo lote hilo kwa ajili ya viwanda vya miwa katika Jimbo la Morogoro Kusini. Mpango wa Maendeleo lazima uangalie usalama na ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia Mpango huu wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017-2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa suala la Benki ya Wanawake Tanzania *(TWB)*. Benki hii ilipoanzishwa mwaka 2009 lengo kuu ilikuwa kuwakomboa wanawake kiuchumi kupitia mikopo nafuu, kinyume na matarajio ya wanawake wote nchini, benki hii imekuwa ikitoa mikopo kwa riba kubwa sana, ya asilima kumi na tisa, riba hii imewafanya wanawake kushindwa kufanya biashara zao vizuri, kwa kuwa wanafanya biashara kwa kuhudumia mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeupitia vema Mpango huu wa Miaka Mitano, sijaona mwanamke akipewa kipaumbele, ukizingatia mwanamke hata katika jamii amekuwa mtu wa mwisho kuthaminiwa katika kipaumbele. Hivyo basi, naishauri Serikali, imwangalie mwanamke kwa jicho la tatu, hasa katika Mpango huu wa Maendeleo ya Taifa, ili kumwezesha kukabiliana na changamoto anazokutana nazo kama mwanamke katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali katika kipaumbele cha fedha katika Mpango huu, basi iongeze mtaji katika Benki ya Wanawake Tanzania *(TWB)*, kwa kiwango cha shilingi bilioni thelathini, ili ifanye jumla ya mtaji wa

benki hiyo, kuwa bilioni hamsini, kwani kwa sasa benki hiyo ina mtaji wa karibu bilioni ishirini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika Mpango huu, katika suala la afya, Serikali imeweka mkakati wa kujenga *blood bank* mikoani. Mkoa wa Mwanza unayo *blood bank* katika hospitali teule ya Bugando, lakini wanawake wengi hupoteza maisha wakati wa kujifungua kwa kupungukiwa na damu. Hivyo basi, naishauri Serikali badala ya kujenga *blood banks* bora inunue majokofu ya kutunzia damu, katika kila Kata na kila Wilaya. Ili kusudi kila kituo cha afya na hospitali ya wilaya, iweze kujitunzia damu, kwa kuwa watu wengi Watanzania hupenda kujitolea damu. Hii itasaidia kupunguza vifo vya akinamama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naishauri Serikali katika Mpango huu wa Maendelo ya Taifa, kwa kushirikiana na Wizara ya afya itenge fedha za kununulia *CT scan* katika kila hospitali ya Mkoa, ikiwemo hospitali ya Mkoa wa Mwanza ya Sekou Toure kwani wananchi hufa kwa magonjwa mbalimbali, ambayo kama kipimo cha *CT scan* kingekuwepo, mgonjwa angeweza kubainika ugonjwa unaomsumbua ili apatiwe matibabu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja baada ya kuwasilisha ushauri wangu kwa njia hii ya maandishi.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Natambua umuhimu wa Mpango kwamba, ndiyo dira ya maendeleo ya nchi kwa maana ya kujua tunatoka wapi, tuko wapi na tunataka kwenda wapi, tunakwendaje na kwa sababu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri kwa Mpango huu. Naomba nichangie kwa kuzingatia kwamba mimi ni Mbunge wa Jimbo la Chilonwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, miundombinu; barabara zinazounganisha Wilaya, (maeneo mbalimbali na Makao Makuu ya Wilaya), ni mbaya sana na hazipitiki vizuri. Hii inafanya uchumi wa Wilaya inayotegemea sana ushuru wa mazao inakuwa mbaya sana. Kwa kuwa wanunuzi wengi wanafika kwa tabu na hivyo wananunua mazao kwa bei ya chini sana jambo linalodidimiza pia uchumi wa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuangalia kwa makini na kuzisaidia Halmashauri na hasa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kwa kujenga madaraja muhimu *strategic* kama haya yafuatayo:-

(a) Daraja linalounganisha Kijiji cha Msanga na Kijiji cha Kawawa.

(b) Daraja linalounganisha Kijiji cha Chilonwa na Kijiji cha Nzali.

(c) Daraja linalounganisha Kijiji cha Dabalo na Kijiji cha Igamba (Dabalo B)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, viwanda; Wilaya ya Chamwino na Jimbo la Chilonwa kwa jumla hakuna kiwanda chochote. Tunahitaji *Agro-Based Industry/Factory* na hasa cha ku-*process* zabibu. Jambo hili litainua uchumi wa mtu mmoja mmoja, lakini pia kukuza uchumi wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na kuunga mkono mpango mzima na kuomba hayo niliyoyaainisha hapo juu yafanyiwe kazi.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani kwa kuingiza katika mpango

(a) Ukarabati wa meli ya *MV*. Butiama; na

(b) Ujenzi wa barabara ya Bunda-Kisovya-Nansio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naomba yafuatayo yawekwe katika Mpango:-

Kwanza, Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi katika Kisiwa cha Ukerewe; jambo litakalowasaidia vijana kupata msingi wa kujiajiri na kupunguza utegemezi wao katika Ziwa Victoria kwenye shughuli za uvuvi na kwa sababu hawana uwezeshwaji, wanajiingiza katika uvuvi haramu.

Pili, ujenzi wa Daraja la kuunganisha Kisorya (Jimbo la Mwibara) na Lugezi (Wilaya ya Ukerewe) ni muhimu kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano ya kijamii na kiuchumi na hivyo kuimarisha hali ya maisha ya wananchi wa Kisiwa cha Ukerewe. Hivyo Daraja hilo nashauri liwekwe katika Mpango.

Tatu, utafiti wa udongo katika Kisiwa cha Ukerewe na maeneo mengine ambayo udongo umechoka, itasaidia kupunguza upungufu wa chakula kwani utafiti utasaidia kujua aina ya mazao tutakayopaswa kulima kulingana na aina ya udongo kulingana na utafiti.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yangu kwenye Mpango huu yatajikita katika Wizara zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo; ukizingatia mafanikio kidogo kwa ufanisi wa Mpango wa awali kwa maoni yangu tatizo kubwa linaloikabili mipango yetu mingi ni ukosefu wa uadilifu kwa watekelezaji wa mipango yetu. Ikiwa ni pamoja na nchi kukumbwa na tatizo kubwa la rushwa, ukosefu wa miundombinu bora ya reli na barabara kwa maeneo ya uzalishaji mazao ya kilimo. Hatuwezi kuwa

na uchumi mzuri mpaka pale tutakapobadilisha mtazamo wetu na kuacha tabia ya uchumi wetu kutumikia siasa, badala ya siasa kutumikia uchumi. Katika kilimo tuna tatizo la masoko ya wakulima wetu, sambamba na ujenzi wa viwanda vidogo vidogo hasa pale ambapo mazao hayo hulimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu; miongoni mwa sababu za mipango mingi kutofikia malengo ni mfumo mzima wa elimu yetu, elimu inayotoa wahitimu wasiokuwa na uwezo wa kuingia kwenye soko la ajira ya kujitegemea. Elimu ambayo haiwajengei uwezo wa kujitegemea na badala yake wanakuwa mzigo kwa Serikali; vyuo vya *VETA* pekee ndio ufumbuzi wa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maliasili; hatuwezi kukuza sekta ya utalii kama hatupo tayari kufufua vivutio vilivyosahauliwa kama kivutio kilichopo Liwale (Gofu la Mjerumani la vita ya maji maji lililopo Mjini Liwale) hivi ni kweli ili kuingia Selou ni lazima watalii wapitie Morogoro kwa nini Mkoa wa Lindi (Liwale) imeachwa yatima katika utalii wa ndani na nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawezaje kuwashirikisha wananchi kushiriki kulinda rasilimali zetu kama hawataona faida ya moja kwa moja itokanayo ya rasilimali zetu. Utatuzi wa migogoro ya mipaka ya hifadhi zetu ni moja ya kikwazo cha sekta hii kushindwa kufikia malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu; ugawaji usiozingatia hali halisi wa miradi ya barabara nchini ni moja ya kikwazo katika Mpango huu. Mfano ni Mkoa wa Lindi ambao mpaka leo mkoa huu haujaweza kuunganishwa na Mkoa jirani wa Morogoro kupitia Liwale na Mkoa wa Ruvuma kupitia Wilaya za Tunduru na Liwale. Sio hivyo tu hata barabara ya Nangurukuru-Liwale ambayo ingeendeleza mazao ya korosho na ufuta ambayo sasa yanalimwa kwa wingi katika Mkoa mzima wa Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Afya ni sekta muhimu sana ambayo tumeshindwa hata kuboresha afya za watu wetu hasa katika kupunguza vifo vya mama na mtoto. Mfano, katika Wilaya ya Liwale hakuna hadi leo hospitali yenye hadhi ya kuwa hospitali ya Wilaya. Hospitali haina miundombinu yoyote inayofanana na hospitali ya Wilaya. Wilaya nzima ina kituo kimoja tu cha afya Wilaya yenye Kata 20 na Mpango huu haujasema chochote kuhusu ni namna gani ya kupambana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa wadau ni muhimu ili mipango yetu iweze kutekelezeka, vile vile uadilifu wa watendaji. Tuongeze bidii ya kupambana na rushwa na uwajibikaji wa pamoja.

MHE. MARTIN M. MSUHA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, kwa maandalizi mazuri ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa letu, kwa kipindi tajwa hapo juu. Mpango huu ni muhimu sana kwani ndiyo dira ya mwelekeo wa Taifa kwa miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu, naomba sasa nichukue nafasi hii kuchangia kisekta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Kilimo; naipongeza Serikali kwa juhudi ambazo imezifanya hadi saa katika kuboresha kilimo nchini. Hata hivyo, katika Mpango huu wa Maendeleo siajona mkakati wa kuendelea kuyaboresha mazao makuu ya biashara kwa maana ya zao la kahawa, tumbaku, korosho na pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa kahawa hususani wanazo kero nyingi sana ambazo zinawakatisha tamaa katika kuliendeleza zao hilo. Kero hizo ni pamoja na:-

(i) Bei kubwa ya pembejeo na utaratibu usiofaa wa kugawa mbolea kwa mtindo wa vocha ambazo zinakwenda kwa *package* ya mbegu, mbolea ya kupandia na kukuzia. Mkulima wa kawaha hahitaji mbegu wala mbolea ya kupandia. Vocha zinazotolewa hazitoshelezi badala yake imekuwa ni lawama kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kuwa, Serikali ifuate mfumo wa kupeleka mbolea kwa mtindo wa vocha na itengeneze mfumo mwingine na kwamba mbolea hizo zipelekwe mapema kabla ya msimu.

(ii) Mfumo wa soko la kahawa hususani Mbinga ni mbovu sana. Walanguzi wa soko huria hudiriki hata kununua kahawa kwa wakulima ikiwa shambani kabla haijakomaa na kuvunwa. Wanaingia mikataba ya kuwaumiza sana wakulima. Endapo mavuno ya msimu huo hayatoshi kulipa deni basi walanguzi hao hunyang'anya mashamba ya wakulima.

(iii) Kutokana na kuwa na soko huria wakulima wamekuwa wakilipwa bei tofauti tofauti ndani ya wilaya moja. Hii inakatisha tamaa sana kiasi kwamba wakulima wameanza kususia utunzaji wa mashamba hayo ya kahawa na ndiyo maana zao hilo limeporomoka kwenye orodha ya mazao makuu ya biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni kuwa Serikali ichukue hatua za makusudi kupiga marufuku ununuzi wa kahawa mbichi ikiwa shambani. Mfumo huu kule Mbinga unajulikana kama "*MAGOMA*". Lakini pia serikali

ichukue hatua za makusudi kuimarisha Chama Kikuu cha Ushirika cha Mbinga kiitwacho *MBIFACU* na kuhakikisha mali ya chama kikuu cha zamani zinarejeshwa kwa chama hiki kipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Elimu; wananchi wa Wilaya ya Mbinga kwa ujumla wake wanaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa Sera ya Elimu Bure. Hata hivyo, kuna changamoto zifuatazo ambazo zinahitaji utatuzi wa haraka sana:-

(i) Utatuzi wa uhaba wa Walimu. Zipo shule zenye wanafunzi zaidi ya 300 darasa la I hadi IV na kuna Mwalimu mmoja tu.

(ii) Vyumba vya madarasa havitoshi kabisa. Zipo shule ambazo wanafuzi wanasoma zaidi ya darasa moja kwa chumba kimoja cha darasa kwa wakati mmoja kwa kugeuziana migongo.

(iii) Suala la vyoo vya kisasa ni tatizo kubwa sana katika shule zetu za msingi.

(iv) Nyumba za Walimu nazo ziangaliwe. Watumishi hao wanaishi katika mazingira magumu sana tena sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nishati na Madini. Tunashukuru Serikali kwa kutekeleza Mradi wa Umeme Vijijini kupitia mpango wake wa *REA*. Hata hivyo, bado kuna vijiji vingi sana katika Wilaya ya Mbinga havikupata umeme kwenye *REA II*. Naomba Serikali sasa ipeleke umeme kwenye vijiji vilivyobaki ambavyo ni zaidi ya 150 kwenye mpango wa mwaka ujao.

Kwenye maeneo yanayotarajiwa kuzalisha umeme sijaona machimbo ya makaa ya mawe katika Kijiji cha Ntunduwalo, Kata ya Ruanda, Wilayani Mbinga yakitajwa kwenye mipango yote miwili wa mwaka mmoja wala ya miaka mitano. Eneo hili yupo mwekezaji anayechimba makaa ya mawe, naiomba Serikali imwangalie mwekezaji huyu na machimbo haya kwa namna ya pekee ili wananchi weweze kunufaika na uwekezaji wake. Kwa ujumla mwekezaji huyu na machimbo haya kwa namna ya pekee ili wananchi waweze kunufaika na uwekezaji wake. Kwa ujumla mwekezaji huyu hana mwelekeo wa kuzalisha umeme hivi karibuni. Mgodi huu uangalie upya kwani pia umekuwa kero kwa wananchi wa kata hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya ujumla; kwa kuwa kwa miaka kadhaa ya nyuma Serikali haikuwa na uwezo wa kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, wakati sasa umefika, ningeishauri Serikali iangalie upya namna ya upangaji wa vipaumbele vya Kitaifa.

Vipaumbele hivyo vingepangwa kisekta badala ya kimiradi kama inavyofanyika kwa sasa. Mfano, miaka mitatu ya kwanza fedha zote za maendeleo zingepelekwa Elimu; miaka mitatu inayofuata fedha zote za maendeleo zipelekwe kwenye Afya na kadhalika. Uwekezaji katika miradi ungeweza kuonekana kwa macho na kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Serikali imekuwa ikija na Mipango mipya tofauti kila miaka mitano. Je, ni kwa kiasi gani kwa kipindi kilichopita Serikali iliweza kutekeleza Mipango yake? Je, katika Mpango huu vyanzo vya mapato vitapatikana wapi ukizingatia baadhi ya wahisani wamejitoa kusaidia nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lako Tukufu kila mwaka Serikali imekuwa ikitueleza inataka kuongeza watalii wafike zaidi ya milioni moja wanaoitembelea Tanzania. Nchi yetu ina vivutio vingi sana kupita nchi nyingine Afrika Mashariki, lakini kuja Tanzania ni gharama sana kuliko Kenya, Uganda au Rwanda. Hii inatokana na kutokuwa na usafiri wetu wa anga kutoka nchi za Ulaya na Marekani. Je, Serikali ina mikakati gani ya kufufua Shirika letu la *ATCL* ili kuweza kuimarisha na kukuza utalii kwa lengo la kupata watalii wengi kuja moja kwa moja mpaka Tanzania badala ya kupitia Kenya inayofanya Utalii wa Tanzania uwe ghali sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa jinsi gani Mpango huu utatekelezwa, kutengeneza reli zetu angalau ziweze kuwa na mabehewa ya mizigo badala ya mizigo na makontena yanayosafirishwa kwenda nchi jirani kama Kongo, Zambia, Rwanda kutumia barabara. Hii inachangia sana kuharibu barabara zetu haziwezi kudumu. Mfano, barabara kutoka Chalinze- Dodoma tu, tayari barabara hii imeharibika kabisa na tangu ijengwe haina hata zaidi ya miaka 20? Serikali itueleze ina mpango gani wa kufufua reli kwa uhalisia siyo kwa maandishi ya hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima, lakini hadi sasa hivi bado kilio chetu ni cha kutegemea mvua na wakulima wengi hawana mitaji. Wengi vijijini bado wanatumia ng'ombe kulimia na wengi hawapati elimu ya kutosha kuhusu mazao ya biashara na Serikali haisaidii ni kwa jinsi gani itawezesha kuhusu kilimo cha umwagiliaji ili waweze kulima kwa kipindi chote mwaka mzima. Je, Serikali ina mikakati ya kuzalisha mbegu za kisasa hapa nchini ili ziwe kwa bei nafuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu nyingi zinatoka nchi za nje na tukumbuke mbegu kutoka nje zinaagizwa kwa fedha za kigeni ukizingatia fedha yetu thamani yake inashuka kila siku na deni la Taifa linakua kila siku. Je, Serikali

inachukua mkakati gani, kuendeleza kilimo ili tuondokane na kilimo cha kutegemea mawingu, kilimo cha jembe la mkono badala ya kuleta kauli mpya kila wakati?

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utahudu viwanda na biashara na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda; Mkoa wa Mara ni Mkoa ambao ulikuwa na Viwanda vikubwa, lakini sasa hivi vimekufa na viwanda hivyo ni *MUTEX*. Hiki Kiwanda cha *MUTEX* kimepoteza ajira nyingi sana za wananchi hasa kwa vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa hili. Ni vizuri Serikali ikajipanga tena upya kufufua kiwanda hiki. Vile vile ningependa kuishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa kufungua mnada wa Tarime mpakani, hii itasaidia kutoa ajira kwa vijana na kuepukana na vitendo viovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mazingira; kutokana na tabianchi hii inayotokana na Mkoa wa Mara kuwa na wafugaji na upatikanaji wa chakula na maji ya mifugo hiyo na kuhamahama kwa mifugo (wanyama) na wingi wa mifugo hiyo wanakandamiza sana ardhi na kusababisha maji kutokupenya ardhini na kusababisha mafuriko na kutuama kwa maji ambayo yanapelekea mazalia ya mbu na kuleta kipindupindu na madhara mengine kwa binadamu na hata kwa mifugo yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu, hii ni sekta ambayo Serikali izingatie na kuipa kipaumbele.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe na timu yako jinsi unavyotuongoza. Pia nampongeza Waziri wa Fedha na Mipango kwa kazi nzuri aliyoifanya inayoonekana kwenye Mpango wa Miaka Mitano aliouleta. Aidha, naipongeza Kamati ya Bajeti kwa maoni yao yanayoleta nuru zaidi katika mikakati ya Maendeleo iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuokoa muda nitachangia kwa kuuliza maswali ya kimkakati *(strategic questions)* ambayo naamini yakijibiwa yataboresha Mpango mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi sasa imepata Rais ambaye pia ni Kiongozi. Kwa hiyo, tuna mtu wa kutuonesha njia ili tujue tunakwenda wapi. Juhudi za Kinabii ambazo Rais, John Pombe Magufuli (JPM) anafanya nchi yetu inaweza sasa kuwa na mpango na kuutekeleza. Pia ninapochangia kwa kuuliza maswali naamini Mheshimiwa Waziri atayafanyia kazi na yale yanayohitaji mwongozo wa Kiongozi wa nchi atayawakilisha. Kwa mantiki hiyo, nauliza kimkakati yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, aya ya 12; kama mfumuko wa bei umepungua kutoka asilimia 9.8 mwaka 2011 hadi alimilia 5.6 mwaka 2015, kwa nini riba katika mabenki yetu yote imebaki juu sana? Riba kubwa ya tarakimu mbili haiwezi kusaidia kusukuma shughuli za uzalishaji katika sekta husika *(productive investments)* riba za tarakimu mbili ni kwa wachuuzi wasiochangia uzalishaji mali na uwekezaji. Nini mkakati wa Serikali kutatua changamoto hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, aya ya 14; umaskini; ni jambo jema kwamba kama Taifa tumepunguza umaskini. Hata hivyo, ili jambo hili liaminike takwimu za umaskini ziwe zinatolewa kimkoa na kiwilaya ili mikakati iwekwe kulingana na eneo husika, ili mikakati iwekwe kulingana na eneo husika. Katika Jimbo langu la Muleba Kusini hali ya umaskini imeongezeka. Katika Jimbo langu Tunahitaji mikakati maalum inayohusu maisha na shughuli zetu, Mpango wa Miaka Mitano unahitaji kugatuliwa kwenda ngazi za wilaya na hata vijiji ili tupambane vizuri na hali halisi na kuweza kuboresha maisha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja linalochangia Wilaya kama Muleba kubaki nyuma kimaendeleo ni kwa Taifa kutokuwa na *specific program* za Wilaya kubwa kieneo *(geographic size)* na wingi wa watu *population size*. Kwa Tanzania bara mgao wa fedha za maendeleo hauzingatii vigezo hivyo. Kwa hiyo, bajeti ya maendeleo inawasaidia zaidi wenye maeneo madogo kuliko wenye maeneo makubwa na watu wengi. Matokeo ni kugawa Mikoa, Wilaya, Vijiji na Majimbo vipande vipande, yaani hivi sasa kwa mtazamo wa kiuchumi kuna utitiri wa maeneo ya utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la wazi kwamba, maeneo ya utawala yakiongezeka na gharama za uendeshaji wa Serikali zitaongezeka. Ingawaje kuna sehemu ambapo ugawaji wa maeneo yataleta ufanisi tusisahau kuwa teknolojia ya mawasiliano, usafiri na miundombinu bora inaondoa umuhimu huo. Kwa mfano, ilikuwa inachukua masaa 36 kuendesha gari kutoka Dar es salaam kwenda Bukoba, hivi sasa ni masaa 16. Kwa hiyo, kinachotakiwa ni mpango mkakati wa kuwa na Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano na bajeti za kuitekeleza iliyojikita na inayozingatia na yenye uwiano wa ukubwa wa eneo na wingi wa watu waliomo kwa Tanzania Bara. Bila hivyo utakuta umaskini unaongezeka katika Mikoa na Wilaya kubwa.

Hii ni tofauti kabisa na malengo ya kuiendeleza Tanzania kwa misingi ya usawa iliyokuwa wenye Mpango wa Maendeleo wa Kwanza wa 1964-1963 *(1st Year Development Plan)* Mikoa kama Kagera ilitakiwa kupiga *mark time* kusubiri wengine, sasa imerudi nyuma na inashika mkia.

Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unatakiwa kuwa na uchambuzi huu wa usalama na uwiano wa maendeleo ya mikoa- *(regional equality)*. Bila hivyo umaskini na kutokuwa na usawa vinaweza kuwa chanzo cha vurugu na kuharibu amani na utulivu wa nchi yetu. Mheshimiwa Rais Magufuli, ana uwezo na upeo wa kurekebisha hali hii isiyoridhisha aliyoirithi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwekezaji (Ibara ya 28); Mpango unakiri kuwa uwekezaji wa sekta binafsi haukufikia malengo. Hili ni jambo zito linalohitaji kuchunguzwa kwa kina. Haitoshi na ni kujidanganya kujivunia uwepo wa rasilimali nyingi chini bila kuwa na uwezo kifedha, kiteknolojia na kiutawala *(managerial capacity)* kuziendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo unahitaji kuweka bayana mikakati ya kuondoa balaa hili, kuwa na rasilimali ardhi bila uwezo wa kuitumia. Badala ya mashamba tuna mapori, tuna rasilimali maji, lakini samaki wanavunwa na Mataifa mengine kwa sababu ya uvuvi duni. Tuna rasilimali misitu lakini hatuna wataalam wa kuvuna misitu na kutengeneza fenicha za kuuza nje, tunaishia kuuza magogo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya Matokeo Makubwa Sasa; jambo hili linahitaji kuangaliwa kwa kina lisijekutwa ni jipu. Mishahara mikubwa inayodaiwa kulipwa kwa Watendaji wa Sekretarieti hiyo ni vyema iwekwe wazi na katika kufanya hivyo sera na mpango wa mishahara endelevu ufafanuliwe kwa wote. Gharama za uendeshaji zikizidi mapato hatuwezi kwenda mbele, tutakwamba. Naunga Mkono uamuzi wa Mheshimiwa Rais, kutangaza mshahara wake na kupendekeza suala la mishahara mikubwa sana kuangaliwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu; kinachohitajika ni reli, reli, reli kila mahali. Bila hivyo ni vigumu kuendelea na kushindana katika kilimo. Aidha, barabara za vijijini *(access roads)* zipewe kipaumbele. Barabara ya Muleba – Kinyambogo - Rubya. Kwa kiwango cha lami ni mfano hai wa jinsi barabara za vijijini zinavyosahaulika. Naamini Mheshimiwa Magufuli atatusaidia kutekeleza jambo hili ambalo alilifanyia kazi alipokuwa Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naamini maswali yangu yakijibiwa tutafanya maendeleo.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anazozifanya. Naomba nimpongeze Dkt. Mpango kwa uwasilishaji wake mzuri.

Naomba kuishauri Serikali katika mambo yafuatayo:-

Ni vyema kuweka wazi mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika Mpango wa Kwanza 2011 – 2016 ili tujue tatizo ni nini? Serikali imeamua maamuzi yapi kwa yale mambo ambayo bado hayajakamilika.

Mpango huo ulilenga kutanzua vikwazo vya kiuchumi na kupunguza umaskini na kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuuaji wa pato la Taifa 6.7% - 7% unalingana na upatikanaji wa huduma za jamii kama afya, maji na elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa uchumi uende sambamba na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipaswa kuweka wazi vigezo vilivyotumika kujua uchumi wa Taifa unakua, *income per capita* peke yake hatoshi kwa sababu upatikanaji wa *income per capita* unajumuisha matajiri sana na maskini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumuko wa bei unasababishwa mara nyingi na *cost push inflation* na *demand pull inflation*. Naipongeza sana Serikali kwenye eneo la *demand pull inflation* ni muda mrefu sasa tumeweza kuhimili mahitaji ya chakula ndani ya nchi lakini kwenye *cost push inflation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametaja eneo la mafuta, ni vyema Serikali ikajipanga kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana na wa bei nafuu. Serikali ihakikishe umeme wa makaa ya mawe, maji na upepo unapatikana ili kupunguza adha ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali ihakikishe barabara za uhakika maeneo yote yenye kilimo cha uhakika kwa lengo la kupunguza gharama pia reli ianze kufanya kazi kwenye maeneo yote muhimu.

Mheshimwa Spika, eneo lingine ni kuhusu thamani ya shilingi ambayo inashuka na haiko *stable*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa Serikali ikaweka mkakati wa kuondoa matumizi ya *dollarization* ambayo nchi nyingi duniani zimedhibiti eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunauza kidogo nje ya nchi kuliko tunavyonunua. Ni vyema sasa tujidhatiti kuongeza kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo; asilimia sabini na tisa ya Watanzania inategemea kilimo, ni vyema tukajipanga katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaanza kuwasikiliza Mawaziri wakijibu baadhi ya hoja, baadaye tutamsikiliza Waziri mtoa hoja. Tutaanza na Waziri Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUNGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika Mpango wa Maendeleo ambao umewekwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme tu kwamba sisi kama Wizara tumepokea michango na maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu Mpango, na tumepokea maoni na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge yanayolenga katika Wizara yetu, yote tumeyapokea na tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii huenda nisijibu yote kwa ajili ya muda, lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge mambo mawili kwamba la kwanza tumepokea maoni yao, na pili tutaendelea kujibu kwa sababu bado tutakuwa na fursa ya kufanya hivyo katika majibu ya bajeti za kisekta ambapo Waheshimiwa Wabunge watachangia tena katika bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea wachangiaji wote ambao waliigusa katika Wizara ya Kilimo, lakini pia walipogusa katika Mpango kwa ujumla. Niseme tu kwamba Mpango wa Maendeleo ambao umewekwa mbele yetu umeipa nafasi kubwa sekta ya kilimo, na umeipa nafasi kubwa pale ulipoongelea kwamba mpango unalenga kunufaisha viwanda na kuinua viwanda hasa vinavyotokana na mazao ya kilimo.

Jambo la pili Mpango huu umeipa fursa kubwa sekta ya kilimo, kilimo kwa dhana pana, kwa maana ya kilimo, mifugo na uvuvi pale ulipoongelea kwamba unapanga kuhuianisha maendeleo ya viwanda pamoja na maisha ama maendeleo ya watu. Ikumbukwe kwamba katika nchi yetu kilimo kinaajiri asilimia kubwa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hata katika maeneo ambayo Mpango huu umeongelea neno kilimo ni kwa maana pana ambapo unaongelea mazao, unaongelea mifugo na unaongelea uvuvi.

Nikienda katika eneo moja moja, machache, Mheshimiwa Ally Saleh alisema kwamba ianzishwe na Benki ya Uvuvi. Katika Benki ya Kilimo inatamkwa kilimo lakini ni kwa dhana pana ambapo uendelezaji wa mazao ya kilimo, kwa maana ya mazao yanayotokana na kilimo mikopo yake inapatikana katika Benki ya Kilimo, lakini pia kwa wale ambao wanaendeleza mazao ya mifugo na wenyewe wanapata fursa hiyo sawa na upande wa mazao, lakini vivyo hivyo kwa upande wa uvuvi. Jambo hili tulilisemea hata tulipokuwa tunajibu swali la jana ambalo lilikuwa linahusisha mambo ya ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Yahaya Massare aliongelea kuhusu malisho pamoja na Waheshimiwa wengine ambao waliongelea kuhusu malisho ya Mifugo akiwemo ndugu yangu wa Jimbo la Kilindi na ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, pamoja na ndugu yangu Mheshimiwa Kakunda na wengine wote ambao waliongelea kuhusu malisho. Jambo hili la malisho kwa mifugo siyo jambo la siku moja, sisi kama Serikali tunaendelea kulifanyia kazi kwa sababu linahusisha Wizara zaidi ya moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Lukuvi ambaye tumekuwa tukishirikiana naye mara kwa mara yanapotokea matatizo ya migogoro yanayohusisha matumizi ya bora ya ardhi. Waheshimiwa Wabunge, jambo la matumizi bora ya ardhi halianzii kwenye ngazi ya Wizara bali linaanzia katika Kamati zetu za matumizi bora ya ardhi ambazo ziko katika ngazi ya vijiji. Wabunge kama wawakilishi tushiriki katika kutoa maoni na katika kutenga maeneo katika matumizi bora ya ardhi pale Kamati zetu zinazotenga matumizi bora ya ardhi zinapokutana. Mimi kama Waziri ni dhahiri kwamba naunga mkono jitihada za Kamati zetu zinapokuwa zinakutana kwa ajili ya kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo liliongelewa na Waheshimiwa Wabunge wengi lilikuwa jambo linalohusu makato katika mazao. Jambo hili pia kwa sababu linahusisha Wizara zaidi ya moja tumeendelea kuyafanyia kazi na tunaamini tunavyoenda katika Bunge hili la Bajeti ambapo mwishoni kabisa tutatengeneza *Finance Bill,* tunategemea yale ambayo yanahusisha tozo ama makato ambayo yanaangukia katika sheria zinazopita katika Bunge letu tutapata fursa ya kuyangalia, lakini Wizara ya Kilimo pamoja na TAMISEMI pamoja na Wizara ya Fedha tumeendelea kuyafanyia kazi haya kwa sababu tayari uamuzi wa Serikali ulishatoka kuhakikisha kwamba tunawatengenezea mazingira bora wakulima, wafugaji na wavuvi ili waweze kufanya kazi zao na kuweza kujiletea tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tunalifanyia kazi, Waheshimiwa Wabunge ambao wengi wenu mmeliongelea ni kuhusu pembejeo. Jambo la pembejeo linalohusisha ruzuku, Serikali tunaendelea kulifanyia kazi kuangalia utaratibu mzuri ambao utakuwa endelevu na ambao

hautaruhusu mianya ya matumizi mabaya ya fedha za umma ambayo yanatokana na baadhi ya mifumo ambayo tumekuwa tukiitumia ya ugawaji wa ruzuku. Kwa hiyo, katika jambo hili, kwanza tunaangalia utaratibu ambao utakuwa endelevu, lakini vilevile tunaangalia utaratibu ambao utagusa watu waliowengi wanaohusika katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili tuliangalia uwezekano wa kuangalia kwanza fedha ambazo zinapatika katika kila sekta, tuliangalia hata katika mazoa utaona makato mengi yaliyokuwa yanalalamikiwa ni makato ambayo hayaendi kuendeleza sekta husika, tunaangalia uwezekano wa makato hayo yaweze kunufaisha sekta na ambayo hayanufaishi sekta yasiwekwe kwenya sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia100 kwa 100, na niendelee kusema kwamba kama mnataka mali mtazipata shambani!

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Charles John Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Mpango wa Pili wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhima ya Mpango wa Pili wa miaka mitano ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Ninaunga mkono dhima hiyo, nikijibu michango ya Waheshimiwa Wabunge, nataka niwaeleze, ukisoma falfasa ya viwanda, watalaam wa falsafa ya viwanda wanakwambia kujenga uchumi wa viwanda ni vita na ukirejea maandiko ya Mwalimu, mnapokwenda vitani lazima wote muungane mkono. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya Watanzania niwaombe tuunge mkono ujenzi wa uchumi wa viwanda, asitokee mtu akabaki nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ni vizuri kujenga uchumi wa viwanda? Uchumi wa viwanda unatusaidia kutengeneza ajira. Watanzania wenzangu mkubali, Tanzania ni Taifa changa kama Afrika lilivyo *continent* changa, zaidi ya asilimia 65 ya Vijana wetu au watu wetu wana umri wa usiyozidi miaka 35, maana yake ni kwamba hawa watu wanataka ajira. Sekta inayoweza kutengeneza ajira ni viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakwenda kwenye kitendawili cha viwanda gani tunavitengeneza! Kama alivyosema pacha wangu akirejea usemi wa babu, ukitaka mali utaipata shambani. Tutalenga sekta ambazo zitawashirikisha watu walio wengi na watu walio wengi wapo katika sekta zile za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo niwashawishi Watanzania, sisi mali tunazo, viwanda vitakavyotutoa ni viwanda ni viwanda vidogo sana, viwanda vidogo na viwanda vya kati, hivi ndivyo viwanda vitakavyotutoa, niwahakikishie Watanzania wanao uwezo wa kufanya hivyo. Badala ya kujenga nyumba ukifanya tathmini ya nyumba zilizojengwa katika Miji, zile zinazoitwa *dead capital, dead capital* unajenga nyumba yako ya ghorofa unafika ghorofa ya tatu huwezi kuendelea, hiyo inaitwa *dead capital,* ukiorodhesha nyumba zote ambazo ni *dead capital* au zile zinazojengwa zikaisha zikawekwa vibao vya tunapangisha kwa miaka sita hizo zote ukijulisha na uka-*convert* pesa yake ukaiweka kwenye viwanda vidogo na viwanda vya kati, vijana wote watapata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwapa utangulizi wa kazi ambayo nitaifanya kwa miaka mitano ni kuwahimiza Watanzania tubadilishe sasa mtazamo ili tuwekeze kwenye viwanda. Jambo la kuwaambia Watanzania ni kwamba sera ipo, *Sustainable Industry Development Policy* ipo ya mwaka 1999 mpaka inakwenda mpaka 2020, tunao mkakati unaitwa *Integrated Industrial Development Strategy* ipo ya 2025.Waheshimiwa Wabunge niwadokeze kitu kimoja kuhusu suala la Kurasini, suala la Kurasini linapotoshwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape siri ya *Kurasini Logistic Industrial Area* tunalenga kwamba sisi tuwe kituo cha mauzo ya nchi zilizotuzunguka, huwezi kuzuia China kuuza nchi za Afrika. China ni soko kubwa sasa tunawaleta hapa. Pia niwape siri msiwambie watu, tunalenga kudhibiti bidhaa *substandard* tunataka bidhaa zote zitengenezwe Kurasini, bidhaa ambazo ni *substandard* hazitaingia hapo, ndiyo mpango mzima na wanaotetea wanaogopa hiyo! Hakuna *substandard* itaingia pale itaanzishwa kitu kinaitwa *Total Quality Management (TQM), TBS* ambayo iko chini yangu nitawahamishia pale kila kitu kinachoka China kitengenezwe pale na msiwe na wasiwasi kwamba Kurasini itaharibu viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nina orodha ya wawekezaji, kuna mwekezaji mmoja anakwenda Tanga anatengeneza kiwanda cha saruji tani milioni 2.5 huyu anazuiliwa na Kurasini? Kuna mtengenezaji wa vigae nimempeleka Mkuranga, muulize Mbunge wa Mkuranga atatengeneza *square kilometer* 80,000 ambazo zitatosheleza Afrika yote, huyu anazuiliwa na Kurasini? kama walivyosema uulize jambo uelezwe, kwa hiyo, kila kitu kina mpango wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie *EPZ*. *EPZ* ni muhimu na inatenguwa kile kitendawili cha wepesi wa kufanya shughuli. Wawekezaji hasa vijana wanaotoka shule wameshindwa kufanyakazi kwa sababu hawakupa maeneo ya kufanyia kazi. Maelekezo ya Serikali ni kwamba kwenye Halmashauri za Miji kuanzia Vijiji, Kata, Tarafa mtenge maeneo mkija ngazi ya Kanda inakuwa ni *EPZ* na wale wanaodai tunapambana kuhakikisha wote wanalipwa. Hii ina maana kwamba tukitengeza *EPZ* tukatengeza maeneo, wawekezaji wanaokuja kuwekeza, Watanzania tunawapa maeneo wanaanza shughuli, na wale wanaotoka nje tutawaelekeza kwenye *EPZ*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja niwape taarifa muelewe. Viwanda vya dunia vilivyokuwa Asia sasa vinarudi Afrika. Viwanda vya dunia nzima vilivyokuwa vimekwenda Asia vinakuja Afrika na mtu asikudanganye, Afrika maana yake ni Tanzania! Kwa hiyo, *EPZ* zimeandaliwa kuwapokea. Ninazo *square kilometers* 100 ziko Bagamoyo, Songea nitawafidia, napeleka kwetu Kigoma, iko ile ya Manyoni, nakwenda Bunda - Mara kuweka *EPZ* na wanaodai wote watapewa fidia. Watu wa Tabora wamelalamikia *EPZ, EPZ* pitieni ngazi ya Mkoa malizeni matatizo yenu, niiteni mimi ndiyo mwenye mamlaka ya *EPZ* nitawapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Dodoma wameniuliza pale nje kwamba Dodoma mbona hamna *EPZ,* Mbunge wa Dodoma usiwe wasiwasi *EPZ* nitawapa. Mimi ndiyo mwenye mamlaka ya kutoa *EPZ*. Tengenezeni mazingira, wakaribisheni Wawekaezaji lazima tutengeneze uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii niongee machache kwa kutoa ufafanuzi kwenye hoja za msingi na nzuri ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Kwa kuwa huu ndiyo mwanzo wa mjadala wetu wa Bunge la Bajeti basi tutakuwa na fursa zaidi ya mara moja, ya kuendelea kueleza yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyaleta na kwa sasa tu niwashukuru sana wale ambao wameongelea suala la utalii ambalo nitalitolea ufafanuzi kidogo katika mawasilisho yangu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge walioongelea juu ya sekta yetu wako kumi na wengi wao waliongea juu ya Utalii kama ambavyo nilisema. Jana Mheshimiwa Mbunge mmoja alitupa takwimu kidogo, ni kweli kwamba mchango wa sekta ya utalii katika uchumi wetu ni mkubwa na unafikia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa na inachangia asimilia 25 au robo nzima ya mapato yote,

hii inatokana na watalii 2,200,000 ambao wanakuja kwetu sasa. Hii ni takwimu ambayo ilifikiwa mwaka 2014 na ninategemea sasa hivi tunakokotoa tumefika karibu mwisho wa kukokotoa idadi ya watalii waliokuja mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe ufafanuzi kidogo kwamba mwaka 2010 ni kweli walikuja watalii 800,000 na wale waliohesabiwa mwaka 2014 walikuwa hao 1,200,000 na kwamba kulikuwa na ongezeko hapo karibu watalii 500,000 katika kipindi hicho. Siyo kwamba, katika miaka hiyo watalii waliokuja ni hao 500,000 gawanya kwa sita au 89,000 kama ilivyosemwa. Maana yake ni kwamba hao 89,000 ni wale wanaongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kutoka 500,000 mwaka 2006, wakafikia 800,000 mwaka 2010, laki tisa, milioni moja, milioni 1.2 ni ongezeko na hiyo 900,000 ni kwa mwaka. Tofauti kati ya milioni 1.2 na 800,000 ile ndiyo ongezeko lililotokea katika kipindi hicho, siyo kwamba katika mwaka mzima waliingia wale ambao wameongezeka tu, hata kidogo!

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba fursa zetu za utalii ni nyingi na kwamba watalii ambao wanakuja hao milioni 1.2 ni wachache sana. Lakini katika uchache wao ndiyo waliochangia robo ya mapato yetu yote ya kigeni hapa nchini. Kwa hiyo, tuna lengo la kuongeza mapato haya kutoka bilioni 2.3 ya sasa na kuyafikisha bilioni tano mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka huu tataanza mpango kabambe kabisa wa kutangaza kwenye masoko ya ndani na yale ambayo yanatuletea watalii wengi katika nchi yetu. Tutatangaza Marekani ndiyo nchi ya kwanza kutuletea watalii, mwaka 2014 iliileta watalii karibu 500,000, tutatangaza Uingereza, Jamhuri ya Muungano wa Kijerumani, *(Federal Republic of Germany)*, Italia na nchi zile ambazo zinatuletea watalii wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tuna lengo la kushirikiana na *United Arab Emirates* ili watalii wale wanaofika Dubai milioni 27 kwa mwaka, angalau milioni tatu waweze kuja Tanzania kama sehemu ya safari yao kule Dubai. Kwa hiyo, kuongeza watalii wetu kwa idadi hiyo na tunaamini kabisa kwamba baada ya mipango hii kutekelezwa tutakuwa tumefikia mapato ya dola za Kimarekani bilioni tano kwa mwaka na kuongeza idadi ya Watanzania walioajiriwa katika utalii moja kwa moja 500,000 mpaka wafike milioni 1.2 na wale ambao wanaohudumia utalii kutoka milioni moja kufika milioni mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, sekta hii ni muhimu sana na sisi wenyewe tumejiandaa kwa kuyalinda haya mapori ambao ni nje ya *TANAPA* na nje ya Mamlaka ya Ngorongoro kwa kuanzisha mamlaka mpya inaitwa *Tanzania Wildlife Authority*. Italinda mapori tengefu, italinda *game reserves* na italinda na

maeneo ambayo yako wazi ili kuhakikisha kwamba wanyama katika maeneo hayo wanatumika kwa faida ya Taifa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana ndugu zangu baada ya hutuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kujadiliwa basi, tutaendelea kutoa ufafanuzi. Mimi naunga sana mkono hoja hii, ahsante sana! *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Injinia Edwin Amandus Ngonyani atafuatiwa na Mheshimiwa January Makamba na Mheshimiwa Dokta Merdad Kalemani ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kuingia katika jengo hili kwa mara ya kwanza. Kupitia fursa hiyo naomba niwashukuru wapiga kura wote wa Jimbo la Namtumbo kwa kazi waliyoifanya pamoja na mateso yote ya kupiga kura mara tatu na mwisho nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kunipa nafasi hii ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Pili ni mwendelezo wa Mpango wa Kwanza pamoja na nyongeza inayozingatia dhima ya Serikali ya Awamu ya Tano kuijenga Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miundombinu iliyopangwa katika Mpango wa Kwanza na hii iliyoongezeka katika Mpango wa Pili yote inahitajika na tutaihitaji katika mpango wa tatu. Kwa hiyo, hoja kwamba tulitekeleza asilimia 53 tu katika awamu ya kwanza ni kutokana na uwezo wetu, sasa tunaingia katika Mpango wa Pili tutamalizia asimilia 47 pamoja na nyongeza nyingi ambazo zipo katika Mpango huu wa Pili, ambao Mheshimiwa Dokta Mpango ameuleta na kwa kweli naomba nichukuwe fursa hii nimshukuru sana alikuwa amechelewa kuja nafasikatika hiyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wameongelea umuhimu wa miundombinu, nashukuru sana Bunge zima limeungana katika kukubali Mpango, tunatofautiana katika utekelezaji, wapo wanaodhani utekelezaji hautafanyika na wapo wanaoomba tupate nguvu tutekeleze. Kwa maana nyingine Mpango wote tunaukubali, labda katika eneo moja tu ambalo Mheshimiwa Bashe ametoa maoni tofauti kwamba suala la kufufua Shirika letu

la *ATCL* liangaliwe kwa namna tofauti kwa kuzingatia hasara zinazopatikana katika mashirika ya ndege duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Bashe na wengine wenye dhana kama yake, usafiri wa anga ni *necessary evil* kwa nchi yoyote, hatuwezi kuukwepa. Inawezekana *from micro point of view* kampuni ikapata hasara, lakini kama nchi usafiri huo unachangia katika sekta mbalimbali na *overall* sekta hiyo ya usafiri wa anga inatuletea faida kubwa, hatuwezi tukaiacha ikashikiliwa na wafanyabiashara peke yao, muda wowote wanaweza wakaondoka kwa sababu wao wanaangalia faida na wanaangalia faida katika kampuni yao peke yake, wakati sisi tunaangalia faida kwa mapana yake ni pamoja na mchango wake katika sekta ya utalii na masuala mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumedhamiria, kujenga reli ya *standard gauge* ya Kati na matawi yake yote, ya *Mtwara Corridor* na ya Kaskazini. Dhamira hiyo kama ambavyo mtaiona katika bajeti inayokuja na mmeona katika kitabu cha Mheshimiwa Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, tumeshaonyesha kwa kutenga trilioni moja haijawahi tokea! Kwa hiyo, naomba mtuamini. Ninalo jembe linaloniongoza, linaloongoza Wizara hii, Profesa Makame Mnyaa Mbarawa. Kwa wale wanaomfahamu yale aliyoyafanya katika Wizara ya Mawasiliano, aliyafanya kimya kimya wanamfahamu ni mtu wa aina gani na mimi nashukuru kufanya kazi chini yake, kwa sababu naamini nitaweza kukidhi haja yangu ya kuwatumikia Watanzania kwa namna ambayo tutafika huku tunakokwenda, uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutatoka kwenye kusherehekea *flyover* na *interchanges* moja tutakuwa na *flyovers* na ma-*interchanges* nyingi sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ngonyani muda wako umekwisha!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Aah, ni kengele ya kwanza hiyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuunga mkono kwa nguvu sana na kwa kutupendelea sisi watu wa miundombinu na hatutawaangusha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa January Makamba, Mheshimiwa Merdad Kalemani ajiandae.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na nianze

kwa kutoa pongezi kubwa kwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuandaa Mpango madhubuti waliouwasilisha hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tulienda kwenye uchaguzi na kila chama kilitoa ahadi kwa Watanzania. Watanzania wakakiamini Chama cha Mapinduzi na wakaamini kwamba ahadi za CCM ndizo zinazotekelezeka, jukumu la kwanza kabisa la chama kinachoshinda uchaguzi ni kuunda Serikali. Kwa hiyo, Serikali imeundwa, Serikali imara na Serikali madhubuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kwanza la Serikali iliyoundwa baada ya uchaguzi ni kutengeneza mpango unaotafsiri Ilani na ahadi za chama kilichoshinda. Hilo ndilo tunalolifanya sasa. Jukumu la pili la Serikali iliyoshinda ni kutengeneza bajeti za kila mwaka za kutekeleza mpango ambao tumesema unatafsiri ilani na ahadi za chama, hilo ndilo linalokuja katika kikao hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mantiki ya kawaida inasema kwamba kama wenzenu wameshinda, wameunda Serikali, wametengeneza mpango ambao unatafsiri yale yaliyowafanya washinde, wenzenu mnapaswa kuwapa nafasi watekeleze mipango yao na bajeti yao. Wanaposhindwa baada ya miaka mitano au katikati tunapofanya tathmini ndipo tunapokuja na kusema ninyi mmeshindwa. Hatuwezi wakati tunatengeneza mpango wetu ambao unatafsiri yale tuliyowaahidi Watanzania tunasimama tunasema ninyi kile, ninyi kile, ninyi hiki. Tupeni nafasi, ni Serikali mpya, tutekeleze ya kwetu katika mwaka wa kwanza kabisa wa Serikali hii ndipo tuje tuzungumze yale ambayo...

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa staili na kasi ya Serikali hii ya Awamu ya Tano hakuna hata chembe ya shaka kabisa kwamba yale tuliyoyaahidi, tuliyoyaandika katika Mpango wetu huu na katika bajeti tutakayoileta yatatekelezwa kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitazama sura, kauli, umakini wa Rais wetu na Wajumbe wa Baraza lake la Mawaziri na Wabunge wa upande wa CCM kwa ujumla, hakuna shaka yoyote kwamba tumedhamiria kutengeneza nchi mpya. Tumedhamiria kutengeneza Taifa jipya, Taifa lenye haki, Taifa lenye usawa na Taifa lenye heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma katika miaka mingi tulijaribu kutengeneza Taifa la namna hiyo…

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika Taarifa!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri naomba ukae!

TAARIFA

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mzungumzaji Mheshimiwa Waziri anajaribu kulipotosha Bunge kwa kusema kwamba chama kilichopata nafasi ya kuunda Serikali kina wajibu wa kuandaa Mpango, jambo ambalo ni kweli, lakini sisi kama Wabunge tumekaa Kikatiba na tunaujadili Mpango huu kama Wabunge halali kwa mujibu wa Katiba, kwa hiyo sisi siyo *intruders* kuujadili Mpango huu. Ningeomba maneno haya ayatoe kwa sababu anajaribu kuivunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa sisi kuujadili Mpango huu. Ndani ya Bunge hili siyo CCM tu ndiyo wanaotakiwa kuujadili, ni Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri January Makamba umepewa taarifa, unaikubali au?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshimia na taadhima napenda kuikataa taarifa hiyo na napenda kuikataa bila kueleza sababu, sababu za kuikataa ni dhahiri kabisa. Isingependeza kupoteza muda kueleza sababu za kuikataa kwa sababu zinaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika naomba niendelee …

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika Taarifa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika…

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nitaruhusu hiyo taarifa lakini hatutafika mwisho labda kama tunataka kutengua Kanuni ili tuongeze muda.

Mheshimiwa Waziri samahani, naomba ukae. Mheshimiwa Waitara, taarifa!

TAARIFA

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (8) kwamba yeye alikuwa Waziri wa Serikali iliyopita kwa hiyo hawezi kutengeneza Taifa jipya na Serikali mpya na nchi mpya. Kwa hiyo atakuwa anadanganya watu. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri January Makamba umepewa taarifa, unaikubali au unaikataa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilinde na naomba ulinde muda wangu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba basi tusikilizane!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa aina ya taarifa iliyotolewa haistahili hata kuielezea kwa nini naikataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kwa kueleza kuhusu mazingira. Nashukuru sana kwamba katika Bunge hili kuna Wabunge wengi wanamazingira na naomba sana tutakapoleta bajeti yetu ya Ofisi ya Makamu wa Rais tutatoa dira mpya na mwelekeo mpya wa namna ya kulinda na kuhifadhi mazingira ya nchi yetu, tunaomba mtuunge mkono. Tutaeleza namna tunavyotaka kujenga uwezo wa kitaasisi wa Serikali na uwezo wa kifedha wa Serikali katika kugharamia shughuli za ulinzi wa mazingira. *(Makofi)*

Mwisho ni kuhusu Muungano, kuhusu Uchaguzi wa Zanzibar. Vitabu vinavyotuongoza kuhusu suala la Zanzibar kwa maana ya Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar vinatuelekeza kwamba jambo hili limekwisha. Suala hili limekwisha, treni imeshaondoka kwenye kituo, wenzetu hawakushiriki, wamefanya uamuzi wa kimkakati ambao umewaondoa katika ushiriki wa siasa na maendeleo ya Zanzibar. Ni uamuzi wao, ni uamuzi ambao wataendelea kuujutia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama CCM tunaamini kwamba ujenzi wa Taifa letu kwa ujumla ni jukumu letu sote na tunawakaribisha wenzetu hata kama wako nje ya Serikali kuendelea kushirikiana na sisi kuijenga Zanzibar na kuijenga Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dokta Merdad Kalemani!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu waliotangulia, kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa mara ya kwanza kabisa kuonekana kwenye Bunge lako Tukufu na mimi nikichangia Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na azma ya Serikali ya hapa kazi tu, haijaishia kwenye maneno. Mwanzoni mwa mwezi huu Mheshimiwa Rais alizindua mradi wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi Namba II *megawatt* 240, lakini mwishoni mwa wiki hii pia amezindua pia ujenzi wa *flyover* katika barabara ya kuelekea uwanja wa ndege na kama haitoshi juzi amezindua pia ukamilishaji wa Daraja la Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Watanzania wote, Waheshimiwa Wabunge na sisi wananchi, tufanye kazi moja ya kutwanga maendeleo, hakuna kazi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze sasa kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika mchango huu wa Mpango wa Maendeleo wa Pili. Katika Mpango huu nijielekeze moja kwa moja katika ukurasa wa 10, kadhalika ukurasa wa 28. Ukurasa wa 10 Waheshimiwa Wabunge, suala la nishati limezungumzwa kwa kirefu sana japo kwa maneno machache, nami niongezee sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnavyotambua Waheshimiwa Wabunge, Serikali ya Awamu ya Tano, kwa wananchi na Waheshimiwa Wabunge tunasema suala la nishati sasa ni la kufa na kupona. Tutake tusitake tutazalisha umeme wa kutosha kujenga viwanda vyetu. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa ridhaa yako Naibu Spika kwa jinsi ambavyo wanaunga mkono kuelekeza nguvu za wananchi kwenye kuzalisha umeme wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 10 wa Mpango huu umezungumza kwamba mwaka 2016 tungefikisha *megawatt* 2,780, bado tunatembea 2016 inaendelea, lakini hata hivyo nguvu kubwa sasa inayoonekana niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge na wananchi, sasa hivi *megawatt* tunazozipata kwenye nishati asilimia kubwa ni kutokana na gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaeleze Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa hivi Kinyerezi peke yake tuna uwezo wa kupata zaidi ya *megawatt* 700. Hapo nyuma tulikuwa tunapata *megawatt* chini ya 300. Lakini kwa sababu tunataka gharama za umeme zishuke na haziwezi kushuka kama hatuzalishi umeme wa gesi na umeme wa maji, niseme tu kwenye upande wa umeme wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kina cha maji cha Mtera kinatosha, kinaongezeka, leo tuna milimita 697 kati ya 698 ambalo ni ongezeko kubwa linatupatia uhakika kwamba tutakuwa na umeme wa kutosha tunakoelekea. Kihansi kati milimita 1,190 tuna milimita 1,782, tunapungukiwa kidogo. Kidatu tuna milimita 471 kati ya milimita 478, kwa hiyo tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa ambayo nataka niwaeleze wananchi ni kupungua kwa gharama za umeme. Mwezi huu gharama za umeme zilizokuwa zinakwaza wananchi tumeondoa gharama za maombi ambayo ilikuwa ni shilingi 6,000.00. tumeziondoa, kadhalika tumeondoa gharama za kufanyiwa *service (service charge)* ambazo pia zilikuwa zinakwaza sana wawekezaji. Lakini wananchi wa vijijini sasa hivi gharama ambayo wanaweza kuwa nayo kimsingi kwa umeme wetu wa *REA* ni bure isipokuwa *VAT* ya shilingi 27,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni juhudi kubwa sana ya Serikali. Na niwahakikishie wananchi kwamba kwa sasa, niongezee japo kidogo jambo ambalo liliulizwa jana kwa Wizara ya Mambo ya Ndani, kwamba wazee wetu sasa hivi inaonekana kuwa wana macho mekundu kwa sababu ya kupuliza kwenye moto. Sasa hivi moto unaokuja sasa siyo wa kupuliza, ni wa umeme wa kukandamiza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi kwamba kutakuwa na umeme vijijini, wataweza kujenga viwanda vidogovidogo kama ambavyo wanafanya nchi nyingine za Thailand na China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba juhudi za maksudi zinaelekezwa kwenye umeme, pia juhudi za maksudi kuendeleza viwanda vidogo vidogo kwa kutumia umeme itaongezeka kwa kiwango kikubwa. Kama mnavyofahamu sasa hivi tunatarajia, kwenye bajeti yetu tutaeleza kwa upana zaidi, tunatarajia kwenye Awamu hii ya Tatu inayokuja tuunganishe umeme zaidi ya vijiji 6,000, ukiunganisha nguvu hiyo kwa wananchi wa vijijini kwa namna yoyote ile mwenye kuweza kusuka nywele kwa kutumia umeme atatumia umeme. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kalemani naomba umalize, muda wako umekwisha.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa George Mcheche Masaju, *Attorney General*!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu anayetuwezesha Wabunge kutekeleza majukumu yetu hapa kama ambavyo tunamuomba kila siku wakati wa dua. Baada ya kusema hayo pia niseme moja kwa moja kwamba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge ambao kwa kutumia haki zao za Kikatiba wameamua kuchangia uboreshaji wa Mpango huu wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano ambao ni Mpango halali Kikatiba na kisheria.

Ninaunga mkono moja kwa moja hoja hii ya Mpango huu wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kutoa ufafanuzi na kushauri baadhi ya maeneo ya Kikatiba na kisheria ambayo yameguswa wakati Waheshimiwa Wabunge wakichangia hapa Bungeni. Moja ni hoja ya kwamba ilipaswa Mpango huu uletwe pamoja na Muswada wa sheria. Naomba kushauri kweli kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(3)(c), inaeleza kwamba Bunge hili litajadili mpango wa muda mrefu au wa muda mfupi na kutunga sheria, lakini pia Ibara hiyo 63(3)(d) inaelekeza juu ya kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kutungwa kwa sheria. Kwa hiyo Ibara hizi lazima zisomwe zote pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niseme hivi, tayari ipo sheria mahsusi ya kusimamia utekelezaji wa mpango, uwe wa muda mrefu au wa muda mfupi, na hii ni Sheria ya Tume ya Mipango ya mwaka 1989. Ukisoma ile Sheria Kifungu cha 5 kinachoelezea ile kazi ndiyo unaona sasa kazi ya Tume ya kusimamia utekelezaji, vipimo, ile *monitoring and evaluation* hiyo ni sheria ya jumla inayosimamia utekelezaji wa mpango wowote ule, uwe wa muda mrefu au wa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 tuliyoipitisha Waheshimiwa Wabunge hapa, ukisoma vifungu, kuanzia kifungu cha 7, kifungu cha 8, 9, 11, 13, 15, 19, 21, 20 na 26 na 32 vinaeleza vizuri. Lakini zaidi ya hizi sheria Bunge lenyewe kwa mujibu wa Katiba limepewa mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa Mpango wowote ule ni wakati huo linapojadili bajeti kwa kipindi kama hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hakukuwa na sababu ya kuja na Muswada wa sheria mahsusi wakati unapoleta mpango hapa, kwa sababu hata Mpango wenyewe haujapitishwa sasa utauleteaje na Muswada wa sheria? zaidi ya hizi Sheria zipo sheria hii ya bajeti imetaja vizuri katika vifungu nilivyovisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huu wa miaka mitanp una nyumbuliwa katika Mpango wa mwaka mmoja mmoja na Mpango wa mwaka mmoja mmoja huu ndiyo unatengenezewa bajeti na ili Mpango huu upitishwe, ili utekelezwe ndiyo unatungiwa sheria ya *Finance Act*. Lakini pia unatungiwa Sheria ya *Appropriation Act* na Sheria nyinginezo. Zaidi ya hapo Mpango huu unatekelezwa kwa kusimamiwa na sheria mbalimbali za kisekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wenyewe maana yake ni nini? Mpango ni mkakati wa Kikatiba na kisheria wa kukuza uchumi na mapato ya Serikali kwa ajili ya kuleta Maendeleo ya Wananchi. Kwa sababu hiyo, zipo na

sheria mbalimbali nyingine za kisekta ambazo zinasimamia utekelezaji wa Mpango. Kwa hiyo hakukuwa na sababu ya kuleta muswada mahususi kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nizungumze juu ya Zanzibar, Uchaguzi wa Zanzibar ulifanyika kwa amani na kuwepo kwa majeshi Zanzibar, suala la ulinzi na usalama ni la Muungano. Kwa hiyo, Majeshi yaliyopo Zanzibar yalisimamia amani na utengemano Zanzibar, kwa sababu ni suala la Muungano siyo kwamba watu wamepelekwa tu kule na ndiyo maana uchaguzi ukafanyika kwa amani na utengamano. Mkuu wa Mkoa wa Pemba aliyetoa maagizo yale aliyatoa kihalali pia chini ya Sheria ya *National Security Council*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge, wamezungumza juu ya kufanyiwa ukaguzi juu ya Deni la Taifa, hii ni mamlaka ya wazi kabisa ya *Control* And *Auditor General* iko pale hawezi kuzuiliwa hiyo haikupaswa kuletwa hata kuzungumziwa humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie kuhusu Mheshimiwa Rais. Ukisoma Ibara ya 35 wamezungumza juu ya *Good Governance* ya utendaji wa Rais. Ibara ya 35 ya Katiba inasema hivi shughuli zote za utendaji katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitatekelezwa na watumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais. Ibara ya 36 inampa Rais kuteua viongozi hawa wote na kusimamia hata nidhamu yao hata kama kuna mamlaka nyingine imesema nidhamu yao itasimamiwa na mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Ibara 36(4) haimnyimi Rais kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wanaokiuka maadili yao. Kwa hiyo, haya ndiyo ambayo wananchi wanataka. Kama sisi watumishi wa umma wajibu wetu ndiyo tunatekeleza majukumu yetu kwa niaba ya Rais, Rais hayuko tayari kuangushwa na watumishi ambao hawafanyikazi kwa kuzingatia sheria. anachokifanya Rais anamsimamisha hata kukiwa na tuhuma ya hadharani kama ya juzi hakumfukuza moja kwa moja, alisema asimamishwe akachunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuchunguzwa mtu anaweza akajitetea hajachukua nafasi ya mtu kwamba labda anaingilia nafasi ya mtu yeyote, vyovyote vile mtu anaweza akaenda Mahakamani. Kwa hiyo, niliona niyaseme hayo kwa sababu ya muda mfupi ulionipatia lakini pia ningechukua nafasi hii…

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji Kumalizika)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, basi naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita Waziri Mtoa Hoja , nitamuita Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango, ili aweze kutoa hitimisho lake naye kwa muda wa dakika 20.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano, 2016/2017 hadi 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ili kuchangia hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango tarehe 20 Aprili, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kwa kuniamini na kunichagua kuwa Naibu Waziri wa Wizara wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda natoa shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kondoa, kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mbunge wao. Nawaahidi kwamba sitawaangusha kwa yale yote niliyowaahidi.

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao walichangia hoja hii kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mpango wa kuyafikia malengo tarajiwa. Serikali imepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wote na itaufanyia kazi kadri itakavyoonekana inafaa kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilizotolewa ni nyingi lakini nitajikita katika kufafanua baadhi ya hoja hizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza, uwepo wa vipaumbele vingi na vinavyofanana kwenye Mipango ya Maendeleo tokea uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa vipaumbele vingi na vinavyofanana tangia uhuru kumetokana na lengo na nia ya Taifa katika kupunguza umaskini nakufikisha nchi kwenye uchumi wa kati. Hata hivyo Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano umeainisha maeneo manne ya vipaumbele ambayo ni haya yafuatayo:-

(i) Kukuza Maendeleo ya viwanda;

(ii) Maendeleo ya watu na mabadiliko ya jamii; na

(iii) Kujenga mazingira wezeshi kwa biashara na uwekezaji katika viwanda pamoja na vile vinavyowezesha utekelezaji wa Mpango wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilisema Serikali ijikite katika kufadhili miradi ya maendeleo ambayo haiwavutii sekta binafsi kuwekeza. Serikali imedhamiria kutanzua vikwazo vya maendeleo kwa kujenga miundombinu msingi ikiwemo ya nishati, barabara, maji na reli ili kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa sekta binafsi kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu hii ni ya gharama kubwa kama tunavyofahamu na hivyo mara nyingi Serikali inachukua jukumu la kuitekeleza. Mpango wa Kwanza ulianza kutekeleza maeneo haya kama njia muhimu ya kufungua fursa za kiuchumi na Mpango wa Pili unalenga kumalizia pale tulipoishia kwenye Mpango wa Kwanza na kuendelea kutekeleza maeneo mengine manne mapya kama nilivyobainisha hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, bado sekta binafsi ina nafasi pia ya kuweza kushiriki katika uwekezaji huu mkubwa maalum utakaowezesha sekta binafsi na wananchi kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu ilikuwa Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuwaandaa wananchi katika kutumia shilingi milioni 50 kwa kila kijiji na jinsi ya kurejesha fedha hizo. Baraza la Taifa la Uwezeshaji limepewa jukumu la kuandaa mfumo mahsusi utakaotumika katika kugawa na kusimamia fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za kiuchumi kutegemeana na fursa za vijiji husika. Kazi hiyo inaendelea na kila kijiji kitapatiwa utaratibu na mfumo huo mara utakapokuwa tayari chini ya usimamizi wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja namba nne, uchumi unakua lakini maisha ya watu wa kawaida yanazidi kuwa magumu. Sekta zinazochangia kukua kwa uchumi wa Tanzania kwa kiwango kikubwa ni sekta ambazo zinaajiri idadi ndogo ya watu. Baadhi ya sekta hizo ni ujenzi ambao inakua kwa asilimia 15.9; biashara na matengenezo kwa asilimia 10; usafirishaji na uhifadhi mizigo asilimia 12.5 na fedha na bima asilimia 10.8 kwa takwimu za mwaka 2014. Sekta inayoajiri idadi kubwa ya Watanzania ambayo ni kilimo inakua kwa wastani wa asilimia 3.5 kwa mwaka.

Kiwango hiki cha ukuaji wa sekta ya kilimo ni kidogo hivyo hauwezi kupunguza kiwango cha umaskini kwa haraka. Pia katika kipindi cha zaidi ya miaka 10 iliyopita tuliwekeza zaidi kwenye misingi ya kiuchumi na mazingira rafiki yanayofungua fursa za kiuchumi na kuchochea uwekezaji kama vile elimu na miundombinu ya barabara. Matokeo yanayoakisi uwekezaji huu huonekana baada ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tafiti mbalimbali zinaonyesha kwamba ili kiwango cha umaskini kiweze kupungua kwa kasi wastani wa kiwango cha kukua kwa uchumi katika kipindi cha zaidi ya miaka 10 kinatakiwa kisiwe chini ya asilimia 10 kwa mwaka. Hivyo basi, wastani wa ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa asilimia 6.7 kwa mwaka hautoshi kupunguza kiwango cha umaskini kwa haraka kama ambavyo imekuwa ikielezwa na wadau wengi wa maendeleo.

Mwisho, tunapoangalia viashiria vya kupunguza umaskini hatuangalii kimoja tu cha ukuaji wa uchumi. Pamoja na viashiria vingine, tunaangalia pia kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012; kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu ilikuwa ni asilimia 2.7 kwa mwaka. Ukuaji huu wa idadi ya watu ni kubwa na hivyo ni changamoto kwa Taifa hususani pale tunapochukua hatua za kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tano, Serikali haijawahi kufikia lengo la kutenga asilimia 35 ya mapato yake ya ndani jambo ambalo limeacha miradi mingi kutokamilika kutokana na kutegemea fedha za wahisani ambazo hazitolewi kwa wakati. Katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo Serikali ilitenga fedha za maendeleo kwa asilimia 27 kwa mwaka ikilinganishwa na lengo la wastani wa asilimia 35 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti una changamoto mbalimbali kama tunavyofahamu ikiwa ni pamoja na mapato kuwa chini ya makadirio na sehemu kubwa ya matumizi kuelekezwa kwenye matumizi ya kawaida. Kama Serikali, changamoto hii tumeiona na ndiyo maana kwa bajeti ya mwaka 2016/2017 tumeamua kuongeza bajeti ya maendeleo kutoka asilimia 27 hadi asilimia 40. Ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge, mtatuunga mkono uamuzi wetu huu wa Serikali mara tutakapo wasilisha rasmi makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya sita, huduma za masuala ya fedha ni muhimu ziimarike mabenki mengi ya biashara pamoja na Benki ya Kilimo zipo mjini wakati walengwa wako vijiji hakuna huduma. Huduma za mabenki ya

kibiashara zimejikita zaidi maeneo ya mjini kufuatia uwepo wa shughuli nyingi za kiuchumi na hivyo kuwa rahisi katika utoaji wa huduma za amana na mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Benki ya Kilimo kilichoanzishwa ni Makao Makuu tu ya benki hii na sasa Serikali inajipanga kuanzisha matawi Mikoani na katika Kanda mbalimbali kulenga wateja walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya saba, kilimo kufuatia umuhimu wake kiuchumi, kitaifa na maisha ya kaya na mtu mmoja mmoja kingekuwa ni miongoni mwa maeneo ya kipaumbele ya Mpango. Kwa maana nyingine ni kuwa Mpango unapaswa kuwa na mikakati kamili ya kutekeleza azma ya kuendeleza sekta ya kilimo kuliko kuwa na kauli mbiu zisizotekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huu kama ilivyo dhima yake unatilia mkazo maendeleo ya viwanda ili kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kipaumbele ya Mpango yamebainisha kwa kuzingatia dhima hii ya mpango yaani kusukuma kasi ya maendeleo ya viwanda kwa maendeleo ya uchumi na maendeleo ya jamii ya Watanzania. Njia pekee ya kufikia azma hii ni kuwa na mfumo wa maendeleo ya viwanda, unaotoa fursa kwa wananchi wengi kushiriki katika maendeleo tarajiwa. Wananchi wengi nchini wanaishi kwa kutegemea kilimo kwa tafsiri pana zikihusisha kilimo cha mazao, ufugaji, misitu na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya yote yamebainishwa kuwa kama ya kipaumbele katika ukurasa wa 43 hadi 44 kwa kitabu cha Mpango na umuhimu wa kuhusisha kilimo tunafahamu katika maeneo ya kipaumbele umezingatia yafuatayo: -

(i) Fursa kubwa ya maliasili za uzalishaji kwa maendeleo ya kilimo;

(ii) Uwezekano kwa wananchi waliowengi kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kama wazalishaji wa malighafi na upatikanaji wa chakula kwa wafanyakazi wa viwandani na wakazi wa mijini; na

(iii) Kupanua soko la ndani kwa bidhaa za viwandani kama walaji, wazalishaji zana za kilimo na pembejeo na pia kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ili kilimo kiweze kuchangia katika uchumi ni lazima tija ya uzalishaji iongezeke na ili uongezeke Mpango umejielekeza katika kuongeza tija ya kilimo kwa mambo yafuatayo:-

(i) Kubadili kilimo kuwa cha kibiashara;

(ii) Upatikanaji wa mitaji;

(iii) Upatikani rahisi na kwa wakati wa pembejeo;

(iv) Kufungamanisha kilimo na sekta ya viwanda ili kuimarisha soko la ndani la bidhaa za kilimo; na

(v) Kuimarisha huduma za utafiti, ugani, na masoko ya mazao yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa kipekee niwaombe wadau wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, kuendelea kutuunga mkono na kushiriki katika jitihada za kujenga na kuimarisha uchumi wetu. Pamoja na mipango mizuri tulionayo ni dhahiri kuwa maendeleo hayapatikani kirahisi wala siyo ya kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo yanahitaji nidhamu katika uwajibikaji kwa kufanyakazi kwa bidii, maarifa, ubunifu na ufanisi katika kufanikisha utekelezaji wa mipango na programu za maendeleo. Tushirikiane sote kwa pamoja katika kutafsiri mapendekezo ya Mpango na bajeti ya Serikali yaliyowasilishwa mbele yetu ili yawe shirikishi na yenye kutekelezeka kwa manufaa ya wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ni wadau namba moja katika ufanisi wa utekelezaji wa Mpango huu wa Pili wa maendeleo uliowasilishwa mbele yetu. Tanzania yenye neema inawezekana chini ya Serikali inayoongozwa na Kiongozi shupavu na mwenye uthubutu kama Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu pia maendeleo ni mchakato na tayari tulishaanza mchakato huu tunaomba mtuunge mkono, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu katika utekelezaji wa kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Hapa Kazi tu!

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Philip Mpango.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniruhusu kusimama hapa ili kuweza kuhitimisha mjadala wa Bunge lako Tukufu kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kuanzia 2016/2017 mpaka mwaka 2020/2021.

Pili, nikushukuru wewe binafsi, pia Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha vizuri majadiliano kuhusu Mpango huu ambao niliuwasilisha tarehe 20 Aprili, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua michango iliyotolewa kwanza na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, lakini pia Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, ambaye ni Naibu Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia ama kwa kuzungumza au kwa maandishi. Ukiacha Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, jumla ya Wabunge 44 wamechangia hoja yangu ambapo Waheshimiwa Wabunge 34 wamechangia kwa kuzungumza na 10 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi na kwa niaba ya watumishi wenzangu wa Wizara ya Fedha na Mipango, tumefurahishwa sana na mjadala juu ya Mpango huu ulivyoendeshwa. Kwa ujumla sisi tunaona kwamba mjadala umechukua mwelekeo wa Tanzania kwanza ambapo hoja nyingi zilizotolewa zilitanguliza zaidi maslahi ya Taifa. Ni matarajio yangu kwamba mwelekeo huu utaendelezwa katika majadiliano yote ya Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sehemu kubwa michango ilikuwa yenye tija ikilenga kuboresha Mpango wenyewe, lakini pia kulikuwa na michango ya kukosoa ili kujenga *(constructive criticism)* na mingine ilikuwa ni ya kuomba ufafanuzi ili kuongeza uelewa. Nafikiri huu ndiyo utaratibu ambao Watanzania wangependa kuona ndani ya Bunge lao na nawapongeza kwa dhati na kuwashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wachache ambao walichukua mkondo tofauti na baadhi walichangia kwa jazba. Ninaomba wajiangalie tena na wabadilike na hasa huku tunakoendelea na Bunge hili la Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba niwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ufafanuzi mzuri wa hoja ambazo zinagusa sekta wanazoziongoza. Nafikiri hii inathibitisha kuwa Serikali yenye dhana ya Hapa Kazi tu inazingatia siyo tu uwajibikaji lakini pia *teamwork*. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nirejee kwa kifupi masuala kadhaa ambayo yalisisitizwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tumesikia msisitizo mkubwa sana juu ya kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani na ni kweli hiki ni kipaumbele kikuu cha Serikali ya Awamu ya Tano. Tumesikia mmesisitiza umuhimu wa kupanua wigo wa mapato, kwamba Serikali ibuni vyanzo vipya na kujumuisha sekta isiyo rasmi katika mfumo wa kodi na tuangalie sekta zinazoibukia. Tumesikia kwamba ipo haja ya kuchukua hatua madhubuti kuziba mianya ya kukwepa kodi na tozo mbalimbali na hasa kwenye sekta ambazo zinakua haraka kama mawasiliano *(telecommunications),* madini na sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia umuhimu wa kuimarisha matumizi ya vyanzo mbadala vya mapato kama vile hati fungani za miundombinu *(local government bonds)*. Pia ushirikiano wa taasisi za fedha katika kukopesha *(loan syndications)*. Mkazo umewekwa kwenye maeneo ambayo bado tunaweza tukakusanya vizuri zaidi na hasa mapato yanayotokana na rasilimali za nchi yetu, ikiwa ni pamoja na rasilimali za bahari, ardhi, misitu na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikiliza ushauri kwamba ni lazima sasa zoezi la kutathimini uwezo wa kukopa *(credit rating)* ili kupanua wigo wa sekta binafsi na Serikali kukopa, hili tumelisikia. Ipo pia haja ya kuboresha baadhi ya sheria ikiwemo ile ya mikopo, dhamana na misaada, namba 30 ya mwaka 1974.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia msisitizo kuhusu umuhimu wa kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji na Waheshimiwa Wabunge wamesisitiza sana tuhakikishe upatikanaji wa malighafi; kuendelea kujenga na kuimarisha miundombinu yetu kwa ajili ya viwanda vilivyopo na tunavyotarajia vianzishwe, wamesisitiza upatikanaji wa ardhi kwa maendeleo ya viwanda katika mikoa yote na miji yote na kushughulikia changamoto ambazo zilijitokeza katika kutekeleza Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Waheshimiwa Wabunge, wamesisitiza umuhimu wa kutoa kipaumbele kwa sekta ya kilimo, kama msingi wa maendeleo ya viwanda, kilimo cha umwagiliaji, umuhimu wa kuimarisha masoko ya mazao na upatikanaji wa bei nzuri kwa wakulima wetu. Tumeendelea kupokea ushauri kuhusu umuhimu wa

kuongeza mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo na pia Benki ya Wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umetolewa ushauri mbalimbali kwamba iko haja ya kuimarisha Mpango huu upande wa mikakati ya kuendeleza viwanda ikiwa ni pamoja na kulinda viwanda vya ndani, kuhakikisha tunaongeza thamani ya bidhaa tunazozalisha viwandani, pia kukamilisha tathimini ya viwanda vilivyobinafsishwa ili kuweza kuviendeleza na kufufua vile ambavyo vimekufa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesisitiza uboreshaji wa rasilimaliwatu na hususani tuhakikishe kwamba rasilimaliwatu inaendana na mahitaji ya viwanda. Kwa kuboresha mitaala ya elimu na kadhalika. Pia kufanya jitiahada ya kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja na mitaji kutoka nje. Kwa kweli nawashukuru sana kwa michango hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe ufafanuzi wa hoja chache, nikitambua kwamba siyo rahisi kufafanua hoja zote ambazo zilisemwa au kuandikwa. Kama ulivyosema nitatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya hoja kuongezea pale ambapo Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri walipoishia.

Moja, kulikuwa na hoja kwamba namna gani Mpango umejikita katika kupunguza utegemezi?

Mheshimiwa Naibu Spika, utegemezi una madhara mengi sana ikiwa ni pamoja na kukosa uhuru. Naomba uniruhusu nitoe mfano wa kule nilikozaliwa. Akinamama kutoka Mkoa wa Kigoma wanafahamu vizuri kwamba ukiazima kitenge cha rafiki yako, ukaenda harusini na umefuatana naye, basi pale unapojimwaga mara nyingi anakukumbusha kwa kusema; "ucheze vizuri usije ukachana kitenge changu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli utegemezi unaendana na masharti na wao wenyewe wanasema *there is no free lunch*. Baadhi ya wafadhili wanaingilia hata maamuzi ya mambo yetu ya maendeleo. Upatikanaji wa hizi fedha za misaada hauna hakika na hivyo ni lazima kuchukua hatua kupunguza utegemezi kwa kuongeza kiwango cha fedha za ndani kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunafanya hivi. Mwaka 2011/2012 tulitenga shilingi trilioni 1.87 kwa ajili ya maendeleo, lakini kufikia mwaka huu wa fedha tunaomalizia tulikuwa tumetenga shilingi trilioni 4.2 na nia yetu kwa kweli ni ya dhati kabisa. Ni lazima tuendelee kuongeza fedha yetu ya ndani ambayo tunaitumia kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana wakati nikiwasilisha mapendekezo ya ukomo wa bajeti nilisema wazi na ninarudia, tumeamua kutenga shilingi trilioni 8.7 kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha ambayo ni asilimia 40 ya bajeti yote kwa ajili ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, bado tumeendelea kuwa na dhamira ya dhati ya kuongeza kiwango cha makusanyo ya mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi. Kwa hiyo, mwaka 2014/2015 wastani wa makusanyo ya kodi katika Pato la Taifa ilikuwa ni asilimia 12.01 mwaka 2020/2021 ambao ndiyo mwisho wa Mpango niliouwasilisha dhamira yetu ni kwamba sasa ifike asilimia 18 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tumeendelea kupunguza matumizi ya Serikali yasiyo ya lazima na kuelekeza hizo fedha kwenye maendeleo, lakini hasa kwenye ujenzi wa viwanda ambapo maana yake tunajenga uwezo wa nchi yetu kujitegemea zaidi na hatimaye tuweze kuondokana kabisa na utegemezi. Tumesisitiza umuhimu wa kujenga mazingira ya uendeshaji biashara na uwekezaji nchini na hiyo yote ni dhamira kwamba, hatimaye tutakapokuwa tumekuza uwekezaji nchini tutakuwa tumejinasua kwenye utegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie hoja hii tu kwa kusema na kuwahakikishia Watanzania kuwa dhamira ya Serikali yetu ya kuondokana na utegemezi, ni thabiti kabisa na wale wenzetu wanaotaka tuendelee kubebwa hadi uzeeni mimi nawasihi wajitambue maana dunia imebadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tunataka uhusiano wa kibiashara na washirika wa maendeleo, tunataka uhusiano wa uwekezaji zaidi na huu ndiyo uhusiano endelevu, huu ndiyo utatuhakikishia uhuru wa kiuchumi na ndiyo uhusiano ambao unaheshimika yaani wenye *dignity* kama nchi na ndio utakaotuhakikishia *sovereignty* ya nchi yetu inabakia kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwepo hoja, kwa nini Serikali inaleta Mpango mpya wakati Mpango uliopita umetekelezwa kwa asilimia 26 tu? Kitaalam tathmini ya utekelezaji wa Mpango wowote unatumia vigezo vingi, upatikanaji wa rasilimali fedha ni moja tu ya vigezo. Viko vigezo vingi kama muda wa utekelezaji, thamani halisi ya hicho tulichopata, lazima tuangalie malengo, *outcomes and impact* (matokeo). Lazima pia tutathimini madhara yaliyotokana na utekelezaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo siyo sahihi hata kidogo kutumia kigezo kimoja tu kuhukumu Mpango kwamba haukufanikiwa. Tathimini ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano ipo na Waheshimiwa Wabunge, tuliwagawieni kitabu ambacho kimeeleza kwa kina tulivyotathimini utekelezaji. Kwa kweli tulibaini kwamba ukizingatia viashiria vingi itakapofika

mwezi Juni, 2016 utekelezaji utakuwa ni takribani asilimia 60 na tuliweka wazi sababu ambazo zilipelekea Mpango huu usifike asilimia 80 au 90. Isitoshe ulimwenguni kote hakuna Mpango unatekelezwa asilimia 100. Hata Mpango wako binafsi haufiki asiliamia 100. Ndiyo ukweli wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulibainisha sababu kubwa zilikuwa ni upungufu wa rasilimali fedha, ushiriki mdogo wa sekta binafsi na udhaifu katika usimamizi. Serikali ya 'Hapa Kazi tu' ni Serikali inayosema ukweli kwa maana ya kutaka kujirekebisha, ndiyo maana hatufichi sababu ambazo zilipelekea utekelezaji usifike kule ambako tungetaka na ndiyo maana katika Mpango huu tumesisitiza maeneo ambayo tumeona yalikuwa na udhaifu. Hivyo Mpango niliouwasilisha utaendelea kutekeleza miradi muhimu kama miundombinu, nishati, usafirishaji na maendeleo ya rasilimali watu ambayo ni lazima tuendelee kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kuwa Serikali ina mikakati gani kupata fedha kwa ajili ya ugharamiaji wa Mpango. Nafikiri nimeshalieleza. Kuna aya mahsusi katika kitabu cha Mpango ambayo inaeleza vyanzo mbalimbali kwa ajili ya ugharamiaji wa Mpango, lakini kikubwa ni lazima tuelekeze nguvu ku-*tap resources* zilizoko kwenye sekta binafsi *(PPP)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Serikali nilisema zinatumika kama chambo, Kiingereza kizuri ni *leveraging private capital*. Hiyo ndiyo itakayotupeleka mbele. Miradi mikubwa kama ujenzi wa reli ya kati, kuijenga kwa Bajeti ya Serikali nilieleza katika Bunge lililopita ni kazi ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, palikuwa na hoja kwamba kuna ukwepaji mkubwa wa kodi unaofanywa na Makampuni ya Simu. Ni hoja nzuri ambayo tunaendelea kuifanyia kazi. Lakini naomba niseme kuwa hizi hisia zipo kwamba makampuni haya hayatupatii takwimu sahihi juu ya muda wa maongezi *(airtime)* unaotumiwa na wateja na hivyo wanavujisha mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda wateja walikuwa wanatumia kadi *(scratch cards)* na hapo ilikuwa ni rahisi kuweza kufuatilia mapato ya kampuni za simu na kuhakiki au kulinganisha idadi ya kadi ambazo zilikuwa zimenunuliwa hapa nchini na zile walizokuwa wameagiza, zilizotumika na zilizobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa teknolojia imebadilika; siku hizi unaweza ukanunua *airtime* kwa njia ya kielektroniki. Sasa hapa changamoto inakuwa ni kwamba, unajuaje mauzo halisi ya muda wa maongezi kwa Makampuni ya Simu kwa siku, kwa mwezi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, simu za mkononi sasa zinatumika kwa ajili ya kusafirisha fedha na ni kwa kiwango kikubwa na haya makampuni yanapata mapato kutokana na hizo *transfers*. Serikali imefanya juhudi kupitia *TCRA* ili kuwezesha mapato haya kwa maana ya *commission charges* hasa kwa upande wa *foreign traffic* na hili limewezekana kwa kufunga mtambo ambao unaitwa *TTMS (Telecommunication Traffic Monitoring System)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo tulilonalo ni kwamba mfumo huu umetusaidia sana kujua hayo mapato kwa zile simu za *international*. Kazi ambayo inafanyika hivi sasa ni kuhakikisha kwamba muda wa maongezi kwa simu za ndani yaani *local traffic* nazo ziwe zinaweza kutambuliwa katika mfumo huu. Kwa hiyo, tunahitaji kuunganisha hii *TTMS* na mfumo mwingine unaoitwa *Airtime Revenue Monitoring Solution (ARMS)*. Na kazi hii itakapokamilika hapo ndipo tutaweza kuwabana na kuwa na uhakika huo wa muda ambao kwa sasa hatuwezi kuu-*capture* vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Jumamosi hii nimeitisha Mkutano kati yetu Wizara, Wizara ya Uchukuzi, *TCRA* yenyewe na Mamlaka ya Mapato Tanzania ili tuharakishe kazi hii ya kuhakikisha kwamba huu mfumo wa *ARMS* unakuwa *integrated* na huu wa *TTMS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme mambo mengine mawili. Moja, kuna Mheshimiwa Mbunge anasema wanawake wamesahaulika. La hasha, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba kwetu sisi tukisema viwanda, kwetu sisi tukisema umeme vijijini, tukisema maji, *focus* yetu ni akinamama. Kwa kweli Mheshimiwa Rais alinipa Naibu Waziri mwenye uwezo mwanamama. Sasa kama na yeye amejisahau nitashangaa kweli kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna hakika kabisa wala hatubabaishi akinamama ndiyo wamebeba uchumi wa nchi hii. Mpangaji yeyote wa mipango katika nchi kama ya kwetu ambaye hatambui mchango mkubwa wa akinamama katika uchumi wa Taifa, basi huyo hafai kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya kati. Naomba niseme kwamba umuhimu wa kujenga reli mpya ya kati na matawi yake yote hapa nchini hauna mjadala hata kidogo. Ni dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga reli mpya kwa kiwango cha *standard gauge* haraka inavyowezekana. Ndiyo maana pamoja na hali ngumu tuliyonayo, tumeamua kwamba tutatenga shilingi trilioni moja mwaka unaokuja kwa kuanzia tuone uwezekano wa kujenga angalau kilometa 50 mpaka 100 za reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*. Kwa sababu reli hii ni fursa itakayotuwezesha kutumia fursa pekee ya Tanzania tuliyonayo kijografia yaani ni *unravel opportunity* ambayo Taifa hili inayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya kati ndiyo itatuwezesha kuhakikisha kwamba biashara ya mazao yetu ya kilimo, ya chakula na ya biashara, uendelezaji wa madini lakini pia utalii. Vile vile kuhakikisha kwamba utangamano katika Afrika Mashariki na nchi zinazotuzunguka unaimarika na ni ukweli ulio bayana, Tanzania tunafaidi kutokana na utangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewekeza katika baadhi ya miundombinu na reli hii ndiyo itatusaidia kuhakikisha kwamba tunafaidi. Naomba nisisitize tu kwamba tatizo letu kubwa hapa nilieleza kikao kilichopita reli hii inakadiriwa ili kuijenga itatumia kati ya dola za Kimarekani bilioni 7.5 mpaka bilioni 9.0. Hizi ni fedha nyingi, siyo fedha kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *challenge* kubwa inayotukabili kama Taifa ni kutafuta *financing* kwa ajili ya kujenga reli ya kati. Mjadala siyo kuijenga, hapana. Kazi kubwa tuliyonayo ni kupata fedha. Trilioni moja hii tuliyotenga ni kuonesha *resolve* tuliyonayo kama Serikali kwamba lazima tujenge hii reli na kwa hiyo nayo tunaitumia kama chambo kuvutia wawekezaji ili waone *seriousness* tuliyonayo ya kujenga reli yetu ya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe tu, kilicho muhimu Waheshimiwa Wabunge, ni kuwa na mkakati ambao ni *credible* wa kujenga hii reli. Kwa ushauri wangu tusijidanganye kusema kwamba sisi *"lets do it alone"* tujitazame tu ndani. Tukijenga matawi ya ndani peke yake haitatosha. Hatuna mzingo wa kutosha nchini kufanya ujenzi wa reli yetu ya ndani uwe *sustainable*. Kwa hiyo, ni muhimu na niwaombe Waheshimiwa Wabunge, maana wale wanaosema tusifikirie kujenga na *extension* ya kwenda Rwanda, jamani mbona hawasemi tufunge ile barabara ya kwenda Rwanda ambayo mizigo inapita hapa. *Transit-trade* peke yake inatuingizia mapato *in foreign currency* na sasa ni sekta ya pili kwa ukubwa kutuingizia mapato ya kigeni hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwaombe tu, tutafute *strategy* ambazo ni *credible* na sidhani kabisa kwamba *strategy* ya kujenga reli inayosema haya matawi ambayo yanatupeleka nchi jirani tusijenge, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeliahidi Bunge lako Tukufu kwamba nitaleta ufafanuzi wa hoja zote tulizozipokea kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge watapata nafasi ya kuzisoma taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nihitimishe kwa kusema yafuatayo:-

Kwanza, kulihakikishia tena Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kuzingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ili

kuboresha utekelezaji wa Mipango yetu ya Maendeleo ili kufikia malengo ambayo tumekusudia. *(Makofi)*

Pia tuna dhamana ya kuleta mabadiliko makubwa kuanzia upangaji wa mipango na utekelezaji wake ili kuiwezesha nchi yetu iondoke kwenye lindi la umaskini na hasa kwa wananchi wengi ambao wanaishi vijijini, lakini hata sehemu nyingine za miji yetu. Kama nilivyosema jana asubuhi wakati nikiwasilisha hoja yangu, kila Mtanzania ni lazima atambue wajibu wake wa kufanya kazi kwa bidii, kwa uadilifu, kwa nidhamu na uzalendo wa hali ya juu ili kujenga Tanzania mpya kwa faida yetu sisi, lakini pia na vizazi vijavyo na watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kuzitaka Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, wajielekeza kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Mpango huu ili tuweze kufikia azma yetu ya kujenga uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu. Nilisema jana na narudia tena, atakayeshindwa kusimamia utekelezaji wa miradi hii tuliyoibainisha aachie ngazi. Kama hataki kuachia, tutalala naye mbele. Wananchi wetu maskini wamechoka na huu umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwahakikishie sekta binafsi ya Tanzania kwamba tumedhamiria kuboresha mazingira yao ya kuwekeza, lakini pia kuhakikisha kwamba wawekezaji wa Kimataifa nao wanafanya biashara ambayo wao wanapata na sisi tunapata. Kwa hiyo, falsafa ya Hapa Kazi Tu itahamia vilevile kwenye kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Tunawaomba wawekezaji wote wa ndani na wa nje waweke nguvu zaidi katika sekta zote, lakini hasa katika maeneo ya kipaumbele ambayo tumeyabainisha katika Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Watanzania wote watambue kwamba ni lazima tujinyime, lazima tujitume na kuvuja jasho ili kupata maendeleo tarajiwa. Wajibu wa kwanza wa kuiendeleza nchi yetu ni wa sisi wenyewe Watanzania. Akili za kutosha tunazo, Mungu alitujalia rasilimali nyingi na fursa tele. Hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na kuwa *semi-industrialize country* inapofika mwaka 2025, inawezekana kabisa hata kabla ya hapo. Tutekeleze falsafa ya Hapa Kazi Tu kwa vitendo na Tanzania mpya tutaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, kwa mujibu wa Kanuni ya 79(3), hoja imehitimishwa sasa nitawahoji.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 79(4) naamini walioafiki wameshinda. Kwa hiyo walioafiki wameshinda, hoja imehitimishwa vizuri.

Waheshimiwa Wabunge nina matangazo kadhaa hapa, tangazo la kwanza Waheshimiwa Wabunge wafuatao wanaombwa wamuone Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, chumba namba 231 Jengo la Utawala baada ya kikao hiki. Nitayasoma majina yao:-

Mheshimiwa Oscar R. Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi; Mheshimiwa Salum Salum, Mbunge wa Meatu; Mheshimiwa Omari Kigua, Mbunge wa Kilindi; Mheshimiwa Joel Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa; Mheshimiwa Jerome D. Bwanausi, Mbunge wa Lulindi; Mheshimiwa Rashid M. Chuachua, Mbunge wa Masasi; Mheshimiwa Goodluck A. Mlinga, Mbunge wa Ulanga; Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mbunge wa Mpanda; Mheshimiwa Richard Mbogo, Mbunge wa Nsimbo; Mheshimiwa Elibariki Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi; Mheshimiwa Yahaya Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi; Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mbunge wa Nanyamba na Mheshimiwa Ajali Akbar, Mbunge wa Newala Vijijini.

Wengine ni Mheshimiwa Charles Kitwanga, Mbunge wa Misungwi; Mheshimiwa Mussa Zungu, Mbunge wa Ilala; Mheshimiwa Juma Nkamia, Mbunge wa Chemba; Mheshimiwa Isack Kamwelwe, Mbunge wa Katavi; Mheshimiwa Augustine Vuma, Mbunge wa Kasulu Vijijini; Mheshimiwa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga; Mheshimiwa Suleiman Nchambi, Mbunge wa Kishapu; Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mbunge wa Kisesa; Mheshimiwa Mohammed Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji; Mheshimiwa Sadifa Khamis, Mbunge wa Donge; Mheshimiwa Haji Ameir Timbe, Mbunge wa Makunduchi na Mheshimiwa Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni Mjini.

Waheshimiwa Wabunge hao watamwona Mheshimiwa Mariam Kisangi, chumba namba 231, Jengo la Utawala baada ya kikao hiki.

Tangazo lingine Waheshimiwa Wabunge, jana kuna Mwongozo uliombwa na Mheshimiwa Juma Nkamia na maelezo niliyoyatoa ni kwamba Kauli ya Serikali ingetolea leo kwa ajili ya maelezo hayo na Mheshimiwa Mwijage, lakini Waheshimiwa Wabunge kwa shughuli tulizokuwa nazo leo na pia shughuli

tutakazokuwa nazo kesho, wakati wa kuipangia hiyo kauli hautaweza kufanyika. Kwa hiyo, kauli hiyo itatolewa siku ya Jumatatu na Mheshimiwa Mwijage.

Tangazo la mwisho, Waheshimiwa Wabunge vipaza sauti vilivyowekwa mezani kwetu ni vipya, kwa hivyo Mbunge si lazima ainame ili aweze kusikika. Hivi vipaza sauti ni vipya, kwa hiyo, hata ukisimama kama hivi unasikika. Kwa hiyo, huna haya ya kuinama ili afya za Wabunge ziweze kuwa vizuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mkiwa mnachangia huna haja ya kuinama, unaweza ukasimama na bado ukasikika kwa sababu ya aina ya kipaza sauti kilichowekwa.

Baada ya matangazo hayo, Waheshimiwa Wabunge naahirisha Bunge hadi siku ya Ijumaa tarehe 22 Aprili, 2016, saa tatu asubuhi.

(Saa 1.31 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 22 Aprili, 2016, Saa Tatu Asubuhi)